**1 JUNI, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 1 Juni, 2023

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Hati za kuwasilisha Mezani.

### HATI ZILIZOWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**SPIKA:** Ahsante sana, Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Maswali kwa Waziri Mkuu.

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali kwa Waziri Mkuu nimwite sasa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kuja kujibu maswali ya Wabunge. Tutaanza na Simon Songe Lusengekile Mbunge wa Busega.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kunipa nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tuna sera ya *Cooperate Social Responsibility (CSR)* kwa jamii yetu inayotoka kwenye makampuni, mashirika, wawekezaji na wakandarasi mbalimbali; lakini fedha hizi zimekuwa zikifika zinacheleweshwa sana kutumika. Leo tunaomba kauli ya Serikali juu ya ucheleweshwaji wa matumizi ya fedha hizi za *CSR?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabla sijaanza kujibu swali la Mheshimiwa Songe Mbunge wa Busega, Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania wenzangu mnajua leo tarehe 01 timu yetu ya *Dar Young Africans* ambayo inapeperusha bendera ya Taifa itaondoka muda mfupi ujao uwanja wetu wa Dar es Salaam kuelekea nchini Jijini Algiers kwa ajili ya mchezo wa pili wa fainali. Naamini sote na tuendelee kila mmoja kwa dhehebu lake tuiombee timu yetu ya *Dar Young African* iweze kushinda mchezo huu wa pili kwa magoli mengi ya kutosha ili Watanzania tuweze kuwa mabingwa. Timu yetu ina uwezo mkubwa, muhimu zaidi tuwaombee wachezaji wetu, na mchezo wa tarehe 03 naamini watanzania tutakuwa kwenye *sceen* kuiombea na tunaamini tutashinda na watarudi na kombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili niungane na Watanzania kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ametoa usafiri wa ndege unaobeba wachezaji, viongozi na wapenzi kadhaa pamoja na viongozi wa Serikali kuisindikiza timu yetu ya *Dar Young*

*African* kwenye mashindano hayo muhimu kwa Taifa letu. Tunatamani sana ushindi huu upatikane mkubwa ili tujenge historia ya kupata kombe hili kwa mara ya kwanza nchini Tanzania. Mwenyezi Mungu awajalie safari njema pia mchezo mwema, mafanikio makubwa kwenye michezo hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijibu swali la Mheshimiwa Songe Mbunge wa Busega kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali tunayo sera ya *CSR* fedha ambayo inapatikana kutoka kwenye mashirika, makampuni na kwa wawekezaji waliowekeza na kufanya shughuli kwenye maeneo yetu kwa kutoa sehemu ya fedha. Iko sheria imetaja na asilimia, sina kumbukumbu ya haraka, lakini fedha ile inatolewa kwenda kwenye jamii iliyoko jirani na mradi huo au uwekezaji huo ulipo kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo. Fedha hii inapotolewa inapoenda kwenye kijiji au halmashauri inapaswa kuingia kwenye mfuko wa mapato ya ndani ya kijiji au halmashauri ili iweze kuratibiwa na kupangiwa miradi ya kufanya kulingana na mahitaji ya jamii yenyewe; na fedha hii inapoingia kwenye mfuko kama mapato manake lazima inaingia kwenye bajeti, inapangiwa matumizi.

Mheshimiwa Sika, na kwa hiyo fedha ikiingia lazima itumike katika kipindi cha mwaka. Hata kama itakuwa imechelewa kuingia lakini wakati wanapofanya mabadiliko madogo ya bajeti ndogo na yenyewe lazima ziingizwe. Kwa hiyo fedha hii inapoingia inakuwa inaingia kama sehemu ya bajeti na ikiwa sehemu ya bajeti ni lazima itumike. Kwa hiyo Serikali inasimamia hili kupitia halmashauri zetu kwa sababu miradi inakuwa kwenye wilaya, vijiji; na pindi fedha hii inapoingia mamlaka husika zinazopanga matumizi lazima zipangie matumizi.

Mheshimiwa Spika, tunajua baadhi ya halmashauri zinazopata bahati kuwa mashirika haya, makampuni haya ya uwekezaji wanapopata fedha hii wanaiona kama ni fedha nje ya bajeti na kwa hiyo upangaji wa matumizi yake unachukua muda mrefu na mwisho wanaingia kwenye migogoro. Sasa nitoe maelekezo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI

yuko hapa, na wanufaika wakubwa wanakuwa ni halmashauri ya wilaya au vijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pindi tunapopata makampuni au wawekezaji na wanatoa gawio hili la maendeleo ya jamii na linaingia kwenye halmashauri basi fedha hii isimamiwe na maelekezo yatoke, wale maafisa masuhuli kwa maana ya mkurugenzi lazima azitambulishe kwenye Baraza la Madiwani. Baraza la Madiwani lipange utaratibu na utaratibu ule uende kwenye miradi moja kwa moja ili wananchi waweze kunufaika kwa mradi waliotamani wao kuujenga, na itaingia pia kwenye kaguzi mbalimbali. Kwa hiyo mkaguzi wa ndani wa halmashauri anawajibika moja kwa moja kufuatilia matumizi ya fedha hizo. Tukifanya hili litaanza kuleta manufaa.

Mheshimiwa Spika, na sisi Serikali tunajua fedha ikiingia huko inatumika kama ilivyokusudiwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde Mbunge wa Mvumi.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na mimi kunipa nafasi hii ya kuuliza swali Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kassim Majaliwa Majaliwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya kazi kubwa sana ya ujenzi wa vituo vya afya nchini. Sambamba na kazi hiyo vilevile Serikali imepeleka vifaa tiba takriban kwenye vituo vyote vya afya nchini Tanzania. Swali langu, kumekuwa na upungufu mkubwa sana wa wataalam katika hivyo vituo wa kutumia hizo mashine na vifaa tiba vilivyopelekwa na Serikali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wataalam kwenye vifaa vyote ili kuweza kunusuru maisha ya Watanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Livingstone Lusinde Mbunge wa Mvumi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naungana naye, kwamba Serikali yetu kutoka awamu ya tano na sasa awamu ya sita imefanya kazi nzuri sana kwa ujenzi wa maeneo ya kutolea huduma nchini; zahanati, vituo vya afya, hospitali za halmashauri za wilaya pia mikoa na kanda, na sasa tunaimarisha pia na huduma kwenye hospitali za kitaifa. Kazi kubwa imefanywa nataka nitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maelekezo yake na kwa usimamizi wake, na sisi tunaendelea kuimarisha maeneo hayo ya utoaji huduma. Awamu ya kwanza ilikuwa ni kujenga miundombinu ya majengo. Kazi hiyo imefanywa vizuri, na tunataka tuwahakikishie Watanzania, kwamba tutaendelea kujenga vituo vya afya na zahanati kulingana na mahitaji kwenye halmashauri zetu na vijiji.

Mheshimiwa Spika, awamu ya pili ni ya kupeleka vifaa tiba na dawa, kazi ambayo sasa inaendelea kwa kasi. Baada ya majengo sasa tunaweka vifaa vya maabara, pia dawa na vifaa vingine kama vile vitanda kwenye wodi. Kazi hii pia inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua mpango wa Serikali wa kupeleka sasa watumishi. Kwa eneo hili la watumishi kazi sasa inaendelea vizuri. Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa vibali kwa Wizara ya Afya pamoja na mamlaka Serikali za Mitaa kuwaajili ya watumishi wa sekta ya afya ili kuwapeleka kwenye maeneo haya yote, zahanati, vituo vya afya na hospitali zote ili waweze kutoa huduma. Tunajua tuna maeneo mengi ya kutolea huduma, mahitaji ni makubwa kulingana na Ikama; kwa hiyo Serikali itaendelea kuajiri kulingana na uwezo wa kifedha kwa lengo la kutoa huduma kwa Watanzania kwenye maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, wakati huo tukiwa tunapewa kibali pia huku ndani tunafanya mapitiom, kwa sababu tunajua kuna maeneo mengine kuna watumishi wengi zaidi kuliko maeneo

mengine, kwa hiyo tunahamisha walikojaa na kuwapeleka maeneo na hasa kutoka maeneo ya mijini ambako kuna mrundikano wa watumishi na kwenda kwenye maeneo ya vijiji ili maeneo yote yaweze kupata huduma. Pia wale waliopo tunawaongezea uwezo kwa kuwapeleka kwenye mafunzo, semina na warsha ambazo pia zitawasaidia kuwafanya waweze kutoa huduma hii kwa urahisi zaidi. Kwa hiyo nitoe pia maelekezo kwa wakurugenzi kufanya mapitio ya kina ya idadi ya watumishi tulionao na maeneo yenye mrundikano mkubwa kuwahamisha kuwapeleka kwenye maeneo ambayo yana watumishi wachache. Malengo yetu ya Serikali huduma hizi zitolewe kwa usawa kwenye maeneo yote

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimwakikishie Mheshimiwa Lusinde kwamba Serikali inaendelea na ajira, na ajira hizi malengo yetu ni kutosheleza watumishi kulingana na ikama inayotakiwa, na Watanzania sasa waweze kupata huduma za afya kama ambavyo Serikali inataka ione Watanzania wakinufaika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Daktari Thea Medard Ntara Mbunge wa Viti Maalum, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Na mimi naomba nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu swali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mkakati wa kutekeleza miradi mikubwa kupitia *Mtwara corridor* lakini mpaka sasa wananchi hawana uelewa juu ya miradi inayojumuishwa na iliyotekelezwa angalau kwa asilimia 50;

Je, Serikali inatoa maelezo gani juu ya utekelezaji wa hiyo Miradi ya *Mtwara Corridor*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Mtwara Corridor* ambao pia na mimi mdau ni mradi ambao unaasisiwa na Serikali yetu. Mradi huu una maeneo mengi yanayotekelezwa ili kusheheneza mahitaji ya *Mtwara Corridor*. *Mtwara Corridor* inatazamiwa kuimarisha huduma mbalimbali kutoka Mtwara kuelekea Mkoani Ruvuma, na pale Ruvuma tuna Mkoa jirani wa Njombe kwa kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo haya. Kwa hiyo mikoa hii minne Lindi, Mtwara, Ruvuma pamoja na Njombe ni wanufaika wakubwa wa mradi huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza tuna mradi wa kuimarisha barabara ambayo tunayo sasa ya lami inatoka Lindi, Mtwara inafika Ruvuma kupitia wilaya zake hapa katikati za Masasi na Tunduru. Na baada ya kufika Songea Mjini Mkoani Ruvuma tuna barabara inakwenda Mbinga mpaka Mbamba Bay, na wale wenyeji mnajua na mimi nimepita huko kuona na kukagua miradi yote hiyo. Sasa tuna barabara inatoka Songea kuelekea Njombe na barabara nzuri inajengwa kutoka Njombe kwenda Ludewa na barabara kote huko tumepita na tumeona kazi nzuri inafanyika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia eneo la pili tunaimarisha bandari zetu zilizoko kwenye maeneo haya. Tumeona na wote mashahidi Bandari ya Mtwara imeimarishwa na leo inaanza kupokea meli kubwa; na lengo bandari hii iweze kuhudumia Mikoa hii ya Lindi, Mtwara mpaka Ruvuma pia na nje ya nchi kwenda Malawi na Msumbiji. Tuna bandari nyingine mbili zimeimarishwa, ile ya Mbamba Bay tumeona imeimarishwa, na bado itajengwa kubwa; lakini pia Lihuli au Litui, moja kati ya miji hii tumeona inaimarishwa. Pia Mkoani Njombe kule Ludewa Tungi kuna bandari pale; lakini pia hata Mkoani Mbeya Wilaya ya Kyela nako pia Ziwa Nyasa kuna bandari pale tumeenda na tumejenga na meli zinatoa huduma na nchi ya jirani.

Mheshimiwa Spika, pia tunataka tuimarishe kazi kubwa ya ujenzi wa reli inayotoka Mtwara kwenda Ruvuma na kwenda Mkoani Njombe kule Liganga Mchuchuma kwa ajili ya kuchukua mawe, na reli hii pia itakwenda mpaka Mbamba Bay. Kwa hiyo hii yote hii ndio inaitwa *Mtwara Corridor*, chini ya *program* ambayo

Mheshimiwa Mbunge anahitaji kujua. Kwa hiyo tumeshaanza kazi hiyo na tunaendelea.

Mheshimiwa Spika, sasa ili wananchi wajue *Mtwara Corridor* ni nini, sasa Serikali inajipanga, tunapoendelea kwenda kujenga *SGR* kutoka Mtwara mpaka mikoa ya Ruvuma pamoja na Njombe kule Mchuchuma tunaendelea sasa kujipanga kutoa elimu ya nini *Mtwara Corridor* inahitaji na namna gani wananchi watanufaika kwa fursa za *Mtwara Corridor* ili tuweze kupata maslahi mazuri kupitia *program* hii.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali tunajipanga sasa kutoa elimu, kutoa hamasa kwa wananchi kuwa tayari kupokea mpango huu wa Mtwara Korido. Kwa hiyo malengo ya Serikali bado yamebaki palepale na utekelezaji unaendelea hatua kwa hatua, na pindi utakapokamilika wananchi wote watakuwa wanajua umuhimu wa *Mtwara Corridor,* ahsante sana, *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salome Wycliffe Makamba Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kuuliza maswali kwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Waziri Mkuu naiona nia ya dhati ya Serikali kuboresha mazingira ya wachimbaji wadogo wadogo kwa hasa kwa kuwatafutia mitaji kwenye taasisi za kifedha hasa benki. Lakini benki hizi zinapokuwa zinawapa mikopo machimbaji wadogo wadogo zinawapa kwa masharti ambayo hayaendani na uhalisia wa biashara hii ya wachimbaji wadogo hasa ukizingatia musa wa uzalishaji na upatikanaji wa madini hayo.

Je, ni nini mkakati wa Serikali kutengeneza mazingira rafiki ya taasisi za kifedha ili waweze kuwapa mikopo wachimbaji wadogo ambayo itazingatia mazingira yao ya upatikanaji wa madini na mazingira yao ya uzalishaji wa madini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Salome Makamba, Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua nafasi ya Serikali katika kusimamia fursa ya wachimbaji wadogo wa madini na upatikanaji wa mitaji bila ya kuathiri utendaji wao. Serikali yetu inayo sera inayoimarisha wajasiriamali, wachimbaji wadogo wa madini, kwa kutumia fursa walizonazo kwa maeneo yao panapopatikana madini kuchimba kwa uhuru na Mheshimiwa Waziri wa Madini mara kadhaa ameeleza mpango wa Serikali wa kupima viwanja kwa ajili yao na kuwasisitiza wajitokeze kushiriki kikamilifu kwenye fursa hii ya uwepo wa madini.

Mheshimiwa Spika, tunatambua changamoto ya wachimbaji hawa ya kukosa vifaa muhimu pamoja na mitaji ya kuanzishia kazi ya uchimbaji. Serikali tuchofanya ni kuelekeza kwenye taasisi za fedha, benki kwa maana ya sekta binafsi na wale wote ambao wanakopesha mikopo na wanaotambulika rasmi upande wa Serikali, tunazo halmashauri za mikopo midogo kwa wanawake na walemavu na tuna mifuko pia ya uwezeshaji ambayo yote hii, maeneo yote haya ni fursa kwa vijana wetu kukopa. Tunatambua ipo changamoto ya masharti mbalimbali ya hizi taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, ni nini tumefanya; ni kutoa maelekezo kwa taasisi hizi. Kwanza lazima wajue huyu anayekuja kukopa anataka kufanya shughuli gani, na shughuli hii kuanzia uwekezaji wake mpaka uzalishaji wake inatumia muda gani, na kwa hiyo masharti yale lazima yalenge utendaji wa sekta hiy,o kwa sababu kila eneo lina muda wake wa uwekezaji na uzalishaji wake na kuingia kwenye masoko. Itakuwa haipendezi kama anajua kwamba mchimbaji mdogo tangu anachimba mpaka kuuza anajua ni ndani ya miezi sita halafu unampa mkopo wa miezi mitatu, utakuwa humtendei haki. Kwa hiyo basi Serikali tunachofanya tumetoa maelekezo sahihi na thabiti kwa taasisi za fedha kuzingatia *nature* ya shughuli au mradi ambao mjasiriamali anaufanya ikiwemo na wachimbaji wadogo. Sisi tunajua uchimbaji mdogo unapaa paa bila ya kuwa na uhakika kwamba

je, utapata madini yenyewe? Na ukipata madini yenyewe, na ukipata ile *process* mpaka kwenye masoko.

Mheshimiwa Spika, mara kadhaa tumeenda kuwasisitiza wajasiriamali lakini mara kadhaa tumehamasisha taasisi za fedha kufanya *study* ya uchimbaji mdogo na kuwafikia wachimbaji wadogo na kuwakopesha tena kwenye riba ndogo, ikiwezekana bila riba kabisa, ili kuwawezesha vijana wetu wajasiriamali kupata mikopo na kuitumia na hatimaye wapate faida. Mara kadhaa pia tumemuagiza Mheshimiwa Waziri wa Madini kusimamia sekta hii; na tumemuona akipita maeneo mbalimbali akizungumza na wajasiriamali wadogo pamoja pia na sekta za fedha ili kuhakikisha kwamba zinatenga fedha kwenye dirisha hili la wachimbaji wadogo ili waweze kupata mikopo yenye mazingira mazuri ya ukopaji na urejeshaji kwa lengo la kuwaondolea adha ya au kufungwa au kunyang'anywa mali zao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Serikali inaendelea kukaa na taasisi za fedha na kuzihamasisha kutenga mitaji kwenye dirisha hilo kwa masharti lakini waangalie utendaji wa sekta hiyo ili wajasiriamali waweze kupata mikopo yao vizuri. Tumeendelea pia kuwataka pia hata wajasiriamali hawa kuunda vikundi vikundi. Wakiwa kwenye vikundi ni rahisi zaidi kwa sababu taasisi nyingi zinaogopa kupoteza fedha, kwa hiyo ushirika ni mkombozi sana kwao. Na sisi tunaendelea kusimamia hasa sheria zilizosajili taasisi hizi za fedha kwa masharti ambayo hawaendi kwa kuweka riba kubwa inayomfanya yule mkopaji kushindwa kurejesha na hatimaye kuuzwa nyumba, labda kunyang'anywa au kufungwa. Kwa hiyo haya yote Serikali tunazingatia. Nataka nitoe wito kwa wajasiriamali washiriki kikamilifu na kwa uhuru mkubwa na wajenge matumaini na Serikali yao kwamba tunasimamia sekta hii ili waweze kupata maslahi kwenye sekta ya madini.

Mheshimiwa Spika, nimuagize Mheshimiwa Waziri wa Madini kufatilia taasisi za fedha zinazokopesha wajasiriamali hawa, kuwa wanapokwenda kukopesha hawaweki riba kubwa inayomuathiri mchimbaji; tunataka kila mmoja afanye kazi hii vizuri na apate faida, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu Serikali imekuwa ikitekeleza sera yake ya elimu bila malipo au maarufu kama elimu bure kwa misingi ya kuwapunguzia gharama wazazi au walezi wa vijana ambao wanasoma katika shule zetu za sekondari hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo bado kumekuwa na michango kadhaa katika shule zetu za umma, ikiwemo michango ya ulinzi, shajara pamoja na chakula;

Je, Serikali haioni umuhimu wa kupitia upya sera hii ili hii michango ambayo nimeainisha ambayo kimsingi inabebwa na wazazi au walezi iwe ni jukumu la Serikali kwa dhana ile ile ya kuwapunguzia gharama wazazi au walezi wa vijana wetu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini na mkuu wa wilaya mstaafu kama ifuatavyo: - *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Sera ya Elimu bila Bila Ada kwa lengo la kuwaondolea adha wazazi ya kuwa na michango mingi na ile michango holela, michango holela. Kila mwezi Serikali yetu inapeleka fedha kwenye halmashauri kwa ajili ya kuwezesha shule zetu za Sekondari, wale wakuu wa shule na uongozi wa shule kuweza kutumia kwenye maeneo ambayo walikuwa wanatarajia sana kupata michango kutoka kwa wazazi ili wazazi wasichangie maeneo hayo na badala yake wazazi waendelee kusimamia maboresho ya mtoto mwenyewe kwenda shule kwa kumnunulia sare, viatu na vitu vingine.

Mheshimiwa Spika, natambua kwamba si maeneo yote yameweza kupata fedha hii hasa eneo la chakula na ulinzi, kama

ulivyoeleza. Maeneo haya ambayo tumetolea fedha ni yale maeneo ambayo yanafanya ukarabati mdogo mdogo wa majengo yanayoharibika, vifaa vya kufundishia na kujifunzia, vitabu, chaki na vitu vingine ili kuondoa adha ya waalimu kuwachangisha wazazi fedha.

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo sasa tunaendelea kushughulika nalo ni maboresho sasa. Tunazo shule nyingi za sekondari ambazo wanafunzi wanaenda asubuhi na kurudi jioni na wanapokuwa shule hawapati chakula. Nikiri kwamba eneo hili Serikali bado tunaendelea kuchakata ili tuone namna nzuri ya kutoa huduma ya chakula shuleni; ingawa tumeona sekta binafsi zinashiriki, wakati mwingine wazazi wenyewe wanaweka mpango wao.

Mheshimiwa Spika, sasa, niliposema michango holela; Tunayo ile michango holela ambayo labda waalimu wanasema njoo kesho na shilingi mia mbili, elfu moja, mia tano, ambazo zinakera kwa wazazi. Hiyo tumeidhibiti na tumepiga marufuku na haipo kabisa na kama ipo, tumeshatoa maelekezo na hapa pia nitatoa maelekezo. Sisi tunaruhusu michango rasmi inayokwenda kufanya shughuli za maendeleo. Shule za msingi, shule za sekondari hizi ni shule za wananchi. Kila kijiji kina shule ya msingi na kinasimamiwa na kijiji chenyewe, na tumeunda kamati ya shule kwa shule za msingi. Sekondari ziko kwenye kata, tumeunda bodi ya shule na inamilikiwa na kata kwenye vijiji vitatu, vinne au vitano, wanasimamia na Mtendaji wa Kata ndio kiongozi wetu anayesimamia maendeleo ya shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inapotokea labda choo kimebomoka hatuzuii wazazi kukaa na kukijenga kwa kuchangia na kujenga hiyo ni michango ya maendeleo. Ingawa michango hii pia tumeiwekea masharti kidogo kwamba anayetakiwa kusimamia michango hii ni mkuu wa wilaya pekee au yeyote ambaye mkuu wa wilaya amemchagua kusimamia. Tunaogopa sasa watu kuchangisha kule holela na ndiyo kwa sababu nilisema michango holela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi Serikali inaendelea kufanya mapitio ya sera hii ili kuwezesha mzazi kupata unafuu zaidi wa kutoa michango kwa ajili ya maboresho ya shule zetu. Lakini pia bado hatuondoi nafasi ya uwajibikaji wa wananchi kwenye shule zao katika kufanya maboresho. Na niliposema mkuu wa wilaya mstaafu najua hili umelisimamia vizuri sana ulipokuwa mkuu wa wilaya kabla hujawa Mbunge na kwa hiyo Serikali tunaendelea kusimamia haya.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wakuu wa wilaya wote nchini, kwenye halmashauri zao kusimamia kutokuwepo kwa michango holela inayokera wananchi na kushindwa kufanya shughuli nyingine na badala yake kuwa wanasababisha wanafunzi wanaondolewa shuleni; hiyo tulishapiga marufuku kabisa. Lakini pia Wakurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha kwamba wanatuhudumia hizi shule lakini na kuweka mpango mzuri kwenye maeneo ambayo yanahitaji pia Halmasjhauri isimamie kupitia bajeti zao, kama ni lazima kuzungumza na wazazi lakini wazazi wenyewe kupitia kamati zao wafanye maamuzi haya ndiyo ambayo kwa sasa tunayasimamia. Lakini niwahakikishie tu kwamba ombi la Mheshimiwa Mbunge la kufanya maboresho ya sera yetu hayo tumepokea na tunayafanyia kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekuwa na mwingiliano wakati wa utekelezaji wa majukumu kati ya Wizara tatu, kwa maana Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Maliasili pamoja na Wizara ya Ardhi hasa kwenye eneo la utoaji wa *GN*. Kwa mfano, Wizara ya TAMISEMI wanatoa *GN* wakati wa uanzishaji wa vijiji, Wizara ya Maliasili wanatoa *GN* kwenye maeneo yao ya hifadhi lakini Wizara mama ambayo ni Wizara ya Ardhi pia inawajibika kwa mujibu wa sheria kutoa *GN* kwenye maeneo yote haya ya mipaka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuwa utoaji wa *GN* wakati mwingine hupelekea mogogoro ya ardhi kwenye maeneo haya. Nilitaka nijue tu Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuboresha Sera ya Taifa ya Ardhi ya ya mwaka 1995, ambayo pia itapelekea maboresho ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 ili kuondokana na kutengeneza *formality* ya utoaji wa *GN* kwa sekta moja ya Ardhi badala ya mgongano ulioko kwa sasa, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri mkuu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, maneno yake ya awali sikuyasikia vizuri naomba arudie tena ili niweze kumjibu kwa usahihi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu kumekua na mwingiliano wa kiutendaji wakati wa utoaji wa *GN* kati ya Wizara tatu kwa maana Wizara ya TAMISEMI, Wizara ya Maliasili na Wizara ya Ardhi. Nikatoa mfano Wizara ya TAMISEMI wanatoa *GN* wakati wa uanzishaji wa vijiji kwa maeneo fulani ambayo yanaweza yakawa ndani ya hifadhi, Wizara ya Maliasili nao wanatoa *GN* kwenye maeneo yao ya hifadhi wakati huo huo Wizara ambayo ni Wizara mama ambayo ni Wizara ya Ardhi nayo inawajibika kutoa *GN* kwenye maeneo hayo hayo. Kwa hiyo kunakuwa na mgongano wa Wizara tatu zote kutoa *GN* kwenye eneo moja la umiliki wa ardhi

Mheshimiwa Spika, wakati mwingine utoaji huu wa *GN* husababisha uzalisha mgogoro wa ardhi, hasa kijiji kinapopandikizwa ndani ya eneo moja la hifadhi na wote wakinwa na *GN* zinazotoka Serikalini. Nilikuwa nataka nijue sasa Serikali ina mpango gani wa maboresho wa Sera ya Taifa ya Ardhi ambayo ni ya Mwaka 1995 ambayo itapelekea maboresho pia ya Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 ili kutengeneza *formality* ya utoaji wa *GN* kwa Wizara moja ili kuondoa muingiliano wa Wizara zote tatu kutoa *GN* kwenye eneo moja la umiliki wa ardhi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, majibu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chege, Mbunge wa Rorya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hizi Wizara zote zilizotajwa na Mheshimiwa Chege, Wizara ya Ardhi, TAMISEMI pamoja na Maliasili. Tunajua zinazo sheria zinazosimamia ardhi; lakini hakuna muingiliano wa moja kwa moja kwa sababu tumejitahidi kila Wizara kuwa na majukumu yake hasa katika utoaji wa *GN*. *GN* inatolewa na Wizara moja tu. Ardhi wanalo jukumu la kusimamia sera ya ardhi nchini na inayo kujumu la kupeleka watendaji wa sekta ya ardhi wenye taaluma ya ardhi kwenye mamlaka hizi hasa mamlaka ya serikali za mitaa.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya serikali za mitaa kwa maana ya halmashauri za wilaya wajibu wake ni kusimamia matumizi, upimaji wa ardhi kwenye maeneo yao ya halmashauri, na wao ndio wanaanzisha mchakato wa upatikanaji wa hati kwa wale wanaotakiwa kumiliki. Lakini pia halmashauri hizi ndizo ambazo zinasimamia mipaka ya kiutawala. Kijiji na kijiji mipaka yake, kata na kata mipaka yake, wilaya na wilaya mipaka yake hata mkoa na mkoa. Kwa hiyo jukumu lao liko tofauti kidogo ingawa kuna mahusiano ya kiutendaji kwa kupeana taarifa baad aya mmoja kukamilisha jukumu lake.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Maliasili na Utalii wale wanahusika na maeneo ya uhifadhi maliasili zetu na uratibu wa maliasili zote nchini. Wanapokuwa na mipaka wanalazimika kwenda sasa mamlaka ya Serikali za mtaa wanalazimika pia kutoa taarifa ardhi; na mipaka hiyo inapothibitishwa na ardhi wao sasa ndio wanatoa hiyo *GN*. Tumefanya kazi kubwa kwenye migogoro mbalimbali ya mipaka kati ya maeneo mawili ya utawala, kati ya maeneo mawili ya utendaji kama wakulima na wahifadhi lakini ni vijiji na hifadhi. Na tunapokuwa na mgogoro hii ndiyo kwa sababu tunaita Wizara zote tatu; Wizara ya Ardhi, Maliasili, TAMISEMI kwa sababu kila mmoja ana jukumu lake, na huo ndio utaratibu ambao sasa hivi unaendelea Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utoaji *GN* kama vile kule Mbarali ambako baada ya muda mfupi tutatoa *GN* ile mpya baada ya *GN 28* ambayo tumeifanyia kazi sana, hiyo ndio Wizara itahusika siyo kila Wizara tu inatoa *GN*, Maliasili inatoa *GN,* Hapana, ni Wizara moja imeshapewa jukumu la kutoa *GN* Wizara nyingine ina *facilitate,* nyingine inasimamia. Kwa hiyo Wizara zetu tatu hizi wakati wote wamekuwa wakiangalia maeneo yenye mwingiliano na wanafanya marekebisho halafu tunawawekea sheria, ili kubainisha ile mipaka ya utendaji.

Mheshimiwa Spika, tutaendela kusimamia maeneo yote yenye changamoto, yenye mwingiliano ili kubainisha majukumu ya kila Wizara ili kusiwe na muingiliano ambao unaweza kuleta migogoro ndani ya Serikali. Kwa hiyo huo ndio mkakati ambao tunao ndani ya Serikali, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Ahsanteni sana.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:** Maswali ya Kawaida.

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali ya kawaida Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Buchosa, sasa aulize swali lake.

Na. 491

### Ununuzi wa Vifaa Tiba Hosptali ya Wilaya Buchosa

**MHE. ERIC J. SHIGONGO** aliuliza: -

Je, lini vifaatiba vya Hospitali ya Wilaya ya Buchosa vitanunuliwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Deogratius Ndejembi, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Eric James Shigongo, Mbunge wa Jimbo la Buchosa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 ilipeleka Bohari Kuu ya Dawa fedha shilingi bilioni 34 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwa hospitali za halmashauri 67 zilizoanza ujenzi mwaka wa fedha 2019/2020 ikiwemo Hospitali ya Wilaya ya Buchosa ambapo kila hospitali ilitengewa shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2022/2023 Hospitali ya Wilaya ya Buchosa imepokea fedha za ruzuku kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba shilingi milioni 800 pamoja na vifaa tiba vyenye thamani ya shilingi milioni 596.

Mheshimiwa Spika, taratibu za kusimika vifaatiba vilivyopokelewa unaendelea kwenye Hospitali ya Halmashauri ya Buchosa. *X–Ray* mashine tayari imefungwa tangu mwezi Aprili 2023. Tunsubiri wataalamu wa mionzi kutoka Tume ya Nguvu za *Atomic* Tanzania kukagua na kutoa kibali ili utoaji wa huduma uweze kuanza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Eric Shigongo, swali la nyongeza.

**MHE. ERIC J SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana Serikali kwa kutekeleza jambo hili ambalo kwa muda mrefu nimekuwa nikilipigia kelele, kwamba fedha milioni 500 wakati vifaa havikuwa vimenunuliwa. Sasa ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa ina mahitaji ya watumishi 166 lakini waliopo ni watumishi 39 pekee na hili linafanya vifaa hivi vishindwe kutumika ipasavyo;

Je, Serikali iko tayari kufanya *commitment* ya lini watumishi hawa watapelekwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kumbukumbu za wananchi wa Buchosa hasa katika Kisiwa cha Kome kwenye Kituo cha Afya cha Nyamisri waliwahi kuahidiwa kupelekewa *X–Ray* mpya, wakati ule Waziri wa TAMISEMI akiwa dada yangu, Mheshimiwa Ummy Mwalimu;

Je, Serikali inaikumbuka ahadi hii au imekwishakuisahau; na kama inaikumbuka, iko tayari kuitimiza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu swali la kwanza la nyongeza la Mheshimiwa Shigongo la kuhusu ni lini Serikali itapeleka watumishi katika Hospitali ya Wilaya ya Buchosa: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza ajira za sekta ya afya 8,070 nchini, na hii ni kwenda kujazia maeneo yenye upungufu wa watumushi, ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa. Hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika hawa watakaoajiriwa hivi karibuni nao watapata watumishi hawa katika hospitali ya wilaya.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la *X-Ray* iliyoahidiwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, katika Kituo cha Afya Nyamisi; tutatekeleza ahadi hii kadiri ya upatikanaji wa fedha. na tutaangalia katika bajeti ya mwaka 2023/2024 kama kituo hiki kimetengewa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba basi *x-ray* iwe kipaumbele kupelekwa kwa ajili ya kuhudumia wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Nyamagana, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Boniventura Kiswaga.

Na. 492

**Ujenzi wa Vituo vya Afya kwa kuzingatia Tarafa**

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA K.n.y. MHE. STANSLAUS S. MABULA** aliuliza:-

Je, Serikali haioni kutoa fedha za ujenzi wa vituo vya afya kwa kigezo cha idadi ya tarafa ni kuwanyima wananchi vituo vya afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula, Mbunge wa Jimbo la Nyamagana, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kati ya tarafa 570 zilizopo 211 hazikuwa na kituo cha afya hata kimoja, hivyo Serikali ilitoa kipaumbele cha ujenzi wa vituo vya afya kwenye tarafa ambazo hazina kituo cha afya. Katika mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali ilijenga vituo vya afya 234. Kipaumbele cha ujenzi kilizingatia tarafa ambazo kata zake hazikua na kituo cha afya. Aidha, ujenzi wa kituo cha afya ulizingatia kata za kimkakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Boniventura Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. BONIVENTURA D. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa, Wilaya ya Nyamagana ina tarafa moja tu, na idadi ya wananchi ni kubwa. Ukigawa kulingana na tarafa mbalimbali maana yake unawanyima fursa wananchi wa Nyamagana kupata huduma stahiki hasa walio pembezoni kule Ngwanyima na Kishiri;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuangalia, hasa idadi ya wananchi na umbali wa kupata huduma kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa hali ileile ya Nyamagana inalingana kabisa na hali ya Jimbo la Magu, hasa Kata ya Mwamanga na Kata ya Lutale;

Je, Serikali ina mpango gani wa kuziona kata hizi ambazo ziko mbali na huduma katika vituo vya afya kwenye wilaya zao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mabula; la kwanza kuhusu Jimbo la Nyamagana kuwa na tarafa moja tu.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye majibu yangu ya msingi, Serikali iliangalia maeneo ambayo ni pembezoni na yako mbali na huduma za afya kabisa na kuyapa kipaumbe na kuwa ni kata za kimkakati. Hili la Nyamagana tunalipokea kama Serikali na kuweza kuangalia ni namna gani tutapeleka timu ya kufanya tathmini na kuona vituo vya afya vya Serikali vilivyopo katika jimbo hili na kuona uwezekano wa kutenga bajeti ya kuwaongezea vituo vya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la kata hizi alizozitaja ikiwemo Kata ya Mwamanga katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kata hizi za kimkakati kote nchini, ikiwemo katika

Halmashauri ya Wilaya ya Magu. Tutaangalia katika bajeti ya mwaka 2023/2024 ni kiasi gani kimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu, ili tuweze kuanza na ujenzi wa kata hizi za Mwamanga na nyingine ambayo aliitaja Mheshimiwa Kiswaga.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge mliosimama ninawaona, lakini niwaombe sana, muda wetu ni mfupi. Nenda moja kwa moja kwenye swali, usitaje ahadi, ilitolewa na nani, usianze ulipita pale ukaahidi. Nenda moja kwa moja kwenye swali. Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniona: -

Mheshimiwa Spika, Tarafa ya Makambako inahudumia Halmashauri mbili, yaani Jimbo la Lupembe…

**SPIKA:** Swali lako Mheshimiwa? Nenda moja kwa moja kwenye swali, unataka Serikali ikujibu nini?

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, nimekuelewa. Nataka Serikali, katika Jimbo la Makambako tarafa moja ina majimbo mawili, kila tarafa iwe na jimbo lake ili Serikali inapopanga mipango ya kuhudumia tarafa tuweze kuhudumiwa vizuri kwenye Tarafa yetu ya Makambako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri vituo vya afya havitoshi kwa Mheshimiwa; kwenye tarafa zake hakuna vituo vya afya.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tunalipokea hilo na tutaangalia katika bajeti zilizotengwa tuone tupeleke kituo cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Singida Mashariki, Kata ya Misupaa pamoja na Isuna hazina vituo vya afya;

Je, ni lini Serikali itajenga vituo hivyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutajenga vituo vya afya hivi katika Kata ya Isuna na nyinginezo kule Singida kadiri ya upatikanaji wa fedha, na tutaangalia kwenye bajeti inayofuata kuona ni kiasi gani kimetengwa ili Serikali ianze ujenzi huo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Katika Tarafa ya Kipatimu Kata ya Chumo tumekamilisha ujenzi wa kituo cha afya mwezi uliopita.

**SPIKA:** Unataka Serikali ifanye nini?

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali italeta vifaa tiba, dawa pamoja na watumishi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.1 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwenye vituo vya afya mbalimbali hapa nchini, na tutaangalia katika bajeti hii ambayo imetengwa kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba hivi; kama Tarafa ya Kipatimu kwenye kituo cha afya alichokitaja Mheshimiwa Ndulane imetengwa na tutapeleka vifaa tiba huko.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, kile Kituo cha Afya cha Bweri ni kituo cha muda mrefu, lakini kimeshindwa kwisha na kwa hiyo, wananchi wa eneo lile wanashindwa kupata huduma;

Je, ni lini Serikali itamalizia hicho kituo ili wananchi wapate huduma nzuri za kituo cha afya?

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata kama kuna fedha imetengwa kwa ajili ya umaliziaji wa Kituo hiki cha Afya cha Bweri ili tuweze kumalizia, na kama haijatengwa tutaangalia katika mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**SPIKA:** Haya, ili nisiwachanganye, maana naona msipoanza na maelezo swali linakuwa gumu. Sasa, anzia kwenye swali usianze na maelezo. Wewe anza tu, lini vifaa tiba vitapepekwa kwenye kituo A, B, C, lini Serikali itajenga kituo cha afya kwenye kata A, B, C, anzia hapo.

Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. Swali lake litaulizwa kwa niaba ya Mheshimiwa Minza Mjika.

Na. 493

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Ihanu – Mufindi**

**MHE. MINZA S. MJIKA K.n.y. MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Ihanu – Mufindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali imetenga shilingi bilioni moja ambapo shilingi milioni 500 ni kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Mgololo, shilingi milioni 150 ni kwa ajili ya ujenzi wa chumba cha upasuaji kwenye Kituo cha Afya Mbalamaziwa na shilingi milioni 350 ujenzi wa Kituo cha Afya Mdabulo. Katika mwaka wa fedha 2023/2024 halmashauri kupitia mapato ya ndani imetenga shilingi milioni 562 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo la *OPD* Kituo cha Afya Ihalimba na shilingi milioni 120 ukamilishaji wa jengo la *OPD* Kituo cha Afya Mapanda.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya Afya kwenye kata za kimkakati kote nchini kikiwemo Kituo cha Afya Ihanu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

a) Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Udekwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili linatoka katika Mkoa wa Simiyu, Wilaya ya Maswa, Wilaya ya Binza;

b) Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Kata ya Binza? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, nikijibu maswali mawili haya ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Kata hii ya Budekwa ipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo. Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wake kadiri ya upatikanaji wa fedha; na tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata kama kuna fedha imetengwa, ili iweze kwenda mara moja kujenga.

Mheshimiwa Spika, nikienda kwenye swali lake la pili la kituo cha afya hiki alichokiulizia kilichoko Mkoani Simiyu, tutaangalia vilevile kuona ni namna gani kama fedha imetengwa basi iweze kwenda mara moja kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata ya Igundu na Namura katika Jimbo la Mwibara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali itajenga vituo hivi vya afya kadiri ya upatikanaji wa fedha na tutaangalia tena katika mwaka wa fedha unaofuata ili tuweze kuweka kipaumbele fedha hiyo iweze Kwenda. Na kama haipo tutatengea kwenye mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza swali la nyongeza, kama ifuatavyo: -

Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya katika Kata ya Vudee na Siji ambavyo viliorodheshwa mwaka elfu mbili na ishirini…?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika,

tutatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya Mundee na Suji kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba kwenye vituo vya afya viwili vilivyokamilika; Kituo cha Afya cha Magazini na Ligela?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata kama kuna fedha imetengwa basi tutahakikisha iweze kwenda mara moja na kama haipo basi tutatenga katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Tarafa ya Nangaru na Milola?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha inajenga vituo vya afya kwenye kata na tarafa za kimkakati kote nchini. Na tutatafuta fedha katika mwaka wa fedha 2023/2024 na kama hakuna fedha hizo basi tutatengea bajeti kwenye mwaka wa fedha 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi, je, ni lini Serikali itajenga wodi za wanaume na wanawake katika Kituo cha Afya cha Ifingo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata ili ifingo waweze kupata fedha hii. Lakini vilevile nichukue nafasi hii kuomba Wakurugenzi wa halmashuri kuwa wanatenga fedha kwa ajili ya ujenzi na umaliziaji wa zahanati na vituo vya afya kwenye halmashauri zao. Serikali Kuu imeshapeleka fedha nyingi sana kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya hivi na zahanati hizi na fedha nyingi ya vifaa tiba na wao wasaidie sasa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; je, ni lini Serikali itafungua kituo cha afya cha Kata ya Lyamugungwe na kupeleka vifaa tiba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata kama kuna fedha imetengwa, na kama bado haikutengwa basi tutatenga kwenye mwaka wa fedha wa 2024/2025.

**SPIKA:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Je, ni lini Serikali itajenga kituo cha afya katika Tarafa ya kimkakati ya Mbuji yenye kata tano?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, ni kipaumbele cha Serikali kuhakikisha inajenga vituo hivi vya afya katika kata za kimkakati. Na tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata tuweze kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya hiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Ole-Shangai, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kumalizia Kituo cha Afya Samunge, Kata ya Samunge?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata ili tuweze kutenga fedha hii ya kumalizia Kituo cha Afya cha Samunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, swali la nyongeza.

**MHE. JEREMIAH A. MRIMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya ukarabati wa Kituo cha Afya Iramba kilichochakaa sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, tutaangalia katika mwaka wa fedha unaofuata na kuipa kipaumbele kata hii na kuweza kupeleka fedha kadiri ya ilivyotengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ningependa kuuliza kuna vituo vya afya vingi nchini ambavyo havijamaliziwa *OPD*...

**SPIKA:** Swali lako?

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, ni lini *OPD* zitamaliziwa katika vitu vya afya ambavyo havina *OPD?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikipeleka fedha kwa awamu katika halmashauri mbalimbali hapa nchini kwa ajili ya umaliziaji wa majengo haya. Tunaendelea kutafuta fedha kuona ni namna gani tunapeleka kwa ajili ya umaliziaji wa majengo ambayo bado hayajakamilika. Na kwa yale yaliyokamilika Serikali inaendelea pia kupeleka vifaa tiba ili huduma kwa wananchi iweze kuanza kutolewa kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itajenga Kituo cha Afya Lupila kwa sababu, majengo yake yamechakaa sana na ni ya muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DEOGRATIUS J. NDEJEMBI):** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Kituo cha Afya Lupila kimetengewa fedha za *World Bank* na kitaenda kujengwa katika mwaka huo wa fedha. Vilevile kuna maombi maalum ya Mheshimiwa Mbunge ya Kituo cha Afya Mfumbi ambayo nayo yanafanyiwa kazi, ili kituo cha afya hicho kiweze kujengwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 494

**Kurudisha Reli ya Mtwara – Mbamba Bay**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA** aliuliza: -

Je, Serikali imefikia wapi katika mpango wake wa kurudisha Reli ya Mtwara – Mbamba Bay na eneo la Mchuchuma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Atupele Fredy Mwakibete, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa awali kwa ajili wa ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ya Mtwara – *Mbamba Bay* na matawi yake ya kuelekea Liganga na Mchuchuma. Aidha, taarifa hiyo ya upembuzi yakinifu na usanifu ilipendekeza kuwa mradi huu utekelezwe kwa utaratibu wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public Private Partnership – PPP)*.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yetu kuwa marekebisho ya Sheria ya *PPP* yatakayofanyika hivi karibuni yatasaidia kuwapata wawekezaji kwa ajili ya kujenga reli hii muhimu. Naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mheshimiwa Mbunge pamoja na wananchi wa Mtwara na Ruvuma kuwa na subira wakati Serikali inashughulikia kwani suala hili litapewa kipaumbele na Serikali katika mwaka 2023/2024 ili kukamilisha taratibu za kumpata mjenzi, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na ya kuleta tumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza;

a) Je, ni lini sasa mtaanza mchakato wa kuwashirikisha wadau kuhusu ujenzi huo?

b) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri uko tayari sasa kuambatana na Mheshimiwa Manyanya na Mheshimiwa Agnes Hokororo, ili kwenda kufanya mikutano kwenye maeneo haya mawili ili wananchi waelewe kabisa kwamba, huo mradi sasa ni kweli utaenda kuanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la mchakato wa kwanza katika ujenzi huu wa *standard gauge* kupitia mfumo huu wa *Public Private Partnership* kwa njia ya ubia, tayari tumeitisha kikao tarehe 15 ya mwezi wa sita, mwezi huu, ambapo kitashirikisha Wizara yetu ya Ujenzi na Uchukuzi, pamoja na Wizara ya Viwanda, Uwekezaji na Biashara na Wizara ya Madini pamoja na taasisi zake zote pamoja na wadau wote ambao wanashiriki katika uchimbaji wa makaa ya mawe. Na kwa hivyo basi, nitoe rai kwa Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa hii ya Ruvuma pamoja na Mtwara kushiriki katika mkutano huu pamoja na Lindi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kuhusu kuambatana kwenda *site;* niko tayari kuambatana na Waheshimiwa aliowatamka, Mheshimiwa Angelina Manyanya pamoja na Agnes Hokororo na yeye mwenyewe Mheshimiwa Dkt. Ntara, ili tukapate kutoa elimu na kuwaelimisha wananchi katika maeneo hayo kuhusu uwepo na ujio wa mradi huu muhimu katika *Mtwara Corridor.*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Mwaluko Aidan Kabudi, swali la nyongeza.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. M. A. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, nashukiuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la

nyongeza. Napenda kujua ni lini Serikali itakarabati reli kutoka Kilosa – Mikumi hadi Kidatu, ili ianze kufanya kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Palamagamba Kabudi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge amefuatilia jambo hili kwa ukaribu. Tumetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa reli hii ya Kilosa – Mikumi, na tutaanza rasmi mwezi wa saba mwaka huu kwa ajili ya kuihuisha tena reli hii ianze kufanya kazi kama ilivyokuwa inafanya kazi miaka ya zamani. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Aboud, swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Watanzania tuna shauku kubwa;

Je, ni lini reli yetu ya kisasa ya mwendokasi itaanza kutoa huduma kwa wananchi kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Reli hii ya mwendokasi *(SGR)* kutoka Dar es Salaam kuja Morogoro, kilometa 300 itaanza kutoa huduma mwezi wa saba. Hivi sasa mwezi huu wa sita tunategemea kupokea mabehewa yenye ghorofa na hatimaye mwezi wa saba tutapokea kichwa. Na kwa kuwa tayari miundombinu yote *testing* na kila kitu kimeshafanyika katika njia hii ipo tayari kwa ajili ya kuanza mara baada ya mabehewa haya yatakayoingia mwezi huu wa sita na vichwa vitakavyoingia mwezi wa saba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deus Sangu, swali la nyongeza.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza mpango wake wa kujenga reli kutoka Tunduma mpaka Bandari ya Kasanga na Kabwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, reli hii ya kutoka Tunduma mpaka Rukwa, katika mwaka wa fedha ujao tutaanza kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa awali, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninataka kujua, je, ni lini mabehewa 37 yaliyokuwa kwenye karakana ya reli yakikarabatiwa kwa ajili ya safari za Kigoma – Dar es Salaam yataingia kwenye reli na kuanza kazi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI (MHE. ATUPELE F. MWAKIBETE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mabehewa aliyoulizia Mheshimiwa Mbunge ni kweli tunakarabati mabehewa 37, na kila mwezi tunakarabati mabehewa 22, 20 za mizigo na mbili za abiria. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wasafiri wote kutoka Kigoma kwamba mwezi ujao mabehewa haya yataanza kufanya kazi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, sasa aulize swali lake.

Na. 495

**Uwekaji wa taa za kuongoza magari – Igunga Mjini**

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaweka taa za kuongoza magari Igunga Mjini kwenye makutano ya barabara kuu ya Singida – Mwanza ili kuepusha ajali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, Mbunge wa Igunga, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2022/23, imepanga kuweka taa za kuongozea magari katika Mji wa Igunga sehemu tatu tofauti kulingana na uhitaji wa sehemu hiyo. Mkandarasi wa kufanya kazi hiyo amepatikana na kukabidhiwa kazi tangu tarehe 01 Aprili, 2023, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nicholaus George Ngassa, swali la nyongeza.

**MHE. NICHOLAUS G. NGASSA:** Mheshimiwa Spika, nitoe shukrani zangu kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Igunga kwa Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kulipokea hili tatizo, na hatimaye tumepata mkandarasi. Sina swali la nyongeza; nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itahakikisha alama zote muhimu katika barabara kuu za nchi yetu zinawekwa na zinasomeka vizuri?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, sijalipata swali lake vizuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, rudia vilevile tu ulivyosema, usianze maelezo ya mwanzo.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nauliza, ni lini Serikali itahakikisha alama zote muhimu za barabarani zinawekwa katika barabara zote kuu za Nchi yetu Tanzania? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, barabara zote zinazojengwa kisheria ni lazima ziwekewe alama zote za barabarani kwa sababu hizo ndizo zinazoongoza watembea kwa miguu, lakini pia wanaotumia magari na vyombo vyote vya moto, na kila tunapojenga barabara hizo kwa kweli huwa tunajitahidi kuweka alama.

Mheshimiwa Spika, changamoto ni kwamba kuna maeneo ambayo tukishaweka hizo alama, na hasa zile za vyuma inatokea baadhi ya wananchi huziharibu, hiyo ndiyo changamoto. Lakini pengine nitumie nafasi hii kuwaomba wananchi kwamba alama zote za barabarani zina umuhimu sana kwa maisha yetu na wale watumia barabara zetu muda wote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, sasa aulize swali lake.

Na. 496

**Ujenzi wa Daraja linalounganisha Kata ya Bokwa na Songe – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Kata ya Bokwa na Songe Kilindi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kazi ya ujenzi wa Daraja la Songe katika barabara ya Kwaluguru – Kiberashi linalounganisha Kata ya Bokwa na Songe na barabara zake unganishi imekamilika tarehe 30 Novemba, 2022. Kwa sasa mkataba upo katika kipindi cha uangalizi hadi tarehe 29 Novemba, 2023, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, kwanza nitoe shukrani za dhati sana kwa Serikali yetu kwa kutujengea daraja hili ambalo lilikuwa linaleta usumbufu mkubwa sana kipindi cha mvua. Baada ya shukrani hizo, sasa nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kata hizi mbili za Songwe na Bokwa kuna ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami; je, Serikali iko tayari kuweka taa katika eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kuna Madaraja mawili ya Chakwale na Nguyami ambayo yanunganisha Wilaya za Kilindi na Gairo. Je, ni lini Serikali itajenga madaraja hayo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa sasa barabara zote zinazojengwa na zinazopita kwenye miji mikubwa ama *centers* kubwa, maelekezo ni kwamba ni lazima tuweke taa kwa ajili ya matumizi ya usiku katika miji yote ambayo ni mikubwa. Kwa hiyo kwa barabara hiyo ambayo inajengwa nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tathmini itafanyika na tutahakikisha kwamba tunaweka taa.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili, tumeshakamilisha usanifu wa kina mwaka huu wa fedha kwa Madaraja yote mawili ya Chakwale na Nguyami ambayo yanaunganisha Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Tanga, na tumepanga fedha, kwamba mwaka 2023/2024, Madaraja yote hayo mawili ya Chakwale na Nguyami yanakwenda kuanza kujengwa, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, sasa aulize swali lake.

Na. 497

**Kubadilisha utaratibu wa utoaji wa vibali vya kuvuna miti**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kubadilisha utaratibu wa utoaji vibali vya kuvuna miti ili kuhusisha Kamati za Maendeleo za Kata na Vijiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Elinikyo Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, usimamizi na matumizi ya rasilimali za misitu hufanywa kwa mujibu wa Sheria ya Misitu Sura 323 na Kanuni zake za mwaka 2004. Aidha, katika kuhakikisha matumizi endelevu, Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii huandaa mwongozo unaotoa namna ya kutoa vibali na usimamizi wa jumla wa matumizi ya misitu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utaratibu huo Serikali ilitoa mwongozo mwaka 2017 unaofahamika kama 'Mwongozo wa Uvunaji Endelevu wa Mazao ya Misitu.' Mwongozo huo umebainisha wajumbe wanaounda kamati ya uvunaji ngazi ya wilaya chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Wilaya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na uwepo wa mwongozo huo wa mwaka 2017, bado kumekuwepo na ongezeko kubwa la kuvuna miti kiholela. Hata wale ambao wanapatiwa vibali, anapewa kibali cha kwenda kuvuna miti mifu anakwenda kuvuna miti hai. Yametokea

kwenye Vijiji vya Mshara na Uswaa, na Mto wote wa Makoa ule unaharibika: -

Je, hamuoni ni wakati sahihi sasa wa kuongeza nguvu wa kushirikisha *ODC* na mikutano mikuu ya vijiji?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa mwongozo huu ni wa muda mrefu sasa, hamuoni ipo haja ya kufanya maboresho ya mwongozo huu ikiwa ni pamoja na kuongeza kipengele kwamba wale wanaopewa vibali vya kuvuna miti na wao wapewe miti kadhaa ya kupanda kwenye maeneo ambayo wanavuna miti?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kuhusu hili ongezeko la ukataji miti hovyo, hususan kwa hawa wavunaji, ni kweli kumekuwa na ongezeko hili, lakini kwenye ile kamati tulitarajia kwamba mwongozo huu usimamiwe vizuri kwa sababu Mwenyekiti wa Serikali ya kijiji ni mjumbe wa kamati ya uvunaji ya wilaya. Kwa hiyo tunatarajia anapoitisha vikao vya vijiji tayari wanakijiji wote wanakuwa wanajua kwamba eneo lao linakwenda kuvunwa, na ujumbe unaotoka kwa wanakijiji anauchukua mwenyekiti na anaingia kule kama mjumbe anaufikisha.

Mheshimiwa Spika, wakati huohuo kuna kamati ya mazingira na kamati ya maliasili ambazo ziko chini ya Serikali ya kijiji, zote hizi zinapitisha utaratibu wa namna ya kuvuna. Kwa hiyo sisi hatuoni kama kuna haja ya kubadilisha mwongozo, isipokuwa usimamizi wa ule mwongozo ndio tunatakiwa tuuboreshe zaidi, kwa maana ya kwenda chini na kufuatilia zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwenye hili suala la pili la kuangalia kipengele kwa wale wanaovuna, kwamba kuwepo na haja ya kurejesha, kwa maana ya kupanda miti; kuna asilimia tano ya mvunaji; anapokuwa ameshapata kibali cha kuvuna anarejesha asilimia tano na inarudishwa kwenye halmashauri ya wilaya. Ile asilimia tano ya fedha zinazotokana na uvunaji inakwenda

kurudisha uoto wa asili kwa kupanda miti. Kwa hiyo tunazielekeza halmashauri kwenye ile fedha inayorudishwa ya uvunaji wahakikishe kwamba inakwenda kwenye matumizi ya upandaji miti ili kurudisha uoto wa asili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

Na. 498

**Kuhamisha Kituo Kidogo cha Polisi Tumbe**

**MHE. OMAR ISSA KOMBO K.n.y. MHE. AMOUR KHAMIS MBAROUK** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali imehamisha Kituo Kidogo cha Polisi Tumbe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amour Khamis Mbarouk, Mbunge wa Tumbe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, shughuli na huduma za Kituo cha Polisi Tumbe kilichopo Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba, zimehamishwa toka Tumbe kwenda Kituo cha Polisi Konde. Sababu ya kufanya hivyo ni uchakavu wa jengo lililokuwa linatumika kama kituo cha polisi ambalo ni mali ya Shehia ya Tumbe Mashariki. Jengo hilo halifai tena kwa matumizi ya kazi za

polisi. Eneo hilo pia ni finyu na limezingirwa na nyumba za makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia fursa hii kumshauri Mheshimiwa Mbunge kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni kupata eneo kubwa zaidi lenye angalau ukubwa wa *square meters* 3,000 kwa ajili ya kujenga kituo cha polisi eneo hilo la Tumbe. Wizara kupitia Jeshi la Polisi itaunga mkono katika ujenzi wa kituo hicho kipya, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Waziri amekiri kwamba kituo hiki kutokana na uchakavu tayari kimeondoka; na tayari kutokana na mahitaji na eneo lile ni kubwa, kuna miradi mikubwa ya Serikali ambayo ipo sasa: -

a) Je, Serikali haioni haja ya kuweka kituo cha dharura katika eneo hili la Tumbe?

b) Je, Wizara iko tayari kwenda kukaa na ofisi ya mkuu wa wilaya pamoja na halmashauri kuangalia eneo kubwa au kupatiwa eneo ambalo litatosha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mbunge wa Wingwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, ni kweli kabisa kwamba eneo hili lina matumizi makubwa kwa kuwa pia kuna miradi mikubwa ambayo inahitaji kituo cha polisi. Lakini kituo cha polisi cha dharura kinaweza kikapatikana endapo tu

mamlaka za halmashauri husika zitatenga jengo ambalo litakuwa na sifa ya kutumika kama kituo cha polisi.

Mheshimiwa Spika, suala la eneo; kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi, ni jukumu la halmashauri sasa kutafuta eneo ambalo tunakwenda kujenga kituo kipya. Na Wizara iko tayari kutoa ushirikiano kwa mamlaka za halmashauri hiyo ili kituo hicho kiweze kujengwa haraka sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya; Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 499

**Kupunguza gharama za matibabu kwa akina mama wanapokwenda kliniki – Sumbawanga**

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za matibabu kwa akina mama wanapokwenda Kliniki Sumbawanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Sera ya Afya ya mwaka 2007 kifungu Na. 5(3) na (4)(c) kinaelekeza kuwa huduma za afya ya uzazi ikiwemo kuhudhuria kliniki, wakati wa uchungu, wakati wa kujifungua, na

baada ya kujifungua pamoja na uzazi wa mpango zitakuwa zikitolewa bila malipo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa wito kwa watumishi katika vituo vya kutolea huduma za afya kutowatoza gharama za uzazi wanawake wote wanaofika vituoni kupata huduma ya afya ya uzazi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, swali la nyongeza.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, ninapenda kujua;

Je, ni kwa nini sasa sera hii haitekelezeki kikamilifu, kwa sababu wanawake wajawazito na watoto chini ya miaka mitano bado wanalipishwa kwenye suala zima la afya?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wazee zaidi ya miaka 60 bado pia wanatozwa pesa wanapokwenda kutibiwa;

Je, kwa nini sera hii haitekelezeki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anashirikiana na Waheshimiwa Wabunge wa mkoa wake kufuatilia masuala muhimu ya afya katika mkoa wake.

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, ni kwa nini sera hii haitekelezwi kwa asilimia 100 kama ilivyozungumzika. Ni kama maeneo mengine, wote tunajua kuna kipindi tulipitia kwenye shida ya upungufu wa dawa, kwa hiyo kunapokuwa na upungufu wa dawa na vifaa tiba basi linaathirika eneo hili kama yanavyoathirika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, lakini pia unakumbuka hapa wakati wa bajeti yetu mlizungumzia suala la mtaji kwa *MSD*. Sasa maana yake *MSD* ikishapata mtaji badala ya kutegemea fedha kutoka kwenye vituo, basi sasa ule mnyororo wa upatikanaji wa dawa hautakatika tena kama ambavyo umekuwa ukikatika, na sasa tutaweza kuhakikisha kwamba sasa dawa zitakuwa zinapatikana wakati wote na vifaa tiba vinapatikana wakati wote, na akina mama wanaweza kupata huduma kama ambavyo inatajwa na sera. Tumeshaainisha, Mheshimiwa Waziri ameunda tume imeonesha kwamba tunahitaji bilioni 167 kuweza kuhudumia wananchi katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu wazee linafanana na hili lingine. Kwanza niseme tu kwamba tumeagiza kila kituo cha afya, kila zahanati, kila hospitali kuwepo na dirisha la wazee. Na tunawaomba wenzetu wakuu wa wilaya na wakurugenzi wasimamie eneo hili la akina mama na eneo la wazee kuhakikisha hili takwa la kisera linatekelezwa ipasavyo, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo; Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 500

**Ukarabati wa Skimu za Umwagiliaji – Kakonko**

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakarabati Skimu za Umwagiliaji za Katengera, Ruhwiti na Muhwazi ili kuboresha kilimo cha umwagiliaji Kakonko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Skimu za Umwagiliaji Katengera, Ruhwiti na Muhwazi ni miongoni mwa skimu zilizoko katika Wilaya ya Kakonko zinazounda mabonde 22 ya kimkakati. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imepanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kupitia mshauri elekezi katika Skimu za Buyungu, Nyakanyezi, Mgunzu, Kayonza, Muhwazi, Ruhuru na Chulanzo zilizoko katika Wilaya ya Kakonko.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetenga fedha za kuanza ujenzi wa skimu zinazounda mabonde 22 ya kimkakati ambapo Skimu za Katengera, Ruhwiti na Muhwazi ni miongoni mwa skimu hizo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aloyce Kamamba, swali la nyongeza.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali ambayo hayajakidhi swali langu, kwa sababu Skimu za Katengera, Ruhwiti na Muhwazi ambazo nimezitaja, siyo skimu mpya, ni skimu ambazo zimekuwepo na zimekuwa zikifanya kazi. Tatizo miundombinu yake imeharibika na hivyo hazifanyi kazi sasa.

Mheshimiwa Spika, swali; Je, lini mtapeleka fedha kwenye skimu hizi kwa ajili ya ukarabati ili ziweze kufanya kazi inayostahili?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; wananchi wetu wakulima hawana taaluma juu ya utumiaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa maana ya kwamba hawana taaluma;

Je, ni nini kauli ya Serikali kuhakikisha kwamba wanakuwa na maarifa na taaluma ya kutosheleza kutumia miundombinu ya umwagiliaji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika majibu yangu ya msingi nimeeleza vyema kabisa tunayo mabonde 22 ya kimkakati. Katika Mkoa wa Kigoma tunafanyia kazi Bonde la Mto Malagarasi na Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, katika maziwa na mito hii miwili ambayo nimeisema ndani yake skimu hizi zinapatikana. Kwa hiyo Serikali imeamua ifanye kazi kubwa kwanza ya upembuzi yakinifu kwenye mabonde haya ambayo pia ndani yake itajumuisha skimu ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitamka. Kwa hiyo nimwondoe hofu kwamba skimu ambazo amezitamka ni ndani ya mkakati wa Serikali katika utekelezaji wa haya mabonde ambapo kazi imekwisha kuanza na ujenzi utaanza mwaka wa fedha ujao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu elimu; tumeajiri wahandisi wa umwagiliaji wa kila wilaya. Hawa watakuwa na jukumu pia la kuhakikisha kwamba wanawapa elimu wakulima wetu juu ya matumizi sahihi ya maji katika kilimocha umwagiliaji. Hivyo wananchi pia wa Jimbo la Buyungu watanufaika na huduma hii kupitia wahandisi wetu walioko wilayani.

**SPIKA:** Mheshimiwa Deodatus Manyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi;

Je, ni nini mkakati wa Serikali kuanzisha miradi ya umwagiliaji kwenye maeneo ya wakulima wadogo wadogo wa chai eneo la Igomini Tarafa ya Igomini Halmashauri ya Njombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nataka kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, hii ni hoja ambayo Mheshimiwa Mbunge alishaifikisha katika Wizara ya Kilimo na tumemuahidi baada ya Bunge hili la bajeti namwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ndugu yangu Raymond Mndolwa waongozane na Mheshimiwa Mbunge kwenda kufanya tathmini katika maeneo yaliyotajwa ili tuweze kuwasaidia wakulima wa chai katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Je, ni lini Serikali itajenga skimu za umwagiliaji katika maeneo ya Mavimba, Lupilo, Minepa, Kivukoni, Namilela katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tumeainisha maeneo mengi ambayo tunakwenda kuyafanyia kazi katika mwaka wa fedha ujao. Nitakaa na Mheshimiwa Mbunge kuangalia maeneo ambayo ameyataja kama hayajajumuishwa basi tuweze kuyaweka katika mpango wetu ili kuhakikisha wananchi hao pia wanafanya kilimo cha umwagiliaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itajenga skimu katika bonde la Eyasi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tarehe 20 Machi, 2023 tulisaini mikataba ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde 22 ya kimkakati hapa nchini Tanzania likiwemo Bonde la Eyasi. Kwa hiyo maana yake skimu zote za Eyasi zitajengwa katika mwaka wa fedha unaokuja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Spika, ahsante; je, ni lini Serikali itapeleka pesa kwa ajili ya kukamilisha miradi ya umwagiliaji katika Kijiji cha Misyaje na Madaba kilichopo Jimbo la Tunduru Kusini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni mkakati wa Serikali kuhakikisha tunakamilisha skimu zote za umwagiliaji ili wananchi wafanye kilimo cha umwagiliaji. Nitakaa na Mheshimiwa Mbunge kuangalia skimu alizozitaja kama hazipo kwenya mpango wa mwaka wa fedha unaokuja basi tuziingize kwenye mpango ili wananchi waweze kushiriki kwenye kilimo cha umwagialiaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, swali la nyongeza.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itapeleka pesa kukamilisha mradi wa Lubasazi kata ya Kolelo na mradi wa…

**SPIKA:** Mheshimiwa ni moja. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema ninayo orodha ya miradi mingi ambayo tunaitekeleza hivi sasa inawezekana nitashindwa kumpa moja kwa moja mradi wake katika hatua iliyofikia lakini mimi nitakaa naye ili tuangalie katika jedwali letu tuone kama mradi huo haupo basi tuweke katika vipaumbele vyetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi swali la nyongeza.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini skimu ya umwagiliaji ya Mwamapuli itaanza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika skimu zaidi ya 42 ambazo tutakwenda kuzijenga katika mwaka wa fedha huu ambao unaishia na ambao unaendelea ni pamoja na Skimu ya Mwamapuli. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hilo liko ndani ya utekelezaji wa Serikali.

**SPIKA:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itajenga skimu za umwagilaiji kwa kutumia maji ya Mto Rwiche katika manispaa ya Kigoma Ujiji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwenye mradi wa umwagiliaji kutumia Bonde la Rwiche tunachosubiri hivi sasa ni ile barua ya kutokuwa na kipingamizi ambayo baada ya hapo tutanza utekelezaji mara moja. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zimeshakamilishwa ndani

ya Serikali tumebakiza kutoka kwa Mhisani tukipata *letter of no objection* tunaendelea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu kwa upande wa Serikali. Nitaleta tangazo la wageni walioko Bungeni siku ya leo.

Tunao wageni 129 wa Mheshimiwa Naibu Spika, Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Kule nyuma kuna Wabunge naona wanazungumza na mwingine amesimama, atafute kiti aketi.

Wageni wawili wa Mheshimiwa Benaya Kapinga, watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa unayetembea huko nyuma sijui unasubiria kutajwa au namna gani. Tafuta kiti uketi tafadhari kwa sababu mimi nimesimama, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, wageni wawili wa Mheshimiwa Salma Kikwete (Mb), Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya CCM Wilaya ya Lindi Mjini. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Khadija Taya kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Cosato Chumi kutoka Dodoma na Uingereza, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Seleman Zedi ambao ni Waratibu wa Umeme Vijijini *(REA)* kutoka Jimbo la Bukene, Mkoa wa Tabora, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Daniel Sillo ambao wametoka Babati Vijijini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 20 wa Mheshimiwa Deo Sanga ambao ni watumishi kutoka *TANESCO* Mikoa ya Iringa na Njombe wakiongozwa na Mhandisi Andrew Ako ambaye ni Meneja wa Mkoa wa Njombe na Mhandisi Abdul Jumbe Meneja wa Mkoa wa Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 30 wa Mheshimiwa Nashon Bidyanguze, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Asia Halamga ambao ni Masister wa Kanisa Katoliki kutoka Hanang, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa Salome Makamba ambao ni wajasiliamali kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 47 wa Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo wanafunzikutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; Mheshimiwa Kunti na Mheshimiwa Salome Makamba tusikilizane.

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; kwanza wanafunzi 40 na walimu 10 wa Shule ya Sekondari Mkonze ya Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia wazazi 20 na wafanyakazi 10 kutoka *Bwipa Day Care* ya Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge hao ndio wageni tulio nao Bungeni asubuhi ya leo. Mheshimiwa Michael Kembaki ulikuwa umesimama unaomba mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa Kanuni namba 54(55).

Mheshimiwa Spika, shule zinafungwa wiki hii lakini pia Wizara imeagiza wadhibiti ubora kuzuia makambi yote ya kimasomo katika kipindi hiki cha likizo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mikoa imepanga utaratibu wa kuongeza ufaulu katika mikoa yao na wameagiza shule kuendelea na masomo ya ziada katika kipindi hiki cha likizo. Hii imepelekea wadhibiti ubora kubaki njia panda, kwamba watekeleze agizo la Wizara au watekeleze agizo la Wakuu wa Mikoa.

Mheshimiwa Spika, niliwahi kutoa swali hapa kuhusu kwamba wanafunzi wanaofanya mtihani darasa la saba wanasoma mpaka mwezi wa tisa wanafanya mtihani, lakini mtaala unapaswa ukamilike Novemba hadi Disemba. Sasa kipindi hiki ndicho ambacho walimu wanatakiwa wafanye kazi ya ziada kuhakikisha watoto wanafaulu. Wizara inazuia walimu wasifanye jitihada kuhakikisha kwamba ufaulu unapatikana kutokana kwamba muda hautoshi wa kufundisha watoto hawa wa darasa la saba.

Mheshimiwa Spika, naomba kiti chako na Bunge hili Wizara itupe ufafanuzi wa kutosha ni lipi lifanyike sasa ili kuhakikisha kwamba watoto wetu wanafaulu na wanasoma kikamilifu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Michael Kembaki akiomba, kwanza alisema Mwongozo, lakini baadaye kumbe anataka kuleta hoja ya dharura na ametoa maelezo hapo kuhusu hoja yake.

Kwa maelezo yake ni kama kuna mkanganyiko wa maelekezo kwa wadhibiti ubora wa elimu ambao wamepewa maelekezo kutoka Wizarani kwamba kusiwe na kambi zinazohusu yale masomo ya ziada, wakati huo huo Mikoa na Wilaya zinajipanga huko ili wafanye vizuri katika maeneo yao. *(Makofi)*

Sasa yeye uzuri wake amemalizia kwa kutaka Wizara itoe ufafanuzi kwa hiyo, hajataka Bunge lijadili kwa sababu pengine jambo hilo limekosa kufanyiwa kazi katika ule utaratibu wa kawaida; na kwa sababu Serikali ipo Bungeni basi tuipe nafasi ya kufafanua jambo hilo kwa dakika chache.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais naona ndiye umekaa kiti cha upande wa Serikali, kwa hiyo kama Naibu Waziri wako ndiye ana maelezo nimpe yeye nafasi ama nikupe wewe nafasi, naona wote wawili mnataka kusimama.

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Juma Kipanga maelezo. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Tumepokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge. Kwa mujibu wa sheria wanafunzi wanatakiwa kusoma darasani siku 194 kwa mwaka. Na kwa kadri muhtasari ulivyoandaliwa wanafunzi kuanzia darasa la kwanza mpaka darasa la saba wanapaswa kukamilisha kupitia muhtasari au mitaala hiyo katika siku hizo 194, na vipindi vimepangwa katika utaratibu huo.

Sasa kwa vile Mheshimiwa Mbunge ameleta hiyo hoja kwamba wakuu wa mikoa wameagiza kwenye baadhi ya mikoa kwamba wale watoto wa madarasa ya mitihani inabidi wabaki kwenye hizo kambi. Naomba tuibebe hoja hii twende tukaifanyie kazi, tuone changamoto zilizopo kwenye mikoa husika halafu kama Serikali tutakuja kutoa kauli na mwongozo hapa Bungeni, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa sababu shule kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge zinafungwa wiki hii na lazima huko wafanye mipango,

mimi nikupe wewe mwenyewe unataka muda gani wa kuja kutoa hayo maelezo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, mpaka kufika kesho asubuhi tutatoa huo mwongozo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge nadhani turidhike na hayo kesho tutampa nafasi Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi wa huo mkanganyiko uliojitokeza na wakati huo sasa tutajua kama itakuwepo hoja kwa ajili ya mjadala au hapana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na ratiba yetu, Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma, Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza ajiandae.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, niendelee kukushukuru sana lakini pia mimi niendelee kukuombea sana kwa Mwenyezi Mungu jambo lako ambalo liko mbele yako uweze kufanikiwa na upate ushindi mkubwa kuiwakilisha Tanzania; na kama mwana mama uendelee kuandika historia kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika,mimi niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu mama Samia Suluhu Hassan kwa niaba ya wanachi wa Jimbo la Ushetu kwa kutujali kwenye suala la

umeme. Wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani Ushetu ilikuwa na kata saba tu zilizokuwa zimeshafikiwa na umeme. Leo Mheshimiwa Rais yuko madarakani kata zote 20 zimeshafikiwa na mtandao wa umeme. Lakini pia kwenye vijiji wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani tulikuwa na vijiji ambavyo vimefikiwa na umeme vilikuwa vijiji 20 lakini leo tunavyoongea vijiji 71 kwenye Jimbo la Ushetu tayari vimefikiwa na umeme. Niendelee kumpongeza Mheshimiwa Rais lakini pia kipekee niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri ndugu yangu Januari Makamba, Ushetu sasa inaendelea kuneemeka, Ushetu sasa inaendelea kung'aa. Niendelee kukuomba; vijiji ambavyo vimebaki kwa wananchi wa Ushetu sasa ni vijiji 41 ambavyo havijafikiwa na umeme kabisa. Niendelee kukuomba uendelee kumbana mkandarasi. Mkandarasi wako anaenda taratibu sana.

Mheshimiwa Spika, jiografia ya eneo la Ushetu na Halmashauri ya Ushetu ni kubwa sana akaze buti. Ukiangalia tu majimbo yetu yote matatu na Halmashauri tatu ukijisemea Kahama Manispaa, Msalala pamoja na Ushetu akimbize. Hata kipindi fulani niliuliza swali hapo nyuma la nyongeza kwamba Mkandarasi anaenda kwa kusua sua msukumeni sasa akimbize. Tunaona mabadiliko sio kama ilivyokuwa mwanzo,na Imani kazi imefanyika akimbize. Vijiji vinahitaji umeme, shule zinahitaji umeme, hospitali zinahitaji umeme na zahanati zetu kwenye vijiji vyetu ambazo amezijenga Mheshimiwa Rais zinahitaji umeme. Akimbize akamilishe hivyo vijiji 41viweze kufikiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini nimeona jana amesema kila jimbo angalau kupata vitongoji 15 kwa ajili ya kuwapatia umeme. Ndugu yangu Januari nikuombe Mheshimiwa Waziri, Ushetu ina vitongoji 561, sasa unaposema tu vitongoji 15 unaacha kipi na unachukua kipi? Tumia hekima yako tumia busara yako. Najua wewe ni kijana unahitaji kesho kubwa pambana ili wananchi wangu wa Ushetu na vitongoji angalau viongezeke kwa sababu ya wingi.

Mheshimiwa Spika, unajua tunatofautiana vitongoji unakuta kuna Halmashauri nyingine ina vitongoji 200 nyingine 300; lakini angalia vitongoji 561 na kitongoji kimoja ukubwa wake unaweza

ukadhani ni vijiji viwili kwa hiyo niombe hili Mheshimiwa Waziri ulichukue utalifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, niendelee kumuomba Mheshimiwa Waziri aiangalie Kahama kwa macho mawili. Mwaka jana tulilia sana, tulisema hapa na Mheshimiwa Idd pamoja na Profesa Kishimba. Kahama ilivyo inahitaji mkoa wa ki-*TANESCO*. Kwa nini Kahama usiipe mkoa wa ki-*TANESCO* kwa upande wa Umeme. Ukingalia wenzio *TRA* tayari wana Mkoa wa ki-*TRA* kwa sababu ya makusanyo yaliyopo pale Kahama. Ukiangalia *NSSF* wana Mkoa wa ki-*NSSF* kwa sababu ya makusanyo yaliyopo pale Kahama. Ukiangalia hata kwenye upande wa kilimo wenzetu wa tumbaku wana mkoa wa ki-tumbaku Kahama kwa sababu ya kazi na ukubwa wa eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, hali ya umeme ya Kahama ni mbaya. Kahama ambayo ina viwanda zaidi ya 422 umeme unakatika kwa wiki, umeme unamaliza wiki haupatikani Kahama. Kahama ambayo inawafanyabiashara, eneo lillotengwa na Manispaa ya Kahama; kuna eneo maarufu linaitwa Dodoma lina vijana waliojiajiri zaidi ya 1,700 umeme vijana wanashinda wamekaa umekatika Kahama. Hii Kahama ambayo ina benki zaidi ya 12 umeme unakatika katika. Kahama ambayo ina hoteli nyingi, ina wageni wengi, ina mzunguko mkubwa, ina kusanya kwa mwezi zaidi ya bilioni nne na milioni mia tano umeme ni wa kusua sua. Kahama ambayo kwa miezi mitatu imeweza kukusanya zaidi ya bilioni 13; Kahama imekusanya bilioni 13 kwa miezi mitatu lakini umeme bado ni wa kusuasua. Yaani Kahama biashara ya *generator* ni kubwa kuliko biashara ya umeme unavyopatikana.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri aiangalie Kahama kwa jicho, aiangalie Kahama na ukubwa wake. Wananchi wa Kahama wanalalamika hakuna umeme, wafanyabiashara wa Kahama wanalalamika hakuna umeme…

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Stella Fiyao.

**TAARIFA**

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa Mheshimiwa Taarifa kwamba, tatizo lililoko Kahama ndio tatizo lililoko Songwe ambalo ndilo lango Kuu la *SADC*. Umeme unakatika kila mara wananchi tunakosa majibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani, unaipokea taarifa hiyo?

**EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwa sababu inaongezea nguvu kwenye miji mikubwa inayokusanya fedha nyingi kwenye mapato makubwa, Serikali ipeleke umeme igeuze na ibadilishe maeneo yale ambayo yana makusanyo makubwa ya fedha yapewe nguvu na yapewe mikoa.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri, maeneo ambayo anapata nguvu, anapata fedha nyingi aelekeze nguvu; Serikali ya Mheshimiwa Rais inahitaji fedha; na jana Mheshimiwa Waziri ametuonesha; mimi sijafika kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, mimi jana nimeliona pale Dodoma, nimeliona, ukigeuka huku unaona Mtumbwi, ukigeuka huku unaona unasogelewa na Samaki. Sasa kwa nini ashindwe kufanya miji inayokua kwa kasi aibadilishie kukatikakatika kwa umeme iwe historia?

Mheshimiwa Spika, mimi nalia na Kahama, eneo la Kahama ukiliwekea mkoa Msalala ambayo ina madini, ina vijana ambao wanahangaika, ina wachimbaji wakubwa itaneemeka na hawatasumbuka na umeme. Kahama ukiipa mkoa, Ushetu wakulima wetu watawekeza viwanda. Ndiyo maana hata juzi wawekezaji wetu wanunuzi wakubwa wa tumbaku wameshindwa kuwekeza kwa sababu hakuna umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, mimi niendelee kukuomba, na niendelee kukupongeza sana, kazi unayoifanya ni kubwa sana, lakini hebu angalia kwa macho mawili miji inayokuwa kwa kasi ipe mkoa. *RCC* Mkoa wa Shinyanga imeshakaa ikamaliza na ikatoa mapendekezo, leo ni zaidi ya miaka mitatu mmekaa tu. Fanyeni ziara muone jiografia ya

maeneo. maeneo mengine Mheshimiwa Waziri wamefanya kazi vizuri sana, wanadhibiti mapato. Lakini wanashindwaje kwenda kujiridhisha maeneo ambayo yanakusanya? Kama kwa mwezi mmoja tu, mfano mwezi wa pili Kahama imekusanya bilioni 8,323,140,550.36 kwenye makusanyo ya umeme wilaya hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimpongeze Tumaini Chonya ambaye ni meneja wa Wilaya, yule bwana halali, anafanya kazi. Akipigiwa simu Msalala anakimbia, Ushetu anakimbia, na sisi tukiwa kwenye mkutano wa hadhara wananchi wakilalamika tu tunamuunganisha hapo tunaweka *loud speaker,* analalamika, anasema anachopata ni sawa na wilaya nyingine kama zilivyo. Sasa hauwezi kuilinganisha Wilaya ya Kahama na wilaya nyingine halafu ukailinganisha matumizi na kuipelekea hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri utakapokuja kuhitimisha suala la Kahama liwe na majibu ya kipekee. Tunahitaji Kahama ipate mkoa. Na kama *RCC* imekwishapitisha ninyi wizara mnashindwa nini? Niendelee kumuomba Mheshimiwa Waziri; kuna kata zangu hazina umeme. Kata ya Igwamanoni…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel, kengele ya pili imeshagonga, malizia sentensi.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Spika, Kata yangu ya Igunda, Kata ya Igwamanoni, Kata ya Chona ni maeneo ambayo vijiji vyake vingi havijapata umeme. Mheshimiwa Waziri, naomba aangalie Mkandarasi, amsukume kwenye kata zangu hizi ili ziweze kupelekewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Samweli Xaday Hhayuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya ajiandae.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsnate sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumpongzea sana Mheshimiwa Waziri wazo lake la kufanya wiki ya nishati hapa Dodoma imetusaidia sana sisi Wabunge. Badala ya kutafuta wa wilaya, mkoa na ngazi ya Taifa wote tunawapata kwa pamoja, kweli wameturahisishia huduma na suluhu zingine tumekuwa tukizipata hapa hapa. nimpongeze sana kwa ubunifu huo, ni vitu vya kuigwa na kuendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa inafanyika kwenye sekta ya nishati, na naamini kwamba miradi hii ikikamilika kwa wakati, na Mheshimiwa Waziri amechambua vizuri, kwamba tutaongeza upatikanaji wa umeme mpaka kufikia *megawatt* 5,213.22 na tutakuwa tunaanza kuuza umeme mpaka nje ya nchi. Ninaomba, kwa sababu lengo hili limewekwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2023/2024, naomba kasi hii iongezeke ili tupate umeme wa uhakika kwani umeme ndio unaowezesha viwanda kuendelea na Tanzania viwanda haviwezekani bila kuwa na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi kirefu tumekuwa na changamoto mmesikia wenzangu wakisema umeme unakatika. Jimbo la Hanang' changamoto hiyo ipo, umeme unakatika na haijulikani wakati gani kuna umeme na shughuli zinalala. Sisi ni wakulima, sisi ni wafugaji; kuchakata mazao hayo ya mifugo, mazao yanayotoka mashambani inakuwa ni changamoto kubwa kwa sababu umeme unakatika sana. Tulikuwa tumesahau kipindi cha hapo katikati masuala ya kuhangaika na *generator* lakini sasa hivi wimbo umekuwa ni huo. Naomba uchukue hatua. Na pale ulitupa kituo cha kupooza umeme ili angalau kupunguza ile *line* kwa sababu *line* ikiwa ndefu nayo inachangia umeme kukatika. Pale Mogitu watu wako wamekwisha tembeatembea naomba zoezi lile la kujenga kituo cha kupooza umeme liharakishe.

Mheshimiwa Spika, wakati Dkt. Samia Suluhu Hassan, anashika nchi vijiji vyangu vyenye umeme vilikuwa 54 tu, kwa sasa

viko 73. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo inafanyika ya kuwapatia wananchi umeme. Hata hivyo, bado tuna vijiji 23 naomba mkandarasi ambae yuko *site* msukume aongeze kasi mradi ule uweze kukamilika na wananchi wapate umeme. Lakini kuna maneo mengine ambapo umeme umegusa tu kama Kijiji cha Getasam nyumba tatu tu ndizo zina umeme. Watu wako waangalie eneo hilo ili utusaidie watu wapate umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna maeneo ambayo yamepata umeme tangu miaka ya 90, watu wameongezeka sana kwenye maeneo hayo. Kata kama ya Gitting maeneo yake mengi yalipata umeme zamani. Sasa hivi tunapeleka umeme kwenye vijiji vipya ambavyo havina umeme lakini wale wa zamani kasi ya *TANESCO* ni ndogo sana.

Mheshimiwa Spika, ukienda Nangwa maeneo mengi watu wengi wengi hawana umeme, ukienda Gendabi maeneo ambayo umeme ulipatikana zamani watu wengi hawana umeme, maeneo ya Jorodom maeneo hayo yaangaliwe kwa jicho la kipekee ili watu wapate umeme.

Mheshimiwa Spika, umeme ukifika kwenye eneo unachangamsjha maendeleo na watu wanajenga zaidi. Wakijenga *TANESCO* waongeze kasi ya kupeleka umeme kwa wananchi. Lakini, kuna changamoto pia, sijui ni *TANESCO* au wakandarasi wenu ambao mmewathibitisha; wanawambia wananchi wafunge umeme. Kwa mfano Kijiji changu cha Dirma Kata ya Bassotu wananchi asilimia kubwa wamefanya *wiring* miaka mitatu mpaka sasa umeme umeme haujaenda. Sasa mnapohmasisha wananchi wafanye *wiring* iende sambamba na miradi ya upelekaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya ya jimboni kwangu; kwenye hotuba yake Mheshimiwa Waziri ameeleza vizuri kuhusu matumizi ya gesi; ni kama matumizi ya mpito, na ikifika 50/50 kwa ule mpango wa kutumia *clean energy* gesi nayo itakuwa *phased out*. Mmefanya *negotiation* ya gesi asili imechukua muda mrefu sana. Ongeza kasi kwenye eneo hilo ili

gesi hii ya kwetu tuweze kuitumia na tunufaike nayo. Imechukua muda mrefu mnajadiliana mjadala huo haufiki mwisho. Simamia, na tunakuamini; wewe nguvu yako ni kubwa na ubunifu tumeuona weka kasi hapo ili hatimaye tuweze kutumia gesi yetu ya asili iweze kunufaisha taifa letu isije ikawa kama makaa ya mawe, ambako dunia sasa inaacha matumizi ya makaa ya mawe na sisi hata hatujawahi kuyatumia. Hivyo, isije ikatokea kwenye gesi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa Bungeni tumejadili sana masuala ya udhibiti vinasaba kwenye mafuta. Huko nyuma kulikuwa na kelele nyingi sana, imeenda *TBS* sasa hivi kumetulia. Maneno yameanza kuwa mengi kwamba sasa *TBS* waondolewe kwenye eneo la usimamizi wa vinasaba kwa ajili ya kuhakikisha ubora wa mafuta yetu. nikushauri tu kwamba, jambo lililotulia tusiliamshe tusiingie kwenye migogoro ambayo haina tija. Mamalaka ya *TBS* ni msimamizi wa ubora kwa bidhaa nyingi kazi kubwa anafanya, maabara zake ni nzuri tuendelee kuwaamini.

Mheshimiwa Spika, nigusie kidogo eneo la Shirika letu la *TANESCO*. Mheshimiwa Waziri, tupia jicho kule kidogo. Shirika hili lina mkataba wa hali bora ya wafanyakazi na chama cha wafanyakazi; lakini kuna harakati mbalimbali zinazofanyika katika kuboresha shirika. Ni jambo jema kwa sababu ili shirika lolote liweze kuwa na ufanisi ni lazima lijitazame. Hata hivyo, majukumu yote yanayofanyika kila mmoja anataka kujua kesho yake iliyo wazi. Hata wewe Mheshimiwa Waziri unapanga mipango yako na upanga vitu ambavyo vitakutengenezea njia ya kazi. Na watumishi nao wanataka kufahamu haki yao na majukumu yao wanayoyafanya na wajibu wao wanaoutekeleza lakini haki ziwe wazi, kama kuna mabadiliko yoyote washirikishwe ili hatimaye nao wajipange kwa sababu ni watu wana mipango yao, badala ya kuwa na harakati ambazo zinafanyika ambazo haziko wazi kwa chama cha wafanyakazi.

Mheshimiwa Spika, nikuombe tu, baada ya kusema haya ambayo nimesema, Jimbo langu la Hanang' ni kati ya majimbo makubwa; tuna vijiji 96 na vitongoji 414. Wakati unapopanga mipango yako ya kazi majimbo haya makubwa uyaangalie kwa

macho ya kipekee ili hatimaye maendeleo yaweze Kwenda sambamba katika nchi yetu. Uki-*concentrate,* na kwa mfano suala hili upande *TARURA* nilishaongelea, kwamba tunagawa rasilimali kijimbo au kiwilaya maeneo mengine ni makubwa na mengine ni madogo. Maeneo haya makubwa yaangaliwe ikiwezekana twende kwa idadi ya watu au kwa hali ya jiografia ya maeneo yanayohusika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadya ya kusema haya nakushukuru sana naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipa nafasi hii niwe mmoja wa wachangiaji wa bajeti yetu hiii muhimu ya Wizara ya Nishati.

Mhemiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuweza kuifanikisha Wizara hii kwa kuipatia fedha kwa wingi na kuweza kufikia malengo yake. Pia, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi wa *REA,* Mkurugenzi wa *TANESCO* Ndugu Maharage Chande na wafanyakazi wao wote kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakiitendea haki Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, leo hii mimi nimesimama, na mara nyingi zaidi ya miaka mitatu minne nilikuwa nikisimama jambo langu kubwa lilikuwa ni kuhusu bei ya umeme Zanzibar. Lakini mimi ninayofuraha, pamoja na Wazanzibari wote jinsi ambavyo Wizara hii chini ya usimamizi wa viongozi hawa na Katibu Mkuu wao Mramba, kuweza kukubaliana na Serikali ya Zanzibar kuweka bei sawa pamoja na Tanzania bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo hili tunawapongeza sana. Leo nitakuwa na mambo mawili ambayo yanataka Mheshimiwa Waziri utakapo *wind up* unipe *status* yake limefikia wapi.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na mpango wa *TANESCO* wameongea na Wizara ya Nishati ya Zanzibar kuhusu kupeleka *cable* nyingine ya umeme, kwa sababu *cable* iliyokuwepo sasa hivi inakaribia kuzidiwa kwa kuwa ina *megawatts* 100 na sasa hivi tuko *abourt* 80 na kuendelea. Pia, kutokana na hali ya uchumi wa Zanzibar ambayo Rais wetu wa kule Dkt Hussein Ali Mwinyi ya Uchumi wa Blue uwekezaji umekuwa mkubwa sana. Sasa uwekezaji huu hautoweza kufanikiwa kama itakuwa hatuna umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, kama tulivyoweza kuzungumza kwenye Kamati yetu; kwanza na-*declare* kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati hii; kwa hiyo, mengi yanayozungumzwa humu na ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Waziri ni kweli, na yote ameyafanya ni kutokana na ushirikiano ambao sisi tunampa ushauri halafu na wao wanauchukua na wanaufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana watu wa *TANESCO,* kwa upande wao wamekuwa wakiwasaidia sana watu wa *ZECO,* zaidi pale inapotokea hitilafu ya umeme mdogo au ukatikaji wa umeme upande wa Bara, yaani Ras Kilomoni kwa ajili ya kwenda Unguja na Majani Mapana Tanga kwa ajili ya Kwenda Pemba, nawapongeza sana wafanyakazi wa *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isipokuwa kwa kumalizia tu na si ka ajili ya muda kwa sababu leo hii katika jambo ambalo umetufurahisha Wabunge ni jinsi ambayo umetuelekeza kujibu hoja na kuuliza swali. Twende moja kwa moja; na mimi ndiyo maana nimeanza moja kwa moja, na huu ni mwendokasi. Nakupongeza sana kwa hili. S*tyle* hii tukiendelea nayo tutaweza ku-*manage* muda wetu. Waheshimiwa Wabunge tuko wengi na kila mmoja anataka kuchangia; na ili tuweze kuchangia ni lazima tu *manage time*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hongera sana na bila kusahau nataka nikwambie jambo lako ni letu sisi sote Wabunge humu ndani. Tuko na wewe, na tunajua una jambo lako lakini ni letu sisi. Ahsante

sana kwa kunipa nafasi hii nakupongeza wewe, Mheshimiwa Waziri na Wizara yote, naunga mkono asilimia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru; na mimi kwa kweli kama mwanamke na tunaoamini uwezo wa wanawake tuna kila sababu ya kuku-*support;* na *In Shaa Allah,* unaipeperusha bendera ya Taifa vizuri, uwezo wako si wa kutilia shaka, tunakutakia kila la heri. Ushindi wako ni ushindi wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwanza kabisa, Mheshimiwa January *my brother* na Naibu wake, naomba tu niwambie kwenye Jimbo la Bunda Mjini umeme umefika takriban vijiji vyote, lakini bado *speed* ya kuunganisha ni ndogo kufikia nyumba za watu, kufikia taasisi bado ni ndogo sana. Bunda umeshakuwa mji wanahitaji maeneo yote yawake umeme. Kwa hiyo, hilo nilisema na niliweke wazi.

Mheshimiwa Spika, kwanza Watanzania wote tumeona fahari ya Bwawa la Mwalimu Nyerere, hilo tunakubaliana kabisa. Lakini tunatamani uendeshaji wake, ukamilishaji wake uendane pia na thamani ya fedha ya Watanzania iliyowekezwa pale kwa sababu ni fahari ya nchi. Kwa sababu tunaamini ukikamilika *on time* utaweza kusaidia changamoto ya umeme hapa nchini, hilo hatubishi.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nina maswali yangu, natakiwa nipate majibu ya kutosha kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba ambao mmeingia na mkanadarasi unataka Mkandarasi akichelewa kukamilisha Mradi anapaswa kutozwa tozo. Sasa huu mradi umechelewa kwa sababu ulitakiwa kukamilika mwaka 2022. Hata hivyo unatakiwa ukamilike mwaka huu, ambapo zimebaki siku 13; na taarifa zilizopo hautakamilika *on time,* utakwenda mpaka

mwakani sijui tarehe 7 Juni. Je, kulikuwa na sababu za kutosha za mkandarasi kushindwa kutozwa tozo. Kwa nini *TANESCO* mpaka sasa hivi hawajamtoza mkandarasi tozo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutokukamilisha tu mwaka 2022 alitakiwa atozwe bilioni 329. Waheshimiwa wabunge, Serikali imekuwa ikichelewa tu kumlipa mkandarasi inatozwa tozo. Ukienda kwenye miradi ya barabara, ukienda kwenye miradi ya maji, kwa nini sisi tunapata kigugumizi kwa kuchukua pesa yetu? kwa nini *TANESCO* wanashindwa kuchukua hii tozo? Tunajua hata kama huko mbele walikosea lakini mwaka jana walishindwa kukamilisha mradi *on time,* mwaka huu mradi haukamiliki *on time;* kigugumizi gani kinakuwepo mkandarasi asitozwe tozo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hili tunawafanya wakandarasi waone Tanzania ni kichwa cha mwendawazimu, na kwamba wanaweza wakafanya wanavyotaka. Nilikuwa namsikia Mheshimiwa Jesca hapa, kwamba, mtu amekiri amepewa shilingi bilioni tatu halafu mambo yanaendela. Ni kwa sababu ya sisi kushindwa kusimamia mikataba yetu kwenye maeneo ambayo yanatu–*favor.*

Mheshimiwa Spika, na hii kwa upande wa *TANESCO* haijaanza leo, ukienda kwenye *Symbion,* ukienda kwenye *IPTL* ukienda kwenye *SONGAS* tunashida gani? Leo tena tunaona fahari ya kuwa na mradi wa Bomba la Gesi hatutaki haya yajirudie na ndiyo maana tunasema. Lazima tujifunze pale tunapojikwaa; hilo moja.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa mkataba, mkandarasi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere alipaswa kujenga miradi mbalimbali kwa ajili ya kutoa huduma za kijamii ya zaidi ya bilioni 200. Sasa mpaka sasa hivi mradi ambao unaenda kumalizika hatujui hizi huduma za kijamii zimefika wapi? Na ni haki yetu na aliji-*commit*, wakati haya yanaendelea yeye nasikia kwa mujibu wa mkataba, kwamba tulikubaliana anaweza tu akaongeza bei ya gharama ya mradi, na tuna taarifa ya kwamba anampango wa kufungua kesi; hili Mheshimiwa Waziri lazima utuambie limekaaje?

Mheshimiwa Spika, yeye hataki kutimiza masharti ya mkataba halafu huku yeye kwenye hicho kipengele ambacho kwa kweli mimi nakisema kibovu bado nasikia anataka kwenda kufungua kesi Mahakamani adai nyongeza wakati huku ameshindwa ku-*meet* vigezo vya mkataba. Tunajua kuna mitambo mingine inatakiwa ije mapema, inaingia tarehe nne mwezi *August* halafu bado ana-*guts* za kutaka kwenda kufungua kesi, hizi ni pesa za Watanzania.

Mheshimiwa Spika, na tunaamini kati ya mkandarasi anayelipwa vizuri *on time* ni huyo wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Kaka yangu umepewa dhamana, tunaamini tusirudie kule tulikotoka, lazima tuwasimamie hawa ili waweze kututendea haki Taifa letu na waheshimu Taifa hili lina wenyewe lina Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hizi fedha zitalipwa na walipakodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwa na Shirika la *TANESCO* ni fahari, tuna miradi mikubwa, Shirika hili lisipokuwa *stable* hawataweza ku-*manage* hii miradi ambayo tuna-*invest*. Tuna taarifa Shirika linadaiwa sana, Shirika linadai sana, *speed* ya kuhakikisha hili Shirika linakuwa *stable* iko wapi? Nitapenda kujua, kuna deni la muda mrefu la Serikali zaidi ya tirioni mbili, kuna deni la bilioni 720 la *TPDC,* lakini ukisoma taarifa mbalimbali Shirika hili la *TANESCO* lenyewe kuhimili madeni ya muda mfupi ni shida.

Mheshimiwa Spika, tunatambua jitihada za Serikali za ku-*invest* kwenye miradi mikubwa, miradi ya umeme inayohitaji uwekezaji wa kutosha lakini lazima tuwe na Shirika la *TANESCO* imara. Nini mkakati wa Serikali wa kuhakiksha Shirika la *TANESCO* linakuwa imara, linaweza kujiendesha likatengeneza faida? ni aibu kukaa humu Bungeni kuimba *TANESCO* inatakiwa iwezeshwe, *TANESCO* inatakiwa iwezeshwe kimuundo, iwezeshwe kimtaji, zaidi ya miaka kumi bado tunaenda ku-*invest* halafu Shirika ni hohehahe? Yaani ni sawa unanunua *furniture* kwenye nyumba ya udongo, *furniture* kali lakini nyumba ina ufa.

Mheshimiwa Spika, lazima hivi vitu vinaenda sambamba tuna-*invest* kwenye miradi tunahakikisha Shirika letu linakuwa *stable*.

*Waheshimiwa Wabunge yasije yakatukuta kama ya Afrika ya Kusini, leo wana mgao mkali kwa sababu gani? Shirika lao limeyumba, Shirika lao haliko stable*. **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, hii miradi tunayowekeza mikubwa ya gharama nafuu lazima Shirika letu litakaloenda kusimamia miradi hii liwe na uwezo wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kingine Mheshimiwa Waziri tunaomba utupe *status* ya umeme nchini ikoje? nilikuwa kwenye kamati Lindi, zaidi ya mara kumi umeme ulikatika. Umemskia Mbunge wa Kahama, umesikia taarifa iliyotolewa na Mbunge wa Mkoa wa Songwe, shida ipo lazima kama Taifa tuambiwe tatizo liko wapi maana kuna manung'uniko; ooo uchakavu wa mitambo, sijui nini;

Mheshimiwa Spika, sasa lazima kama Wabunge Wawakilishi wa Wananchi tupate maelezo sahihi *status* ya umeme nchini ikoje. Tunafurahi sasa hivi mkakati wako wa gesi lakini bado spidi ya uunganishaji wa gesi kwenye viwanda ni ndogo sana. Tunataka tujue kwenye viwanda peke yake zitatumika kiasi gani kujenga miundombinu ya gesi ili sasa viwango vyetu viwe na uhakika wa kupata umeme wa kutosha na waweze kuchangia uchumi kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Ester Bulaya umetumia mfano hapo wa Afrika Kusini na mimi sifahamu kama wanamgao na sijui sababu zinazosababisha mgao wao; na ili tusije tukaingia kwenye mgogoro wa Kidiplomasia kwa kujua kwamba nchi yao ilikuwa inajadiliwa humu ndani nafafikiri inabidi mchango huo tuuondoe ili tukae sawasawa. Mheshimiwa nakupa nafasi kwa sababu mwenyewe upo nilitaka umalize zile hoja zako nakupa

nafasi huo mfano wa Afrika Kusini ili tuuondoe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, sawa nauondoa.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, atafuatiwa na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, ajiandae.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji asubuhi hii katika Wizara yetu hii ya Nishati. Awali kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu Subhanahu Wa Ta'ala kwa kutujalia afya njema, uzima lakini pia kuendelea amani kutamalaki katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri January Makamba, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara kwa kweli wanafanya nzuri na mwenye macho haambiwi tazama kwa sababu ukienda kwenye maonyesho pale unajione mwenyewe. Kama leo Mtanzania Mheshimiwa Mbunge ambaye hajawahi kufika kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini ameweza kulionia akiwa Dodoma na ameliona si kwamba ameliona picha ameona kwa uhalisia kabisa. Kwa hiyo kweli huu ni ubunifa mkubwa na ni mapinduzi ya kiteknolojia na kiutendaji katika sekta yetu hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, mimi niende kwenye maeneo matatu makubwa na nianze tu kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuendeleza ushirikiano mzuri baina ya *TANESCO* na *ZECO* Zanzibar hali kadhalika baina ya Wizara ya Nishati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Tanzania Visiwani, ambayo ni Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli ushirikiano ni mzuri na ndiyo haya mwenzangu Kaka yangu Pondeza ameyazungumza hapa. Kwamba hivi sasa tumeweza kufika kile kilio chetu ambacho tulichangia hapa mwaka jana kwa sauti kubwa kwamba bei za Tanzania Visiwani na za Tanzania Bara ambao wote hawa ni raia wamoja na ni ndugu – kulikuwa kuna tofauti kubwa sana, na sasa

hivi ni furaha kwamba tumeambiwa kwamba hii kadhia imeweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, sasa ni ombi langu tu, kwamba tuwasiliane na wenzetu wa *ZECO* tukaone tafsiri ya haya mazungumzo na makubaliano tafsiri yake ikaonekane kwenye *bill*. Kwa sababu mimi nikiwa kama mtumiaji wa umeme bado ile tafsiri na mabadiliko hali sijayaona bado. Sasa ningeliomba tu kwamba haya mabaliko ambayo yanaonekana kwamba bei imekwenda kuwa *negotiated* na hadi sasa bei zinafanana basi ikaonekane kwenye *bill* ya mwananchi, kwa sababu siyo *fair* kwa Mtanzania huyu huyu ambaye kwenye Tigo, kwenye Zantel, kwenye *Vodacom* analipia sawasawa baina ya Tanzania bara na Tanzania Visiwani lakini umeme kuwe kuna tofauti. Nafikiri tunaamini kama hilo limekaa sawa ni vizuri na kama bado kuna tofauti ndogo tukarekebishe.

Mheshimiwa Spika, suala jingine ni kwanza nitangulize shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri kutokana na jitihada na tafiti ambazo zinaendelea katika vyanzo vingine vya umeme. Kwa sababu ni hatari kuendelea kutegemea vyanzo vya maji peke yake. Kama tunavyojua kwamba nchi hii iinakabiliwa kama ilivyo dunia kwa ujumla na mabaliko ya Tabianchi na hatujui siku gani utakuja ukame wa kutisha na vyanzo vyetu vya maji vije viweze kuteteleka na hapa itakuwa hatuna msalia Mtume isipokuwa tukangalie vile vyanzo ambavyo havitegemei maji moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningelimuomba tu Mheshimiwa Waziri hapa atengeneze jitihada. Mwenzangu Mheshimiwa Sanga jana amezungumza hapa, kwamba kuna maeneo tayari ameshafanyia tafiti kama Makambako, lakini yapo maeneo mengi Tanzania kuna maeneo ambayo yana-*potential* ya umeme wa jotoardhi, umeme wa *solar* na umeme wa upepo. Sasa nafikiria maeneo ambayo tayari tafiti zimeshakamilika sasa nafikiri tuende tuka-*invest* ili angalau tupate *megawatt* chache za kuweza kuziweka kama akiba ili siku ambayo tutateteleka kwenye maji basi angalau tutakuwa tuna sehemu ya kukimbilia.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu ya mchango wangu niende kwenye ile ambayo jana alizungumza hapa Mheshimiwa Waziri, ile kuhama kutoka kwenye nishati chafu ya kupikia na kwenda kwenye nishati safi na salama ya kupikia. Na hapa tena niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa ambayo anayaifanya, na niombee Mungu mradi wa *LNG* nao uende ukafanikiwe haraka ili uende ukaongeze ufanisi katika hili.

Mheshimiwa Spika, hapa pia nafikiria nimuombe tu Mheshimiwa Waziri tujitahidi kadri inavyowezekana, kwa sababu kama tunavyojua, kwamba bado kuna jitihada nyingi zinaendelea katika nchi hii katika suala la kuhama au *shifting* kutoka kwenye kutumia nishati chafu hii na kwenda kwenye nishati safi na salama. Wenzetu wa misitu wanafanya kazi hiyo, wenzetu wa mazingira wanfanya kazi hiyo. Sasa hivi jitihada twende tukazichanganye kwa pamoja ili tuweze kupata ufanisi mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Tanzania inapoteza takriban hekta laki nne kwa mwaka. Na hekta hizi laki nne ambazo zinapotea kwa mwaka ndizo ambazo zinahifadhi na zinatiririsha maji kupeleka kwenye vyanzo vyetu vya umeme vya Kihansi, Pangani, Mtera, hali kadhalika na chanzo cha umeme ambacho sasa hivi tunakitegemea cha Bwawa la Mwalimu Nyerere. Sasa iwapo misitu hii itaendelea kupotea basi ni hatari kubwa kwa *investment* kubwa ambayo inafanywa na Serikali kwenye miradi yetu ya maji. Kwa hiyo, ningeliomba tu Mheshimiwa Waziri akajitahidi kukaa na wenzake hawa wa sekta ya TAMISEMI ili kuangalia wanafanya jitihada hizi kwa kiasi gani ili kuzichanganya kwa pamoja ili ziweze kuleta tija.

Mheshimiwa Spika, lakini pia ombi langu, tusije tukavamia tukachukua *regist*er kwamba hizi nishati mbadala ziende kwa kila mahali Tanzania zienee. Ningeliomba tu kwamba tukaangalie uwezekano wa maeneo mbalimbali ambayo yako *very strategic,* ambayo ni *potential.* Kuna maeneo ambayo yana misitu na kasi ya kupotea kwa misitu ni kubwa; twende huko tukashambulie kwanza kabla hatujaenda kuangalia kila mahali. Kwa hiyo kwa utaratibu wetu sisi hasa Wizara ya Nishati tukaangalie maeneo

ambayo yanatuhusu zaidi kwanza halafu tena baadaye ndipo tukaangalie upande mwingine.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa *promotion* ambayo anaendelea kuifanya. Waheshimiwa Wabunge hawa walifanya kazi kubwa kipindi cha sensa, walifanya *promotion* ya sensa na Tanzania nzima ilisimama na matokeo yake matokeo ya sensa sisi tunayajua. Kwa hiyo nafikiria na hii *promotion* ambayo unajumuisha Wabunge katika uendelezaji wa nishati safi na salama basi hii inakwenda kuzaa matunda makubwa, kama ambayo ulitufunza.

Mheshimiwa Spika, nishukuru na niunge mkono hoja kwa asilimia 100. Ahsante sana

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo atafuatiwa na Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Wizara hii muhimu, lakini pia nataka nikuahidi kwamba nitaenda hoja kwa hoja.

Mheshimiwa Spika, hali ya upatikanaji wa umeme nchini ipo katika sura mbili. Sura ya kwanza ni utekelezaji wa miradi mikubwa ya kuzalisha umeme lakini vilevile na miradi mikubwa ya kusambaza umeme. Sura ya pili ni kuunganisha umeme kwa watumiaji; ndivyo ilivyo hali ya upatikanaji umeme.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nijikite kule kwenye kuunganisha umeme. Hali ya kuunganisha umeme kwa watumiaji bado si nzuri; na siasa kubwa ya umeme kule kuwaunganishia watumiaji hali yetu bado si nzuri.

Mheshimiwa Spika, mimi kwenye jimbo langu vijiji vyote vimepata umeme lakini vitongoji takriban vyote havina umeme. Na bahati mbaya *REA* walikuwa wakishafikisha kwenye Kijiji wanalambisha umeme basi, kisha wanaondoka. Na kitu

ambacho nashangaa hata zile *scope* nani alikuwa anaenda kukagua? Maana yake ni mtaa mdigo unalambishwa na kijiji kiwe tayari kina umeme.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo mawili ambayo mimi nataka Serikali iwe *bold*. Suala la gharama ya kuunganisha umeme kwa 27,000 hebu Serikali ilijadili jambo hili, je, ni jambo la kiuhalisia? Maana sisi tumesema sana kwenye mikutano kwmaba umeme ni 27,000, lakini uhalisia siyo 27,000. Serikali iseme, kama inatakiwa kiasi fulani iseme kwa uhalisia wake. Wananchi wanajiunganishia umeme wanaweka ile *connectivity* ndani, kwa maana ya miundombinu, lakini akija kwenye kuunganishiwa 27,000 wanaambiwa kuna nguzo moja inatakiwa ije kwako inabidi utoe 300,000. Jambo hili wananchi wanashindwa kuelewa. Lakini *mentality* ya *TANESCO* inaangalia, kwamba kitongoji kile kina watu wachache na hivyo tukipeleka umeme hatina wateja. kwa hiyo kuna *conflict* hiyo.

Mheshimiwa Spika, mimi nashauri kuwe na muundo mathubuti, muundo wa kwanza *REA* iendelee na shughuli ya miradi mikubwa, iwe kama na sura ya *TANROADS,* lakini vilevile tuwe na Wakala wa Umeme Vijijini ambaye sasa ata-*deal* yeye na ku-*connect* kwenye vitongoji atafute nguzo atafute *transformer* ili kazi ya kuunganisha aifanye yeye; lakini anayehusika na wateja ni *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* sasa yeye ni kuangalia namna gani anaweza kupata fedha baada ya wananchi kuunganishiwa umeme. Tukienda na muundo huu hali yetu ya upatikanaji umeme na kuunganisha umeme kwa wananchi itakuwa imekaa sawasawa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tuwe na *REA* ambasyo itakuwa na sura kama ya *TANROADS* lakini tuwe na Wakala Umeme Vijijini ambaye atakuwa na sura kama ya *TARURA* halafu *TANESCO* yeye a-*deal* sasa na masoko, namna gani anaendesha Wananchi wapate huduma ile sasa ya umeme.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba Serikali ikiwezekana wakati Waziri ana *wind up* tupate uhakika kwamba 27,000 inakidhi au 27,000 haikidhi? Kama kuna kiwango ambacho tunaona inafaa basi ipendekezwe na wananchi wataona kweli hiki kina uhalisia, lakini tunavyoenda hivi kila mmoja anamdanganya mwenzake, sasa hatuwezi kwenda na utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kuhusu suala la nishati ya umeme katika maeneo mbalimbali *(power mix)*. *Private* sekta inakuja na miradi kama ya *solar* kutaka iweze kuiuzia *TANESCO* umeme. Lakini mimi nataka niseme pamoja na sera yetu kusema hivyo lakini kuna uzito mkubwa sana. Ili kuja kupata mradi wa *sola*r uiuzie *TANESCO it takes ages,* na ni ngumu kweli kweli. Sasa turuhusu watu waje tupate umeme wa kutosha watu waweze kujiunganishia. Lakini ni jambo gumu kweli kweli kwa mtu mwenye kutaka kuzalisha ueme lakini hata *tariffs* ambazo inatakiwa walipe haziendani na namna ambavyo wameweza kufanya kazi ya kuwekeza hili suala hilo; kwa hiyo nilikuwa naliomba hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni kuhusu upatikanaji wa vifaa. Kinachosumbua tusiunganishiwe umeme vijijini ni kukosekana kwa *transformer* na kukosekana kwa nguzo. Haijulikani, na ndilo jambo gumu. Kule kwenye ofisi za *TANESCO* wanasubiri wapate nguzo, wanasubiri wapate *Transformer, transformer* hazipatikani. Sasa jambo hili kuna kipindi tulizuia hakuna *transformer* kutoka nje zitengenezwe hapa ndani. Sasa Mheshimiwa Waziri aje atuambie kama tunaruhusu *transformer* zije kwa wingi lakini na shida ni nini, nguzo tunazalisha hapa kwetu, na zenyewe nazo tulizuia kwamba zisitoke nje ya nchi kama inawezekana nguzo zije za kutosha za ndani ya nchi na hizo zitakazotoka nje ili kwamba kuwe na uhakika wa kupata nguzo, hapo ndiyo tutaenda kila kitongoji kitapata umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lengo la Mheshimiwa Waziri, hata mwaka jana, alitaka vitongoji vyote vipate umeme. Lakini kuna uzito, hata hivi 15 bado ni vitone vya maji. Kwa hiyo, jambo hili nalo tuliangalie ni namna gani tunakuja na utaratibu madhubuti, kwanza kimuundo, kwa maana ya kuwa na wakala

wa usambazaji wa umeme vijijini lakini *REA* yeye awe na sura nyingine ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine ni kuhusu usambazaji wa gesi. Mkoa ambao unakula mkaa kwa wingi ni Mkoa wa Dar es Salaam. *TPDC* wana mradi wa kusambaza umeme kwenye nyumba, lakini jambo hili nalo haliendi sawa sawa. Serikali iangalie, kama *TPDC* hawezi basi apatikane muwekezaji ambaye ataweza kufanya kazi ya kusambaza umeme. Kufanya hivyo tutazuia matumizi ya mkaa kwenda Dar es Salaam na tutailinda miti yetu. Kwa hiyo jambo hili nalo liweze kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine, nimepitia maoni ya Kamati. Kamati inaongelea habari ya kwamba *TBS* kwenye suala la vinasaba ipewe uwezo, ijengewe uwezo wa kutosha na ipewe muda ili iweze kuja na utaratibu wake. Jambo hili ni zuri; lakini kwa maana nyingine tena tayari *tender* imetangazwa kwamba ipatikane kampuni ambayo inaweza kufanya kazi ya vinasaba. Kwa hiyo kuna *contradiction* kati ya Kamati lakini mimi nachotaka kusema hali ambayo *TBS* ilichukua, ilichukua katika wakati mgumu sana na jambo hili *TBS* wamejitahidi. Sasa kama Serikali inaona ipo haja tuone kwa nini tunatoka tunamuacha *TBS* ambaye katupitisha kwenye kipindi cha mpito kama kuna mambo ya kurekebisha basi yaweze kurekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi mimi naipongeza sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Sisi sasa katika ukanda huu wa Afrika hasa hasa Kusini mwa Afrika tunaingia katika idadi ya nchi ambazo zina umeme mkubwa na tunaweza kusambaza nje. Nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri. Wizara hii ni kubwa, ina mambo mengi na Wizara yenye mapambano mengi; lakini anafanya kazi kubwa na aendelee kufanya kazi kubwa ili kwamba Taifa letu liwe na umeme wa uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Flatei Gregory Massay atafuatiwa na Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel ajiandae.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa nafasi. Kwanza nimshukuru Mungu kwa kutupa uhai siku ya leo, lakini pili nitoe shukrani zangu kwa Serikali hasa wakati huu ambapo sisi wa vijijini tunaonekana. Shukrani zangu zimwendee Rais Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayofanya lakini pia Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Nishati na Ndugu yangu Byabato Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeyasema haya makusudi kwa sababu mwaka juzi Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja kuzindua umeme katika Mkoa wa Manyara, aliuwashia kwenye Kijiji kilichoko katika Jimbo la Mbulu Vijijini Mungahay; na kule tulikupa jina nafikiri unalikumbuka; tulikuita *"Tlhaqwe"*. Hilo jina ni maarufu sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Na tulikupa kwa sababu umewasha umeme kwenye vijiji ambavyo kwa kweli vilikuwa ndani sana. Sasa baada ya kuja kuwasha umeme kwa kweli mambo yamekwenda siyo mabaya ndiyo maana natoa pongezi hizi kwa Wizara. Lakini kubwa zaidi vijiji vyetu viko 76 na 43 vimepata umeme bado 33. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naona Mheshimiwa Waziri ni kijana na ni kijana mwenzangu ambaye tumefanya mengi. Wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini kwanza wanafaidi sana jambo la umeme kwa sababu sisi kule bahati nzuri tuna viwanda vingi, na sisi ni wakulima, na unajua haya, na umefanya ziara mara nyingi katika eneo letu. Sasa nikuombe kabla sijasahau, hivi vijiji 33 ndugu yangu mtupatie namna ya kuvimaliza haraka. Kwa nini? Tofauti ya majimbo yetu ya vijijini yana kilometa nyingi kufikia kijiji hadi kijiji. Tuna mkandarasi kweli anafanya kazi yake lakini kwa kweli amefanya kazi taratibu mno kutoka wakati huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu, muwezesheni huyu mkandarasi. Mimi sina shida naye lakini ukweli ni kwamba anajitahidi; inawezekana lakini kwa sasa kwa kweli sitaki kumlaumu au kumtuhumu kwa sababu ni ndugu yetu anafanya

kazi yake kadiri anavyoweza; lakini kwa kweli kwa sasa hajabahatika kuwasha vijiji 10. Sasa sina hakika mnafanyaje mtusaidie sisi, ni kilio cha wananchi wa Mbulu. Mtusaidie kwa kweli, muwezesheni. Matatizo yake, ninavyo sikia sina hakika, analia sana fedha hajawezeshwa sijui inawezekana vipi mumsaidie. Kwa kweli mumsimamie amalize hivyo vijiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo lililoko kwetu sisi kutoka kijiji kimoja hadi kwenda kijiji kingine anahitaji kujenga zile nguzo kubwa kilometa 25, kilometa 20, kilometa 30 na hizo ndizo zilizobaki na kule kwangu kuna kata tatu. Kata ya Yaeda Chini, Kata ya Eshkesh; na hizo kata nazozisema Mheshimiwa Waziri ni kata ambazo kwa kweli ziko kwa Wahadzabe; na katika eneo la Tanzania hii, Wahadzabe wako kwangu. Ningefurahi, Mheshimiwa Waziri hebu weka *legacy,* sijui nisemaje kwa Kiswahili sanifu. Weka historia, wewe uwe Waziri wa kwanza kuwapelekea Wahadzabe umeme kwenye Vijiji vya Munguamollo, Dumanga, Yaeda Chini pamoja na Eshkesh. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo vijiji nimevitaja Mheshimiwa Waziri hivyo ndivyo vijiji vya Wahadzabe ambao kimsingi wakipata umeme, mimi naamini watatoka kule vijijini, huwa mara nyingi wanakaa kwenye mlima na wanarina asali na kupata mizizi ya miti.

Mheshimiwa Spika, na wakati wa sensa, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ilibidi tuwinde wanyama wa pori waje kula na tuwahesabu. Kwa hiyo, ukishawapelekea umeme Mheshimiwa Waziri ni wazi kwamba wale ndugu zangu watakuja wakiwa wame-*settle* mahali, watakaa kwenye majumba yao wapate umeme. Nina hakika ukija Mheshimiwa Waziri utafurahi sana. Hawa ndugu zangu kwa kweli kwanza wameenda shule, lakini pili wanataka maendeleo na tatu kwa sababu hiyo basi utakapowapelekea maendeleo hasa haya ya umeme ni wazi kwamba nyumba zao zitawaka umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nyumba zao si kama nyumba hizi za kwetu ambazo umezizoea, wana nyumba za asili ambazo naamini wakishawasha umeme kule watakaa na kuendelea

kukaa maeneo hayo. Kwa hiyo niombe sana hilo. Na hizo kata kwa kweli ni muhimu sana kwa sababu tangu dunia imeumbwa hawajawahi kuona waya wa umeme, na kwa sababu hiyo basi na mimi nadhani muone namna gani utaratibu wa kuwasaidia hawa wakandarasi wanaokuja vijijini kwa sababu moja; wakandarasi wa mijini wao wanakuja na ile kushusha umeme mnaita *underline*. Sasa kwao ni rahisi sana kupata fedha na kuweza kujilipa na kuendelea lakini wakandarasi kwenye jimbo langu mimi wanahitaji hela nyingi kabla ya kuanza kutekeleza huo mradi. Kwa mfano, kwa vijiji hivi 33 ukiangalia urefu wao, umbali ni mkubwa sana. Ninaona wanakazana wamepeleka maeneo nguzo lakini sasa namna ya kufikisha umeme hapo imekuwa tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ombi langu lingine kubwa, nimeona kwenye bajeti yako, nikupongeze sana, bajeti imekaa vizuri na nimeona kabisa umeweka *deadline* unakwenda kumaliza vijiji vyote. Nimefurahi sana kusikia hivyo, na nikupongeze kwa hilo. Na ninashukuru sana Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kuweka fedha ambazo kila kijiji kinakwenda kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi muondoe ule utaratibu wenu wa ujazilizo. Kwa sababu ujazilizo maana yake nini; mnapeleka umeme halafu baadaye mnajaziliza sehemu ambazo hazikupata umeme. Sasa, kwa mimi wa vijijini kwa sababu sijapata kabisa kitu kinachoitwa umeme kwa hiyo ni wazi kabisa sitapata nini? Ujazilizo. Kwa hiyo, mtuone sisi wa vijijini ambao hatuna namna yoyote ya kupata huo umeme, haujafika bado, mtuwekee *share* au akiba kwa sababu sisi ni wananchi pia ili basi mnapopeleka umeme sisi tuwe na *share* yetu ya ujazilizo. Kwa sababu mnapeleka umeme aidha kilometa moja, na kwa sababu sisi pia hatukupata kwa sababu tu ya mazingira tuliyokaa, lakini basi muone mtakavyopeleka umeme huo ujazilizo ambao mjini wanapata sisi tupate na *share* yetu iwepo. Nimesema hivyo makusudi kwa sababu hamna namna nyingine nitaweza kupata umeme ikiwa ujazilizo utapita *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi nimeona kabisa vitongoji. Mimi vitongoji vyangu ni vingi, viko vitongoji 400,

naomba Mheshimiwa Waziri uone hilo. Vitongoji kule kwangu ni sawa sawa na kijiji na tofauti kabisa na maeneo ya mjini. Na utakumbuka amechangia mchangiaji mmoja hapa, sisi wa vijijini na hali ya milima na miteremko kule inahitaji uangalifu wa kutosha sana Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo ombi langu mimi, wakandarasi walioko kule mjaribu kuwa-*treat* tofauti na walioko mjini. Si kwamba nawatetea bali ninaona hali ya mazingira yetu yalivyo kule. Kwa mtu wa kawaida huwezi kutekeleza mradi ambao unaonekana upo katika milima na maporomoko kutokana na hali yao ya kuwapatia fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa nikuombe, ushauri wangu kwa Wizara yako, na huu nadhani ukiupokea utakusaidia. Kuna gesi tumekuwa tukiisema muda wote na muda wote tumeona mkifanya vizuri. Mtwara naona wameanza kazi nzuri, kuna majengo au nyumba 223 ambayo nafikiri yameingia gesi lakini kuna gesi ambayo tunataka kupeleka kwenye magari na mitambo hii ya kuendesha nini? tunasema kwa mfano gari. Mimi ningefurahi sana hata gari langu kupata gesi, kuondoa kitu kinachoitwa *carburetor* na kuweka gesi. Mimi ningeomba hapa Dodoma muweke kituo kikubwa cha ku-*supply* hiyo gesi, itasaidia sana. Muanze na majengo ya Mawaziri hapa na Naibu Mawaziri, itatusaidia sisi kufanya uhamasishaji na sisi tutajiunga huko. Maana kwa mfano ukijaza gesi Dar es Salaam ukija nayo Dodoma si imekwisha? Utajazia wapi? Naomba sasa muone namna gani Mheshimiwa Waziri, kwa sababu wewe ni kijana na Naibu wako wote ni vijana. Mimi nina hakika mtatupeleka kwenye ulimwengu mzuri wa kupunguza matumizi hasa haya ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naona kengele imelia nakushukuru sana. Ahsante kwa muda, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba atafuatiwa na Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Ole Mollel, Mheshimiwa John Marko Sallu ajiandae.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu kabisa. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi

Mungu kwa kunijalia afya nzuri na leo hii nikaweza kusimama katika Bunge hili. Lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa January Makamba na Naibu wake, wajomba zangu wale wote wawili, kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha Watanzania wa mijini na vijijini wanapata huduma hii muhimu ya nishati ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini, nina vijiji 24 ambavyo vinahitajika kuwashwa umeme. Vijiji tisa kati ya 24 ndivyo vimewashwa umeme, vijiji 11 bado vinaendelea, mkandarasi yupo *site* anaendelea na kazi; vijiji vinne bado kabisa havijafikiwa kuwashwa umeme. Kwa maelezo ya mkandarasi amezungumza mpaka kufikia Desemba vijiji vyote 24 vya Mtwara Vijijini vitakuwa vimewashwa umeme. Kwa hiyo nimuombe mkandarasi ambaye anashughulika na suala hili katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini aongeze *speed* ili mpaka kufikia Desemba basi vijiji vyote viwe vimekamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, gesi hii inatoka katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini katika Kijiji cha Msimbati, lakini kwa masikitiko makubwa sehemu ambayo inatoka gesi asilia umeme unawaka maeneo ya barabarani, ukiingia ndani hakuna umeme. Vijiji na vitongoji vingi umeme hakuna katika Kijiji hiki cha Msimbati ambapo gesi hii asilia inatoka. Kwa hiyo hii ni aibu, ni aibu kubwa sana. Niombe sana Mheshimiwa Waziri, wewe ni msikivu sana, nikuombe Kaka yangu tuhakikishe vijiji hivi vinapatiwa umeme haraka sana kutokana na umuhimu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vijiji ambavyo vina shida ya umeme ni Kijiji cha Mnuyo katika Vitongoji vya Mnamba, Bumbwini, Lianje pamoja na Vitongonji wa Najibu na vitongoji vingine vingi sijavitaja. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana, sehemu hii ni sehemu muhimu, sehemu hii ndio sehemu ambako gesi inatoka. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri wananchi hawa waweze kufurahia huduma hii ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sehemu ambayo gesi inachakatwa, Madimba, maeneo mengi na vijiji vingi navyo hakuna umeme. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, nayo sehemu hii kwa

umuhimu wake naomba umeme ufike kwa haraka kwenye vijiji pamoja na vitongoji. Kwa mfano Vitongoji vyote vya Mahiva, Uvikwani, Litembe, Miembeni, Namnaida *B*, Namindondi pamoja na Mitambo Shuleni hakuna umeme. Hii ni aibu kubwa kweli kweli kwa sababu maeneo haya sehemu ambayo gesi ipo, sehemu ambayo inachakatwa gesi umeme hakuna. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, na nikushukuru Mheshimiwa Waziri, kwa moyo wangu wa dhati kabisa, nilizungumza na wewe nikakueleza juu ya changamoto hizi, nashukuru Mheshimiwa Waziri jitihada ambazo umezichukua zinaendelea kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa hivi ninavyozungumza…

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatokea wapi? Aah! Mheshimiwa Shamsia Mtamba kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Soud.

**TAARIFA**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa Shamsia kwamba ni utaratibu ambao Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania umeuwekwa kwamba wale ambao *either* kama ni *source* ya maji au ni ya umeme basi kwanza waanze kupata umeme wao kabla ya kusambaza katika maeneo mengine. Kwa hivyo kama kweli kuna maeneo ambayo gesi inapita lakini hao hawanufaiki nayo basi nafikiria Mheshimiwa Waziri lazima ajitahidi awa *support* hao.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia Mtamba unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninaipokea tena kwa mikono miwili.

Mheshimiwa Spika, sehemu hii ya Msimbati na Madimba ni sehemu muhimu sana, na nimekuwa nikisema katika Bunge hili;

barabara mbovu hakuna, huduma ya nishati ya umeme ndio kama hivyo hakuna, miundombinu ya watu wale maskini ya Mungu ni duni. Kwa hiyo, sehemu kama hii ni sehemu ya kuiangalia sana, sehemu kama hii inahitaji miundombinu ya shule nzuri ziwepo, maeneo haya shule nzuri hakuna, miundombinu ya afya, huduma za afya nzuri katika maeneo haya inahitaji ziwepo lakini miundombinu hiyo hakuna. Kwa hiyo ninaipokea taarifa ya Mheshimiwa kwamba maeneo haya ni lazima wayaangalie kwa macho mawili kutokana na umuhimu wake. Watu wale wanaweza wakahujumu kule. Kwa hiyo lazima Serikali muone umuhimu wa Vijiji vya Msimbati na Madimba, muwawekee mambo mazuri ili wananchi wale basi wafurahie na neema hii waliopewa na Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwisho kabisa ni kusisitiza. Mheshimiwa Waziri, kwanza tunakushukuru kwa unyenyekevu wako na usikivu wako. Tumekaa kikao na wewe sisi Wabunge wa Mtwara, na Wabunge wa Mtwara kwa kweli tuna changamoto kubwa sana ya umeme. Tuna changamoto kubwa wananchi wetu wanalalamika, wananchi wetu vitu vyao vinaungua, wanapoteza vitu vyao kila siku kutokana na changamoto ya umeme ya kukatika katika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri tunakuomba sana tuliyoyakubaliana kwenye kikao yafanyike kwa wakati na uamuzi mzuri uliouchukua wa kuhakikisha unakuja kutatua changamoto ya umeme katika Mkoa wetu wa Mtwara ndani ya siku 90 basi Mheshimiwa Waziri tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu uweze kutimiza hili ili wananchi wa Mtwara waweze kufurahia huduma hii bora, huduma hii muhimu ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo mengi kwa kweli yamesimama, mambo mengi hayaendi, viwanda vingi sasa hivi wawekezaji wanashindwa kuja Mtwara kutokana na umeme kutokuwa wa uhakika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe, wewe ni mtu msikivu wewe ni mtu ambaye unafikika, wewe ni mnyenyekevu njoo umalize tatizo la umeme katika mkoa wetu haraka. Njoo umalize tatizo la umeme katika Mkoa wa Mtwara kwa uharaka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Ole Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa John Marko Sallu, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos ajiandae.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu ambayo ndiyo inafanya Taifa letu liwe na mwanga kila saa.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru wewe mwenyewe kwa jinsi ambavyo unaongoza Bunge letu na niseme tu kwa moyo wa dhati kwamba wewe ni Spika ambaye nimeona na nadhani kwa sababu ya taaluma yako ya sheria ndio maana unatuongoza vizuri katika Bunge hili. Kwa kweli Mungu akubariki sana. Lakini nikutakie kila la kheri katika safari yako ya shughuli iliyoko mbele yako. Mungu akutangulie na naamini utashinda kwa sababu una uwezo mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme pia nimshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaongoza Taifa letu na kusimamia kila Nyanja ya Taifa letu kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata huduma mbalimbali katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini nitakuwa mwizi wa fadhila nisipompongeza pia Mheshimiwa Waziri, Ndugu yangu Makamba pamoja na wasaidizi wake Naibu Waziri pamoja na Wizara nzima kwa ujumla wataalamu ambao wanamsaidia. Kwa kweli mnachapa kazi na mnajitahidi pamoja na changamoto nyingi ambazo mnakabiliana nazo. Mwenyezi Mungu aendelee kuwatia nguvu ili muendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais akatekeleze majukumu haya na wananchi waendelee kumwamini, na *In Shaa Allah* Mungu akijalia aendelee kuongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, kwanza mimi niseme tu kwamba bajeti hii nimefarijika na ninaipongeza kwa sababu moja tu; nikiangalia jinsi ambavyo bajeti hii ni ya shilingi trilioni tatu na bilioni karibu 48 na *point* juu; lakini ukiangalia Wizara imekuja na kwamba ujenzi wa

miundombinu ni asilimia 97.1. Hiyo tu peke yake mimi ilinifanya nione kwamba hawa watu wako *committed,* kwamba kweli wanataka kupunguza changamoto za wananchi. Matumizi ya kawaida ni asilimia 2.9 tu. Hapo peke yake imenionesha kwamba kwa kweli Wizara hii iko kwenye mazingira ambayo ya kujisikia kwamba ingetaka kuondoa matatizo yote ya umeme katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama tujuavyo, changamoto zinakuwepo tu kwa sababu ya *resources* tulizonazo, kwamba hazitoshi. Na kwa sababu hazitoshi ndiyo maana sasa unaona tunaendelea kuzungumza katika Bunge hili kuiomba Serikali sasa ione ni jinsi gani inaweza kuhakikisha kwamba changamoto zilizopo za upatikanaji wa umeme katika maeneo yetu, katika vijiji, kata na vitongoji viweze kuwepo umeme katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye Jimbo langu la Arumeru Magharibi; mimi nina kata 27, vijiji 86, vitongoji 268. Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kusema kwamba atatupatia vitongoji 15 kwa kila Jimbo; lakini katika vitongoji mia mbili karibu 68 ukitoa vitongoji, 15 hebu fikiri kwamba hali itakuwaje huko kwenye jimbo? Kwa hiyo bado tunaiomba Serikali ione ni jinsi gani itahakikisha kwamba inatupunguzia adha hii sisi Wabunge kwa sababu tunapokuwa majimboni, tunapokuwa kwenye ziara mbalimbali changamoto kubwa wananchi wanatudai umeme na wanasema mbona umeme hakuna? Tunajaribu kwaambia Serikali imeanza mchakato wa kuhakikisha kwamba kila kijiji inapata umeme halafu tutakuja kwenye kitongoji. Sasa katika bajeti hii vitongoji 15 bado tunaona kidogo Serikali ingeangalia, na hasa Wizara ingeangalia namna ambayo itatufikisha.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu la Arumeru Magharibi katika vitongoji vingi, ambavyo siwezi kuvitaja, lakini kata ambazo mpaka sasa vitongoji vyake havina umeme ni vya Bwawani, Oljoro, Nduruma, Musa, Mwandeti, Oldonyo Sambu kwa maana ya Kata ya Otoroto, Mlangarini, Sambasha, Oldonyo Sambu, Oldonyouwas, Lengijabe, Lemanyaka, Kimnyak. Vitongoji vya hiyo kata hizi zote ambazo nimezitaja bado havina umeme; na

wananchi wetu katika kata hizo nilizozitaja hawako mbalimbali, kwa maana hawako *scattered,* wako karibu karibu kabisa; kwa hiyo wanahitaji umeme kwa kiwango cha hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na unajua umeme ni sehemu kubwa sana ya maendeleo. Kama ni kuchaji simu, uchomeleaji, kusaga mahindi, na kufanya mambo mengi basi wananchi wanategemea kupata huduma ya umeme ili mwisho wa siku basi waendelee kufurahia huduma kutoka kwenye Serikali yao. Mheshimiwa Waziri nikuombe sana, Jimbo la Arumeru Magharibi ni jimbo moja gumu mno, na ugumu wake miundombinu yake jinsi ilivyokaa ramani yake imekaa vibaya, na hivyo niombe sana kwa kweli ujaribu kutusaidia kwa sababu wananchi wanahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo kuna suala la uimarishaji wa *TANESCO. TANESCO* inahitaji kuimarishwa. Niwapongeze Wizara kwa sababu mmefanya mabadiliko makubwa hivi karibuni katika hiki kipindi cha mwaka mmoja, naona kama kuna mabadiliko makubwa ndani ya *TANESCO* kiasi fulani lakini bado mnahitaji kufanya kazi kubwa kurekebisha *TANESCO;* lakini pia *TANESCO* isaidiwe kupata fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiachilia madai makubwa, yale ambayo yametajwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, nikiangalia mfano taasisi za Serikali. Taasisi za Serikali hazilipi bili za umeme, ni kwa nini? Ukisoma ripoti ya Kamati, taasisi za Serikali tu peke yake inadaiwa zaidi ya bilioni 334, hazilipi. Naomba hili nalo liangaliwe, *TANESCO* ipewe nguvu. *TANESCO* bado haina nguvu kwa upande wa madeni makubwa, lakini pia Serikali na taasisi za Serikali zinavyotumia umeme hailipi ina maana gani? Kwa hiyo naomba kama taasisi hizi kwenye bajeti zao zimeweka ulipaji wa bili ya umeme kwa nini wasilipe? Mheshimiwa Waziri *TANESCO* wasaidiwe wawakatie umeme. Wakiwakatia nafikiri watashtuka na watalipa bili. Hii siyo sawa, tutakuwa tunawaonea *TANESCO* lakini hatuwasaidii.

Mheshimiwa Spika, Namshukuru sana Meneja wangu wa *TANESCO* Mkoa wa Arusha kwa sababu anajitahidi sana. Ukimpigia simu saa yoyote maskini ya Mungu anapokea, ana-

*deal* na mambo makubwa makubwa magumu. Kwa kweli nampongeza sana na ninashukuru sana kwa sababu ni mtu msikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la uunganishaji wa umeme. Uunganishaji wa umeme bado hatuelewi vizuri kama Wabunge na hata Watanzania hawaelewi; kwamba, ni wapi ambapo ni shilingi 27,000, ni wapi ambapo labda inatozwa nguzo moja shilingi laki tatu karibu na 60, ni wapi inakuwa sijui ngapi? Hili nalo Mheshimiwa Waziri inabidi Wizara iliangalie sana na itoe kabisa *schedule* ambayo nchi nzima itajulikana. Kama maeneo yametofautiana basi iwekwe vizuri. Kuna wananchi unakuta nguzo imefika mpaka kwake, Serikali imefikisha nguzo pale lakini insahindwa kuvuta umeme kwa sababu ya gharama kubwa. Kwa hiyo hebu tuangalie ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu hawa waweze kuendelea kufurahia matunda ya nchi yao na hasa kuhakikisha kwamba siku zijazo Chama cha Mapinduzi kinaendelea kung'ara ndani ya nchi yetu na kuendelea kutawala vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshawataja Wabunge watakaoendelea hapa, lakini nimeletewa hoja na Mbunge kuhusu akidi hapa ndani. Sasa kabla hesabu haijafanyika Wabunge walioko nje wapigiwe kengele warejee ndani ili tuweze kujua akidi ipo ama haipo. Wabunge walio nje wapigiwe kengele Katibu wa Bunge atafanya zoezi hilo halafu tutafanya kazi ya kujua kama akidi tunayo au hapana kwa mujibu wa Katiba yetu na Kanuni zetu.

*(Hapa kengele ilipigwa ili Wabunge waliokuwa nje ya ukumbi warejee ndani ya ukumbi)*

**SPIKA:** Nilikuwa nimeshamwita Mheshimiwa John Marko Sallu atafuatiwa na Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. JOHN M. SALLU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata nafasi hii. Kwanza nikushukuru sana kwa jinsi unavyotuongoza na unavyotulea, na jambo lako ni jambo letu na *Insha Allah* Mwenyezi Mungu ataliwekea mkono litakwenda kwa kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumshukuru sana Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupa fedha nyingi ambazo zimeendesha miradi mingi katika majimbo yetu hususan Jimbo langu la Handeni Vijijini. Kwa kweli tunamshukuru sana kwenye Jimbo letu la Handeni Vijijini ameleta fedha ambazo zimeendesha miradi mingi sana ya maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumshukuru ndugu yangu January Makamba, Naibu wake Byabato, Katibu Mkuu Ndugu yangu Mramba na timu yote ya Wizara kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha umeme na mambo yote ya mafuta ambayo yapo chini ya Wizara yao yanakwenda vizuri kabisa na nchi yetu inaimarika; kwa kweli hongereni hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na *speed* inavyokwenda sasa hivi ya umeme vijijini kwenye Jimbo letu la Handeni Vijijini mpaka ikifika mwezi Desemba vijiji vyote 91 vitakuwa vimeshapata umeme. Kwa kweli tunashukuru, tunashukuru sana kwa sababu heka heka na *speed* ya mkandarasi inaenda vizuri kwa hiyo tuna imani ikifika mwezi Desemba hali ya vijiji vyetu kupata umeme itakuwa imefika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe ombi kwenye vitongoji. Jimbo letu la Handeni Vijijini lina vitongoji 770, kwa hiyo naomba tuangalie kwa jicho la huruma kwa sababu vitongoji ni vingi sana na shida ya umeme vitongojini ni kubwa na tayari vitongoji vile vina idadi kubwa ya watu kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nipende kumshukuru sana Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mara ya pili kwa kuridhia kutoa fedha ambazo zinaleta mwarobaini ambao

ulikuwa unasababishwa na tatizo la kukatika umeme zaidi ya mara 20 kwa siku kwenye Jimbo langu la Handeni Vijijini. Sasa ameridhia kutoa fedha bilioni 77.5 kwa ajili ya kujenga *sub station* kubwa ya *MVA 120* pale Mkata, na *line* ya *double circuit* itatoka Mkata kuelekea upande wa Kwa Msisi, Mkalamo mpaka Pangani kwenye migodi ya *graphite* na chuma, na *line* nyingine itatoka pale Mkata itaelekea Kabuku Mzundu mpaka kwa Bojo kwenye migodi ya *dolomite, calcite* pamoja na chuma. *Line* nyingine itakwenda upande wa Manga – Madebe – Sua mpaka Kang'ata kwenye migodi ya dhahabu. Kwa kweli umeme huo utatukomboa sana hata kiuchumi kwenye eneo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kama haitoshi Mama huyu vile vile ameridhia kutoa fedha kwa ajili ya *line* nyingine kubwa itakayotokea pale Mkata kuelekea Handeni Mji mpaka kwa ndugu zetu wa kule Kilindi. Kwa kweli tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niipongeze Wizara kwa kuzama zaidi kwenye vyanzo vya nishati jadidifu. Hivi karibuni tumeshuhudia wakisaini umeme wa umemejua. Na mimi napenda kusisitiza hapo kwenye nishati jadidifu kwa sababu kwanza ni nishati salama lakini vile vile itatuongezea nguvu kwenye Gridi yetu ya Taifa. Kwenye *masterplan* inatakiwa ikifika mwaka 2030 *masterplan* ya umeme tunatakiwa tuwe na *megawatt* zisizopungua 10,000. Sasa nilikuwa nashauri tuzame zaidi kwenye Umeme wa Jotoardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Umeme wa Jotoardhi Tanzania tuna viashiria 50 vya umeme wa joto ardhi ambavyo tukivitumia vizuri tutaweza kupata *megawatt* zisizopungua 5,000 ambazo zitakuwa ni mchango mkubwa sana kwenye Gridi yetu ya Taifa. Lakini kwa kuanzia kuna maeneo matano ambayo tayari yamekaa vizuri, na ninaishukuru Wizara imeweza kununua *ridge* kwa ajili ya kuchimba ili tupate mvuke ule wa kuendesha zile *turbines.*

Mheshimiwa Spika, katika hayo maeneo matano ambayo yanatarajiwa kutota *megawatt* 200 naomba Wizara ipeleke fedha kuhakikisha jambo hili linatokea. Lakini vile vile niombe Serikali kwa ujumla kukamilisha Sheria ya Umeme wa Jotoardhi kwa sababu bila sheria hatutakwenda vizuri kwenye eneo hilo;

kwa sababu kwenye jotoardhi inatakiwa kuwe na sheria madhubuti itakayowawezesha hata wawekezaji kuweza kuvutiwa kuja kuwekeza kwenye umeme wa jotoardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ndugu zangu hii joto ardhi huwa pamoja na kuzalisha umeme lakini lina vitu vingi unaweza kuvuna ndani yake. Kwa mfano mvuke ule ukishatumika kutengeneza umeme utaweza kutusaidia kukausha mazao, kukausha mbegu zetu, kwa yale maeneo yanayolimwa mbegu za kuzalisha mbegu. Pia itatusaidia kukausha vitu kama samaki, lakini vile vile inazalisha vitu kama *hydrogen na sulphur* ambazo zitatumika hospitalini, vile vile tunaweza tukapata *Carbon dioxide* ambayo huwa inatumika kwenye vinywaji baridi bia na soda. Kwa hiyo jotoardhi hili lina faida kubwa sana, kwa hiyo nilikuwa naomba tuwekee mkazo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nashukuru sana naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo ajiandae.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze na mimi kukupongeza kwa makusudi kuamua kugombea nafasi ya Uspika. Tuna imani kubwa na wewe, tuna amini kwamba utakwenda kushinda. Kwa namna ya Rais wetu alivyoitangaza Tanzania na namna anavyoonesha ujasiri na uwezo mkubwa wa mwanamke wa Tanzania tunaamini hii itakuwa kwako ni kampeni tosha ya kukufanya urudi na ushindi. Mwenyezi Mungu atakujalia utashinda. Ila ufahamu, ushindi wako ni fahari ya Wabunge Wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo nichukue fursa hii kumpongeza Waziri na Naibu wake Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuleta mabadiliko kwenye Wizara ya Nishati.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe.

**TAARIFA**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba wanawake ni fahari ya wanaume na ushindi wako utakuwa ni fahari ya Watanzania wote na wanaume kwa ujumla. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Tauhida unapokea taarifa hiyo?

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, niseme kwamba nimeipokea taarifa. Nianze kwa hapo kaka yangu tuacheni wanawake kidogo tujidai wa Tanzania, msiwe na wivu kwenye hilo. Huu ni wakati wetu wa kujidai, kujivuna na kuringa. Tupeni fursa kidogo na sisi turinge wanawake wa Tanzania. Tunaheshimu na tunatambua msaada mkubwa mnaotupa mpaka tukafika hapa tulipofika. Wanaume wa Tanzania mmetuunga mkono na mmetu-*support* vya kutosha. Ila kuna muda tuacheni na mkituona tunasema jueni tu kwamba ni wakati wetu wa kuringa acheni turinge kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maringo hayo ya wanawake wa Tanzania na wewe utaenda kuionesha wanawake wa Tanzania wana ringaje miaka hii, tunaamini utaenda kushinda. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa anayoifanya na Naibu Waziri. Mheshimiwa Waziri una Naibu Waziri mzuri, msikivu na mfanyakazi hodari. Mwenyezi Mungu kakujalia umepangiwa Naibu Waziri hana machachari ambaye anafanya kazi vizuri kama unavyofanya wewe mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri tumepanga kwa makusudi Wabunge wa Zanzibar kila atakayesimama tukupongeze kwa punguzo lililoenda kushusha umeme wa Zanzibar. Mwaka jana kila Mbunge wa Zanzibar aliyesimama alikuwa analalamikia bei ya umeme iliyokwenda Zanzibar.

Binadamu ukitendewa mema basi ukumbuke na kushukuru. Kama hukuweza kushukuru kwa binadamu mwenzio unayemuona ni ngumu kumshukuru Mja wako aliyekuumba ambaye humuoni. Tunakushukuru na tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kukujalia kuweza kukupa nguvu na uwezo na hekima na akili ya kuweza kufanya kazi kwa kiwango cha juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wamepunguza umeme Zanzibar na bei imepungua. Tumuombe, bado dhana na dhamira ya Wabunge wa Zanzibar tulilozungumza hapa na kupiga kelele aliloenda kulitimiza, kuondosha bei ya umeme kupunguza lakini bado kwa wananchi haijashuka vizuri. Tunaomba; ninaelewa vizuri kwamba hii si Wizara ya Muungano; lakini ninapata shida kutenganisha maji na mafuta. Unapoizungumza Tanzania tayari umezungumza Zanzibar na Bara. Mheshimiwa Waziri tukuombe kwa unyenyekevu mkubwa tulete maombi yetu kwako haya ni maombi. Sisi tukiwa kama Wabunge wa Zanzibar tukuombe tunaomba hebu kaa kitako na Waziri wa Zanzibar uone maeneo gani yana shida kiasi kwamba huku umeme umeshuka halafu kule bado bei ya wananchi iko pale pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la madeni ambalo linatukabili ambalo hilo deni ni kubwa linahitaji kulipwa ili tuweze kuendesha nchi yetu vizuri. Hatulikatai Mheshimiwa Waziri, tunaodaiwa, tutalipa, tunakuahidi wananchi wa Zanzibar tutalipa. Lakini tunaomba mtumie akili na uwezo aliyokupeni Mwenyezi Mungu kuona deni tunalipaje, mkae na Waziri msaidiane kuona deni tunalipaje lakini vile vile kuona mwananchi wa Zanzibar anapata umeme sawa na Mtanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umeme ndiyo kila kitu kwa sasa. Ili Mwananchi wa Zanzibar aweze kunufaika lazima naye nishati ya umeme kwake imwendee bei ikiwa nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wetu wa Zanzibar ni msikivu, Rais wetu wa Zanzibar anasaidia wananchi wa Zanzibar. Tunaomba ona Waziri ukizungumza nae wa Zanzibar mtataka lipi kwenye lipi? muone mnaongea na viongozi wetu kuweza kufanya sasa.

Dhamira njema uliyoifanya Serikali yetu ya Muungano ilioifanya kushusha bei ya umeme imfikie mwananchi wa chini wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, mimi nikisimama hapa namuongelea mwanamke wa Tanzania ninamzungumza mwanamke wa Tanzania ndiyo anayenifanya nije hapa Bungeni, kwa hiyo kila nitakaposimama sina ajenda zaidi ya kumzungumza mwanamke wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Waziri. Wakati picha za mwanzo naanza kuziangalia alianza kupeleka majiko ya gesi vijijini, aliwapelekea wanyonge vijijini. Alifanya jambo hili na anastahili kupongezwa. Hakuanza mikoa ambayo ni ya mjini, alikwenda vijijini, aliienda kwa dhana ya kusema kwamba mwanamke wa Tanzania kubeba kuni kichwani iwe basi. Mheshimiwa Waziri atembee kwenye dhamira ya aliyemteua, dhamira ya Mheshimiwa Rais wetu kumuona mwanamke wa Tanzania anaishi Tanzania akiwa hana matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda huu tuliyokuwa nao tunataka tutumie vizuri fursa hii tushikeni. Endeleeni kutushika mkono fanya vizuri kaka, fanya vizuri, mwanamke wa Tanzania mfikirie. Anakwenda shambani tena anakwenda na mume wake wanalima lakini muda wa kurudi mwanamke amejitishwa kuni kichwani, mtoto mgongoni, baba anafanya kazi moja ya kuburula baiskeli. Akifika nyumbani akiutua mzigo wa kuni anapanga jiko kupika ugali watoto wale na baba ale. Sasa, mwanamke huyu wa Tanzania atapumzika lini? atajisikia lini? Tumwombe Mheshimiwa Waziri, kwamba katika hili aongeze jitihada za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la umeme tunajua kuna msemo unasema kawia ufike. Kwenda mwenyewe kwa taratibu na mipango yake atafika vizuri. Na kuna muda nimshauri Mheshimiwa Waziri, kuna mambo mazuri anayoyafanya, kaka yangu amezungumza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tuko Dodoma Wabunge tunakwenda kuona bwawa la kufua umeme, niambie Mheshimiwa Waziri kama

haya yangekuwa wazi, kila kitu kikawa wazi wananchi wa Tanzania wangekuwa wanafahamu nini kinaendelea? itumie Wizara yako kwa wale ambao wana nafasi, mara kwa mara fanyeni vipindi lawama na manung'uniko ya watanzania yatapungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna maendeleo watu wanalala siku moja ndani ya nchi wakaamka maendeleo yakawa yamekuja, maendeleo ni safari ndefu. Kuna muda mwingine unaweza kutoa mfano hata wa familia yako, angalia muda mlioutumia kupiga hatua, kutoka kwenye ujenzi mpaka mnapomaliza mnakwenda hatua kwa hatua. Maendeleo haya yataleta maneno na maneno yake Mheshimiwa Waziri na Naibu wake yasiwarudisheni nyuma, maneno hata kwenye kanga yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwetu Zanzibar kuna mtu ambaye anatengeneza kanga, ukipeleka maneno hayo ukafikisha maneno mia moja unapewa zawadi ya kanga. Kwa hiyo maneno hayafanyi mtu asifanye jambo lake, maneno ndiyo yamekufanya wewe kufanya ukue zaidi na ufanye kazi zaidi. Kiongozi *level* uliyofikia wewe si wa kusikiliza maneno, sikiliza Watanzania wanyonge wanataka nini? Hakuna mnyonge anayepiga kelele, hakuna mnyonge anaesema maneno ya hovyo, kila siku mnyonge kazi yake anamuomba Mungu, kusema Mungu tupatie, tuletee, tupe, hiyo ndiyo kazi ya mnyonge. Aliyeshiba na aliyepata mafanikio ndiyo mwenye kelele na mwenye maneno. Kwa hiyo nimpe moyo Mheshimiwa Waziri kaka yangu aendelee kufanya kazi, atimize kiu, ndoto na malengo ya Mheshimiwa Rais wetu. Kama atalifanya hilo atatutendea haki wanawake wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano mmoja; atoka siku moja na gari, apite, akifika maeneo ya Chalinze kwa Mheshimiwa Ridhiwani mpaka unapandisha Kibaha aangalie ndugu zake wanaobeba boda boda na mkaa, amuangalie yule boda boda anavyoumia na mkaa, hafanyi vile kwa kutaka. Anafanya kwa kutafuta riziki yake, tunataka tunapotoka na magari yetu tuwakute wamebeba mitungi ya gesi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa haya, ahsante sana.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN. GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea kuna wageni ambao wameingia baada ya tangazo tulilokuwa tumekwisha kutangaza asubuhi.

Wapo wageni 60 wa Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro na Mzumbe kutoka Mkoa wa Morogoro wakiongozwa na Mhadhiri wao Ndugu Hamad Msamaha Masoud, karibu sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wapo wageni waliyotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, tunao wanafunzi 100 na walimu 10 kutoa Shule ya Mont ya Jijini Dar es salaam, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 64 wa Shule ya Msingi Kilimani kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao pia walimu na wanafunzi 136 kutoka Shule ya *Akili Stars Pre and Primary School* ya Mkoani Mbeya, karibuni sana, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo na Mheshimiwa Jonas William Mbunda ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa furasa na mimi leo kuchangia hotuba hii ya Wizara ya Nishati. Kwanza kabisa nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na mimi siku ya leo kuweza kuchangia bajeti hii ya nishati.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya na hasa kutuwakilisha kwenda kushuhudia uapisho wa Rais wa Nchi ya Nigeria, vivyo hivyo kuendelea kutuwakilisha sana Watanzania katika mambo mbalimbali kimataifa. Nichukue fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara, kaka yangu January Makamba. Kazi kubwa unaendelea kuifanya katika nchi hii kama alivyosema dada yangu Tauhida hapo. Sisi wananchi na hasa wananchi wa Jimbo la Msalala tunakuelewa. Tunakuelewa kwa ukarimu wako, tunakuelewa kwa uchapaji kazi wako; na wananchi wameniagiza kwa wema uliyowatendea baada ya wewe kufika katika Jimbo la Msalala kutuona, kututembelea na kutusikiliza maeneo mbalimbali yakiwemo maeneo ya wachimbaji wadogo wadogo kwenye maeneo yetu ya Msalala. Nimpongeze sana kwa kazi kubwa unayoendelea kuifanya lakini pia nimpongeze Naibu wako Waziri kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya, nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO,* Mkurugenzi Mkuu wa *REA* kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii mimi nimesimama hapa kuwawakilisha wananchi wa Msalala kuhusiana na kero mbali mbali zinazohusu suala la umeme. Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Cherehani amezungumza asubuhi hapa kupongeza jitihada mbalimbali ambazo zinaendelea kwenye Wilaya yetu ya Kahama na hasa Mradi wa *REA* ambao unaendelea kutekelezwa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikili ni kweli hapo mwanzoni palikuwa pamesuasua sana lakini sasahivi mkandarasi anaenda sawa sina haja ya kurudia kwa sababu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu Cherehani amelizungumza jambo hili. Hata hivyo, niongezee hapo tu kidogo katika kumuhakikishia kwamba huyu mkandarasi anaenda ku-*perform* vizuri Mheshimiwa Waziri sisi wananchi wa Kahama, tunaomba huyu mkandarasi aweze kuongezewa zile kilomita mbili ili awe anamaliza kabisa ili kumuondolea usumbufu baadaye kuwa anarudi kuja kutekeleza zile kilomita mbili ambazo zimebaki. Kwa hiyo nikuombe sana muongezee mkataba. Sambamba na hilo kwa sababu ya vifaa niombe Mheshimiwa Waziri nendeni mkajaribu kuona utaratibu wa kumfungulia *LC* ili

aweze kupata *material* kwa wakati, aweze kutimiza miradi hii kwa wakati ili wananchi wa Jimbo la Msalala na Wilaya ya Kahama waweze kunufaika na miradi hii ya umme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi amelizungumza Mbunge mwenzangu na mimi naomba nikazie. Wilaya ya Kahama ndiyo Wilaya ambayo inaongoza kwa kukusanya mapato yatokanayo na umeme kwenye Mkoa wa Shinyanga. Utaona makusanyo kwenye Mkoa wa Shinyanga ni takribani bilioni 16, lakini kiasi cha shilingi bilioni 13 zinatoka kwenye Wilaya ya Kahama. Ukitazama hapo utaona Wilaya ya Shinyanga Mjini ni bilioni mbili na Wilaya ya Kishapu ni kama bilioni moja na kitu. Kwa hiyo Wilaya ya Kahama ni eneo muhimu sana katika uwekezaji wa sekta ya umeme. Kwa hiyo nikuombe sana weka jicho lako katika kuwekeza kwenye Wilaya ya Kahama ikiwemo kuanzisha Mkoa wa ki-*TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia Mkoa wa Dar es salaam wameanzisha mikoa minne ya ki-*TANESCO,* sasa tunashindwa nini kuanzisha Mkoa wa ki-*TANESCO* katika Wilaya ya Kahama ili tuweze kuhakikisha ya kwamba tunasogeza huduma hii kwa haraka kwa wananchi wetu lakini pia tuone namna ya kuweza kusaidia watu ambao wanatoka kwenye maeneo mbalimbali kwenye maeneo yetu? Kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri hili jambo la kuanzisha kwenye bajeti hii twende tukaanzishe Mkoa wa ki-*TANESCO.* (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na nimwambie Mheshimiwa Waziri, Meneja wa *TANESCO* Wilaya ya Kahama anafanya kazi kubwa sana. Wilaya ya Kahama ina halmashauri tatu, na ule ni sawa sawa na mkoa. Lakini pia kutokana na shughuli nyingi na maeneo mengi inanuwia vigumu meneja huyu kufika kwenye maeneo yale. Kwa hiyo niombe, baada ya kuanzishwa Mkoa wa ki-*TANESCO* katika maeneo yale, mkianzisha na ofisi kubwa za wilaya katika halmashauri zetu inatusadia sana kuhakikisha kwamba wananchi wanapata ile huduma kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, wafanye mazungumzo na hawa watu wa

*TRA*. Wananchi wanalalamika kwamba kumekuwa na tabia sasa hivi, hasa ile kodi ya majengo ambayo inakatwa kwenye umeme. Kumekuwa na ulimbikizaji wa kodi ile haikatwi kwa wakati matokeo yake wananchi wetu ambao wana uchumi duni wa kununua umeme unakuta mtu anaenda kununua wa shilingi 10,000 wakati huo huo anadaiwa shilingi 6,000 au 10,000 hiyo, inakatwa na anapata *unit* ndogo. Kwa hiyo niombe mfanye *coordination* ya ninyi pamoja na *TRA* waweze kukata kodi ile mapema iwezekanavyo ili kuondoa mzigo mkubwa kwa wananchi wetu hawa kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimempongeza sana Mheshimiwa Waziri, nisisahau kumpongeza meneja wangu wa mkoa anafanya kazi kubwa sana Mkoa wa Shinyanga, nisisahau kumpongeza meneja wa kanda anafanya kazi kubwa sana. Bila ya hawa maendeleo huko kwetu, hasa katika sekta ya nishati yatashuka. Pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, siku zote huwa anazungumzia habari ya umeme, kwamba unapozungumzia umeme ni mambo matatu; uzalishaji, sina shaka na uzalishaji kwa sababu mambo mengi yanafanyika, anazindua miradi mingi, na juzi tumemuona Mheshimiwa Rais akiizindua Mradi wa Rusumo kazi kubwa inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafilishaji sina shaka na usafilishaji, usambazaji sina shaka na usambazaji. Nataka nimuongezee hapo Mheshimiwa Waziri, aende akaanzishe suala jingine la ukusanyaji, *TANESCO* waweke mikakati mizuri ya kukusanya mapato kwenye maeneo yetu ili kuiwezesha *TANESCO* kuweza kusimama na kutengeneza faidi lakini pia kulipa madeni mbalimbali kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba *EWURA* wametenga fedha kwa ajili ya kukopesha vijana wetu, kuanzisha vituo vya mafuta kwenye maeneo ambayo yana umbali mrefu kwenye vituo hivi vikubwa vya mafuta. Niombe kwenye maeneo hayo Mheshimiwa Waziri watafute namna ya kutoa semina nzuri kwa vijana wetu. Kuona ni namna gani wanaweza kupata taarifa sahihi ya namna gani wanaweza kupata mikopo hii ili na wao waweze kutumia fursa hii

ya mikopo ya kuanzisha vituo vidogo vidogo vya mafuta kwenye maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo kwa Mheshimiwa Waziri sasa naomba nizungumze suala moja zuri sana. Sitaki kuzungumza leo habari ya mafuta, na nimeona kwenye bajeti yake Mheshimiwa Waziri hapa amezungumzia habari nzuri ya mafuta. Mimi nataka leo nizungumze habari ya *lubricant,* kwa maana ya vilainishi.

Mheshimiwa Spika, biashara ya vilainishi kwenye nchi hii ni biashara kubwa sana. Kama Wizara hawataweka jicho katika kuhakikisha kwamba wanadhibiti uingizwaji wa *lubricants,* kwa maana ya vilainishi *fake* kwenye nchi hii itaendelea kutia hasara kubwa sana wananchi wetu katika maeneo haya. Mimi ni shuhuda nimeweza kuweka *oil* kwenye gari langu imeharibu *engine.*

Mheshimiwa Spika, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri, wananchi wengi wanaharibikiwa *engine* zao ni kwa sababu ya uingizwaji wa *oil* ambazo ni *fake* kwenye hii. Sasa niombe kwenye Wizara hii na *EWURA,* kupitia *TBS* waweke udhibiti mzuri ili kuhakikisha kwamba *oil* zinazoingia nchini ziwe ni *oil* ambazo zimethibitishwa na *TBS* kwa ajili ya kumlinda mtu anayekwenda kutumia. Tunaingia hasara kubwa sana ya gari zetu, tunaingia hasara kubwa sana kununua vilaishi hivi *fake*.

Mheshimiwa Spika, na hasa utaona kuna viwanda vingi bubu ambavyo vimeanzishwa kwenye maeneo hayo, wananunua *oil* ambazo ni chafu ni kwenye maeneo yale, wanazisafisha *oil* zile, wanaofanya *package* kwenye maeneo yale na matokeo yake tunaenda kuuziwa *oil* ya *Total* kumbe ni *oil* ya *Total* ambayo ni *fake*. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri waanzishe utaratibu wa kuwasajili wauza *oil* na vilainishi kwenye nchi hii ili kuwalinda wawekezaji wetu kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nizungumze suala zima la namna ya kulinda biashara hii katika nchi hii. Katika makubaliano ya Mheshimiwa Waziri na nchi za *East Africa,* hasa Kenya, katika

ushindani wa biashara hii utaona hapa Tanzania na Kenya kumekuwa na *competition* kubwa. Uanzishwaji wa viwanda vya vilainishi kwenye nchi imekuwa changamoto yake ni kubwa. kwa sababu ya kodi ambayo tunaweka kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, utaona wamekubaliana kwamba *import duty* ya *lubricant* katika nchi hii na katika *East Africa* iwe ni 10 *percent,* lakini ukienda Kenya utaona kabisa Kenya wameweka 16 *percent VAT* lakini huku sisi tumeweka 18 *percent VAT* na kodi mbalimbali zingine. Kwa kufanya hivyo wamefanya viwanda vingi viende vikaanzishwe Kenya na wamefanya sasa iwe kwamba kununua *oil* Kenya ni rahisi kuliko kununua *oil* hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri, yeye pamoja na Waziri wa Fedha wakae chini waone namna ya kupunguza na kuondoa kodi hizi mbalimbali ambazo zitaweka usawa wa nchi za *East Africa* ili kuwawezesha wawekezaji kwenye maeneo haya kuja kuwekeza viwanda vikubwa vya kutengeneza *oil* hapa nchini, *oil* iliyo na ubora, *oil* ambayo yenye kiwango kilichothibitishwa na *TBS* ili kuondoa hili wimbi la kuingiza *oil* chafu kwenye maeneo ya nchi yetu hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa Mheshimiwa Waziri nataka nizungumze habari ya vijana wetu ambao wanasoma masuala ya umeme kwenye vyuo vyetu. Tunao vijana wengi wamesomea umeme, wamehitimu kwenye vyuo vyetu, lakini hii kwa mkakati alionao Mheshimiwa Waziri wa kupeleka umeme kwenye vijiji na vitongojini tunategemea mafundi ambao wanaenda kufanya *installation* kwenye nyumba za watu wetu kwenye maeneo yale leo hii hawajathibitishwa, hawajapata ithibati, hawajawa *registered* kwenye *CRB.* Matokeo yake ni kwamba mtu anakwenda kufunga umeme kwenye nyumba, anatumia kiasi cha shilingi 50,000 mpaka 100,000 kwenda kumuona mkandarasi tu amgongee muhuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sasa nimuombe, ili kutengeneza ajira ya vijana wetu hawa ambao wamemaliza chuo kwenye maeneo hayo muweke utaratibu mzuri wa kuwasajili hao vijana ambao

wamemaliza chuo waliyosomea mambo ya umeme, waweze kuwa na uwezo wa kwenda kuhakikisha ya kwamba wanathibisha na kugonga mihuri fomu zile kuondoa usumbufu na kutengeneza ajira kwenye maeneo hayo. Kwa hiyo niombe sana, gharama, kama alivyosema hapa Mbunge mwenzangu Kenneth Nollo, muangalie na mtuambie ukweli gharama ya shilingi 27,000 inalipa? na kama hailipi mje na mkakati wa kuona namna gani mnaboresha. Kwa sababu utaona wametangaza shilingi 27,000…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa kengle imeishagonga, malizia sentensi. *(Makofi)*

**MHE. IDDI. KASSIM IDDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Wao wametangaza shilingi 27,000, lakini ukiangalia mtu unakwenda kuvuta umeme fundi anachaji 100,000 kwa ajili ya kugongewa muhuri, lakini pia kufanya *installation* kwenye nyumba ni zaidi ya 100,000 mpaka 200,000. Kwa hiyo gharama inarudi kule kule. Kwa hiyo niombe waliangalie suala hili haraka iwezekanavyo na watueleze ukweli wa jambo hili ili tuweze kuwaelewesha wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia 100. Nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa unayo endelea kuifanya, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Jonas William Mbunda na Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao ajiandae.

Mheshimiwa Jonas William Mbunda, atafuatiwa na Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao na Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi ajiandae.

Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Palamagamba, ahaa Mheshimiwa Sebastian yupo samahani.

Mheshimiwa Hamis Tabasam Mwagao atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastiana Simon Kapufi na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Aidani Kabudi ajiandae.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie kwenye bajeti ya nishati. Pamoja na kukushukuru lakini tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu katika safari hiyo uendako Mwenyezi Mungu akujalie upate ushindi na ushindi ulio mnono. Watanzania wote sasa hivi dua zetu zielekee kwa Mheshimiwa Tulia, *inshallah* na Mwenyezi Mungu atakujalia katika hilo. Wanaokwenda Kanisani, wanaokwenda Msikitini kwa sababu hili jambo litaleta heshima katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naanza kuchangia, na ninaanza na hao wenzetu wa *REA*. Ni kwamba kazi ya *REA* ni kubwa sana katika nchi hii. Wamefanya miradi mingi mizuri sana katika hii miradi ambayo imefanyika. Mimi ni mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, tumepita nafasi ya kuangalia miradi, kwa kweli imefanyika kwa ustadi mkubwa, na Wizara tunaishukuru sana, wamekuja na jambo la kupeleka ma-*engineer* kila Wilaya ambao wanakwenda kusimamia miradi ya *REA* na kutoa taarifa Serikalini na kwa sisi Waheshimiwa Wabunge. Tunaipongeza Wizara kwa ubunifu huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini katika jambo hili nikwamba mwanzo ni mgumu sana, sasa katika mwanzo huu tunataka Wizara waje watueleze hapa katika majumuisho yao.

Mheshimiwa Waziri ni kwamba hawa mainjinia walioko kule wamejiegesha katika ofisi za *TANESCO*. Maeneo mengi ofisi za *TANESCO* ni za kupanga ambavyo wana vyumba vyao na watumishi wao. Sasa hawa Mameneja ambao mliowapeleka wa *REA* wanakuwa wameelea. Hadhi ya kumuita injinia ambaye ni Meneja wa *REA* katika eneo hilo inakosekana.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili ni kwamba hawana usafiri hata kwa kuanzia pamoja na bajeti zetu ndogo hizi pikipiki *boxer* ni 2,700,000, na kama zitatolewa ushuru hizi pikipiki zinaweza

zikawa msaada mkubwa sana katika kutembelea na kuona miradi ya *REA* inayoendelea, na ninyi kama Wizara mtapata taarifa mnazozitaka kwa haraka, kwa sababu tayari waratibu mnao katika makao makuu yote ya wilaya nchini. Lakini la pili ni wakandarasi wanaofanya kazi. Ni kwamba mnao wakandarasi wengi, wako wakandarasi wazuri wanaofanya kazi tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, Lakini kuna mkandarasi Mheshimiwa Waziri, ungenisikiliza, kwa sababu huyu mkandarsai anafanya kazi katika Mkoa wa Tanga na Wilaya jirani ya Korogwe na Lushoto. Huyu mkandarasi tumekwenda kule Kwenda kuangalia kazi yake, ni kwamba amepewa fedha kwa ajili ya kufanya kazi Korogwe, Mkinga pamoja na Pangani.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa sisi wanasiasa ni kwamba hili tunaloliona, huyu mkandarasi pamoja na kwamba alifanya kazi nzuri huko nyuma za miradi mikubwa na akapata hii kazi na akachukua *advance* zaidi ya bilioni tatu na kitu, sasa tunaomba aanze kukatwa penati kuanzia muda alioacha kukamilisha mradi ule. Na kwa sababu kesi za kuishitaki nchi zinakuwa nyingi nendeni naye kwa utaratibu mzuri, kaeni vizuri sana kisheria, apigwe *penalty* yule, na hizo penati ni takriban milioni 33 kwa siku. Tangu sisi tumetoka kule nafikiri sasa hivi huyu anakaribia kufikia asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, m-*terminate contract* yake, lakini isiwe sababu ya kuilaumu *REA* kwa sababu *REA* imesimamia miradi mingi kwenye kandarasi zaidi ya 60, mkandarasi mmoja si sababu hiyo. Kwa hiyo tunaomba watu wa *REA* wawe makini katika kuangalia wakandarasi tena wa aina hii, na huyu mkandarasi, kwa sababu tayari anapofanya kazi ni kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati na huyo Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati, Mheshimiwa Kitandula, anapita kusimamia miradi yetu kila kitu.

Mheshimiwa Spika, leo hata kwa kwenyewe Mwenyekiti nako kumepata mkandarasi wa hovyo, sasa inakuwa ni tatizo kubwa. Tukija humu ndani ya Bunge lazima tuwe wakweli, tuseme, Mwenyekiti hawezi kusema lakini sisi tunaoyasimamia haya

mambo tunayaona, sasa lazima tuseme. Kwa hiyo sisi tunawapongeza sana *REA* kwa kazi nzuri wanayoifanya, wapo wanaoweza kuangalia huyu mkandarasi mmoja kati ya wakandarasi 60, mtu kama huyu anataka kaharibu sifa. Lakini tunaipongeza sana *REA* kwa kazi na miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika hili tunaomba sasa *REA* umeme huu unaopelekwa vijijini, kuna watu masikini. Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumza hapa, huu umeme wa jua mnaouona huu shilingi 27,000 shilingi labda 50,000 akifanya na *installation* ndani takriban inafika shilingi 100,000. Kule mngeenda Guangzhou Mheshimiwa Waziri, maonesho ni tarehe tano mwezi wan ne takriban mpaka mwezi wa sita. Kaangalieni, kule kuna taa za sola nzuri, kuna watu hawahitaji huu umeme wa kuchoma *welding* wanataka umeme wa taa, friji na *Tv*. Tumieni umeme wa jua kwenda kuwapelekea hawa watu.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali inatoa ruzuku kwenye kuunganishia mtu umeme, toeni sasa hiyo ruzuku ifanye kazi kwenye taa za sola na wakipelekewa watu masikini huko vijijini watashukuru na kuliombea Taifa hili hakuna mfano wake, na wao waonje ladha ya keki ya nchi hii, kwa sababu huu umeme wa jua hauhitaji gharama kubwa za kiasi hicho. Juzi tumeenda kuweka saini wewe mwenyewe Mheshimiwa ulikuwa shahidi, umeme wa upepo. Umeangalia gharama kuna *megawatts* 50 gharama zake zile ni tofauti. Japo gharama za kwanza zitakuwa ngumu lakini badaye tunaanza kunufaika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala ambalo Mheshimiwa Iddi hapa amelizungumza, suala la hawa vijana wetu. Vijana wanamaliza katika vyuo na wamesomea umeme. Sasa hawa vijana wakiwa wanakosa kazi na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwenye Ilani tunataka ajira milioni 10 tutazipata wapi ilhali kuna ajira manzifunga? Hawa vijana tayari wangepata leseni hawa wenzetu wa *EWURA* usajili *CRB. CRB* wanasajili wakandarasi wa ujenzi *class seven* mpaka *class one,* sasa hawa *EWURA* wangesajili hawa vijana wangepewa *class,* kama ni *class seven* waanzie huko.

Mheshimiwa Spika, hawa vijana wakafanye kazi ya *installation,* mmewafundisha umeme, watashindwa kutengeneza umeme vijijini wa taa tatu au taa nne? Kwa hiyo kila kazi itafanyika kwa *class* yake. Hawa vijana mngewapa na gharama zikawa ndogo za kulipa. Kama mnakwenda kujenga vituo vya mafuta vijijini mnashindwaje kuwapa leseni hawa vijana wakaenda wakafanya kazi? Wapo ma-*engineers* wengine wamemaliza vyuo, hawa ma-*engineers* waliomaliza vyuo nao wanatakiwa kusaidiwa. Wangefanya kazi hizi ambazo zinakuwa ni nyepesi na mnapunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, muhuri shilingi 50,000, fundi shilingi 100,000 bado *installation* ya umeme. Mtu akinunua *installation* ya umeme anunue mita, *socket breaker*, tayari inafika kama shilingi laki tatu na zaidi, hizi gharama zinakuwa kubwa kwa hiyo ziangalieni hizi gharama. Huyo mtu akimaliza kufanya kazi haitaji muhuri, yeye mwenyewe awe ni muhuri, anagonga muhuri wake. Na kwa sababu ana leseni anapeleka *TANESCO* wanakwenda kutoa. Mheshimiwa Waziri hili haliwezi kukushinda. Nafikiri hili na tulilishauri mpaka kwenye kamati. Kwenye majumuisho, uje ulisemee kwa sababu litakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TBS*. Hawa wenzetu wa *TBS* ni wachanga wamepewa kazi ya kuweka kinasaba katika magari. Ushauri wetu sisi tunachosema ni kwamba waongeze jitihada na juhudi katika kazi; tunajua ni wachanga. Aliyekuwepo pale *TFI* alifanya kazi kwa miaka 11 ndipo akawa *giant,* sasa hili ni shirika la Serikali lipunguzieni milolongo. *TBS* apewe fedha ili anunuee magari, aweke katika kanda, asaidiane na *EWURA* hii kazi ili tupunguze *dumping* ya mafuta nchini.

Mheshimiwa Spika, lakini *automation machine* tulielekeza sisi kwenye tenda zake sasa anazokuja kufanya sasa hivi *TBS* aje kwa *automation machine* ili yale magari yaweze kuwekewa kule. Lakini kuna kelele na minung'uniko midogo midogo, *TBS* amalize, aweke *session* mbili. Asubuhi wawepo wafanyakazi watakaofanya kazi saa mbili mpaka saa kumi na wawepo watakaofanya saa kumi mpaka saa nne usiku, ili magari yasilale depo yanapakiwa mafuta. Kila gari iliyopakiwa depo iwekewe

mafuta, ikishawekewa kinasaba ifungwe *seal*. Lazima *TBS* naye afunge *seal* yake ili kusudi hiyo gari ifungwe *seal* ya *deport* na itafungwa *seal* ya *TBS*. Tumpe uwezo *TBS* aweze kufanya kazi. Taifa hili liweze kuokoka na mafuta ya *dumping* nchini.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; ninaomba dakika moja tu. Ni kwamba katika Jimbo langu umeme unakatika, Mheshimiwa January mwenyewe alikuja ukaona, na akatueleza kabisa kwamba anatengeneza *line* nyingine kutoka Mpovu Geita kuja Sengerema. Wananchi wa Sengerema wamenituma katika jambo hili na umeme visiwani, niletewe umeme visiwani.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana…

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** … hongera sana Mheshimiwa January Makamba baada ya kutoka hapa basi uniambie sasa lini Sengerema tunapata umeme? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Sebastian Simon Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Prof. Palamagamba Kabudi. Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Na mimi, kama ilivyo ada, kuna usemi unaosema kwamba sauti ya wengi ni sauti ya Mungu. Nafahamu wengi wameongea kwa maana ya suala lililoko mbele yako lakini naamini kwa kuwa ni wengi wanalizungumza hilo tunarejea kwamba sauti yao ni sauti ya Mungu na mimi naikunja mikono yangu ikiamini Mwenyezi Mungu atatenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo nimshukuru ndugu yangu Mheshimiwa Januari, kwa maana ya Waziri, Naibu Waziri lakini na

watendaji wote kwa kazi ambazo wanaendelea kufanya. Shukrani nyingine za ziada nizielekeze kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa kazi kubwa inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, ulitutahadharisha tusitaje nchi moja moja kwa maana ya kuepuka migogoro ya kiitifaki na mambo mengine ya namna hiyo lakini mimi nikuombe…

**SPIKA:** Ngoja niiweke sawa. Ukiwa unataja kama mfano wa jambo zuri linalofanyika huko, ambalo sisi tunapaswa kujifunza ama kuiga ni sawa. Lakini kama wana changamoto yao hiyo ndiyo inayokuwa changamoto kwenye kuitaja nchi hapa ndani. Ahsante sana.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi nitaliweka kwenye sura kwamba haya yote mazuri tunayofanya ndani ya nchi basi changamoto zinazoifika nchi nyingine kwetu iwe ni somo. Nilikuwa naomba niliweke kwenye sura hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa maana ya utekelezaji wa vipaumbele vya mwaka 2022 na 2023 ni upelekaji wa mradi mkubwa wa kuimarisha grid ya Taifa kwa Mikoa ya Katavi, Kigoma na Kagera. Lakini hilo Mheshimiwa Waziri amelirudia tena, kwa maana pia ndio vipaumbele vya 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Katavi kwa ujumla wake kuna wimbi kubwa la kuongezeka kwa miradi; na sisi pale Mpanda uzalishaji ambao tumekuwa tukiendelea nao ni uzalishaji kupitia majenereta haya ambayo yanatumia mafuta. Niishukuru Serikali kwa hilo, na najua tulikuwa na jenereta nne, kwa msaada wa Mheshimiwa Makamu wa Rais tukaongezewa jenereta moja, na *watts* ambazo tumekuwa tukipata kwa kipindi chote ilikuwa ni megawati 6.25 kwa majenereta matano. Lakini kwa maana ya ongezeko kubwa la miradi nilikuwa namuomba Mheshimiwa Waziri, kuna mambo mawili, nikiamini kwa maana ya suala zima la grid ya Taifa njia ya msongo wa *kv* 132 kutoka Tabora Kwenda Katavi mpaka sasa hivi kwa mujibu wa taarifa za Mheshimiwa Waziri iko asilimia 26.7.

Mheshimiwa Spika, rai au ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri. Kasi ya maendeleo ya wananchi ni kubwa na yeyote akija Mpanda akija Katavi atakubaliana na mimi katika eneo hilo. Tumuombe Mheshimiwa Waziri, wakati tukisubiri huu umeme wa msongo mkubwa atusaidie, lengo ni kupeleka mbele maendeleo ya watu wetu. Nimuombe sana katika hilo. Waliweza kutusaiida jenereta, najua ni kipindi cha mpito kwa usikivu wake ndugu yangu Mheshimiwa Makamba tuliangalie hilo; wametusaidia hapo katikati. Na wakati wengine wakilalamika najua kuna suala la kukatika kwa umeme lakini mimi nishukuru walau kwa jitihada hizo zilizofanyika, maana unaposema ahsante hata ukiomba unafikiriwa kwa hiyo naomba mnifikirie katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, nikitoka hapo. Nimezungumzia habari ya mashine hizo na ongezeko la wawekezaji, na nimesema suluhu kwa kipindi hiki ni hiyo *grid* ya Taifa. Kuna mradi wa *REA;* mimi nimebakiwa na vijiji vitano. Vijiji hivyo ambavyo kwa mujibu wa taarifa wanasema mpaka ikifika mwezi Juni kwenda Agosti 2023 umeme utakuwa umewashwa katika maeneo hayo, vijiji hivyo ni vya Kamakuka, Mkokwa, Nguvu Mali, Nseso na Mkwajuni. Nimuombe Mheshimiwa, maeneo yote hayo ambayo nimeyazungumza kilimo kinafanyika, uzalishaji ni mkubwa na kuna viwanda vidogo vidogo vya ukoboaji wa mazao. Kwa hiyo tukiwapelekea umeme tunakwenda kuwasaidia na nikiamini upatikanaji huo wa umeme utasukuma mbele jitihada hizo za wananchi.

Mheshimiwa Spika, lakini nikitoka hapo, nimshukuru Mheshimiwa Waziri; tuna mradi mwingine tuna takribani milioni 260 ambazo tunakwenda kupeleka umeme kwa ajili ya kusukuma *pump* kwa ajili ya Vijiji vya *Society* na Kakese, lakini pia kwa maana ya Zahanati ya Mwamkulu na Kakese, tumepewa takribani milioni 260, nishukuru sana kwa suala hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo yote nishukuru pia kwa ajili ya mradi wa ujazilizaji mzunguko wa pili *(b),* tunaambiwa vitongoji 1,686 na Katavi ikiwemo vitanufaika. Kwa hiyo mimi nishukuru kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya shukrani hizo maelezo yangu ya jumla natamani niione *TANESCO,* au shirika kwa ujumla wake ambalo kwa kiwango kikubwa Serikali imekuwa ikililea shirika hili, ikilipa nguvu shirika hili basi tufike sehemu tuone huyu mtu ambaye amaelelewa kwa kiwango kikubwa amefika sehemu anaweza kusimama.

Mheshimiwa Spika, nalisema hilo kwa sababu gani, kati ya maeneo ambapo huwezi ukalalamika uwepo wa wateja ni pamoja na eneo hili la *TANESCO,* wateja wapo tu ni wa kufikia. Labda nilichokuwa naomba au kushauri, tubadilishe mtazamo tuachane na ile biashara ya mazoea. Kama wateja ndio wanaolalamika tunaomba huduma, tunaomba huduma maana yake suala la soko siyo tatizo. Kwa hiyo tukiachana na biashara ya mazoea, *TANESCO* kwa jitihada wanazofanya, na wakabadilika; kuna taasisi nyingine mnaona kila kukicha inafanya mabadiliko; kawaangalie *TANROADS* na *TARURA* wanafanya mabadiliko kila kukicha. Na mimi natamani *TANESCO* waachane na biashara ya mazoea tunagalie sura hiyo kwamba ni soko la uhakika lakini kwa nini watu walalamike kila siku? Maana yake kuna kitu wanatakiwa wabadilike, na wakibadilika, mimi naamini haya yote ambayo yanazungumzwa, ukiangalia kwa maana ya nchi hii yenye fursa kibao, kwa maana ya kutekeleza miradi ya nishati jadilifu ikiwemo joto ardhi, tungamotaka, upepo na jua pamoja na matumizi bora ya nishati yanawezekana. Na nchi yetu njema, fursa zote zipo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naongea na jirani yangu hapa Mheshimiwa kuna sehemu moja kama unaenda Moshi, unaambiwa jihadhari upepo mkali, hiyo ni fursa. Kama tunaambiwa tunapita kwa magari kwamba jihadhari upepo mkali, hiyo ni fursa, na maeneo mengine yote ni fursa. Lakini moja kubwa haya yote hata kama tutatumia vyanzo vyote hivi kuviingiza kwenye *grid* ya Taifa, tusiache, kama nilivyozungumza pale mwanzo, kuchukua tahadhari. Sitamani siku moja tukaona migawo hii ikiendelea eti kwa sababu kuna jambo moja hatukufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa unyenyekevu mkubwa naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa John Danielson Pallangyo, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati ambayo ndiyo hasa inatupeleka kwenye maendeleo nchi hii. Pamoja na shukrani hizo nichukue nafasi hii pia kuungana na wenzangu kukuombea uso wa Mungu upatane nawe katika hiyo safari ambayo unaiendea. Tunaamini kabisa kwamba unaweza. Kwa namna ambavyo unaendesha hili Bunge kwa umahiri mkubwa, huko unakokwenda ni shaihi kabisa. Tunakuombea Mungu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anatufanyia kazi Watanzania. Pamoja na fedha nyingi sana ambazo ameweza kupeleka majimboni mabilioni kwa mabilioni, lakini pia ameendelea kutekeleza miradi mkakati mikubwa na mfano mzuri kabisa ni hili Bwawa la Nyerere ambalo linakuja kutuongezea umeme mwingi sana kwenye *grid* ya Taifa, megawati 2,115. Kazi inayofanyika ni nzuri na sasa hivi kazi imefikia asilimia 86.89; kwa kweli tunamshukuru na kumpongeza.

Mheshimiwa Spika, lakini kipekee nimpongeze Waziri Januari Makamba na Naibu wake Stephen Byabato lakini pia Katibu Mkuu *Eng.* Mramba na Naibu wake Bwana Butuka na watendaji wote pale Wizarani, kazi ni nzuri inaonekana. Waliobahatika kufika kwenye mabanda ya maonesho ya wiki ya nishati, wanaweza kukubaliana na mimi kwamba Wizara inafanya kazi nzuri na mmejipanga vizuri. Kwa hiyo ninachoweza kusema ni kwamba muendelee vivyo hivyo; ari hiyo hiyo, nguvu hiyohiyo, msirudi nyuma kwa sababu hii kazi ya kusambaza nishati kwa Watanzania ndiyo maendeleo yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na sifa na pongezi hizo kwa Wizara nizungumzie kidogo kuhusu *REA*. *T*unashukuru kwamba *REA* wanafanya kazi vizuri lakini kuna mapungufu. Waheshimiwa Wabunge wamesema, kwamba bado vijiji vingi havijapata

umeme, vitongoji ndivyo vingi zaidi; lakini pia hat akule kwangu kule Arumeru Mashariki hali sio shwari sana. Kuna kata, vijiji na vitongoji ambavyo bado havijapata umeme. Hivi ni kama vile Kata za Uwiro, Marurango, King'ori na Majengo, kuna vijiji na vitongoji ambavyo havijapata umeme wa *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na niseme kwamba, tatizo kubwa sana ni kwamba, hawa wakandarasi ambao wanapewa hii kazi wanapokuja majimboni wanakwenda moja kwa moja *site* bila kuwasiliana na mamlaka. Wanapaswa wakifika waripoti kwa *DC,* waripoti Halmashauri, lakini pia na Ofisi ya Mbunge kwa sababu Mbunge ndiye anayefuatilia hizi fedha. wanapokuja halafu wanakwenda moja kwa moja *site* kunakuwa kuna maswali mengi kwamba, kazi inaendeleaje, lakini kama wakipitia kwenye hizi ofisi nilizosema tukakaa chini wakatueleza mpango kazi inakuwa ni rahisi kuwafuatilia na kujua kwamba, kazi inaendeleaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kule Korogwe ambalo limezungumzwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Nishati ni mfano halisi, kwamba kuna mapungufu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, niseme kwamba bei ya kuunganisha umeme bado haiko *clear.* Nadhani ni wakati umefika Serikali iwe wazi iseme sasa kwamba, utaratibu uko hivi, shilingi 27,000/= zitatumika maeneo fulani na kulipia nguzo itakuwa maeneo fulani, ili tuache kuuliza maswali ambayo tunakutana nayo kwa wananchi na hatimaye na sisi tuwe na amani.

Mheshimiwa Spika, nilisema kwamba, kazi ni nzuri inayofanyika na Wabunge wote wamepongeza. Na niseme kwamba, Mheshimiwa Waziri endeleeni kufanya kazi vizuri, msimamie hapohapo, Watanzania wanawaona na wanawaelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo machache nakushukuru sana kwa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, tutamalizia na Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika hoja hii. Kwanza kabisa naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu ili niweze kuchangia hoja hii. Na mimi naomba niungane na wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Januari, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hiyo. Naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuweza kusimamia na kuweza kuiwezesha Wizara kuweza kufikia mahali walikofikia katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kuishukuru Serikali kwa ajili ya Mkoa wa Kigoma. Kwa muda mrefu Kigoma tulikuwa hatuko kwenye *grid* ya Taifa, lakini tangu mwaka jana umeme wa *grid* ya Taifa uliwashwa katika Wilaya nne na Wilaya tatu zilikuwa zimesalia, lakini niipongeze Serikali kwa Mradi wa Rusumo – Nyakanazi, kilovoti 400 zilizopatikana na ninaamini Wilaya zilizosalia kwa maana ya Kigoma Vijijini, Kigoma Mjini na Uvinza zitaweza kupatiwa umeme. Hivyo, ninaishukuru Serikali na ninaipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika miradi ya *REA* wapo wakandarasi ambao wamefanya vizuri na wengine ambao hawajaweza kufanya vizuri. Na kwa sababu kwa mwaka huu Serikali iliahidi kwamba wananchi wote watakuwa wamepata umeme katika vijiji vyote, lakini bado umeme haujawafikia wananchi. Ninaomba Serikali iwasimamie wakandarasi wote wale ambao hawajaweza kukamilisha miradi hiyo ili waweze kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na hatimaye vijiji vyote viweze kupatiwa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Kigoma katika mradi wa umeme awamu ya kwanza hatukuwa tumepata umeme wa *REA*. Katika awamu ya pili hatukuwa tumepata umeme wa *REA,* lakini tumekuja kupata umeme wa *REA* katika awamu ya tatu. Tunamuomba Mheshimiwa Waziri asimamie wakandarasi hao ili umeme uweze kufika katika vijiji vingi lakini pia katika vitongoji. Kwa sababu ukiangalia maeneo mengi vijiji vichache ndivyo vimepata umeme na penyewe kwenye *center,* lakini vitongoji havijaweza kufikiwa na umeme. Tunaomba kwa sababu tumeshatoa ahadi kwa wananchi, wananchi wote wafikishiwe umeme hadi kwenye vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini zipo shule zetu za msingi na shule za sekondari nazo bado hazijapata umeme, vilevile na taasisi. Tunaomba Serikali ihakikishe umeme unawafikia wananchi, uwafikie wenye taasisi ili waweze kunufaika na umeme wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana wapo wakandarasi ambao wengine wamefanya vizuri na wengine hawajafanya vizuri. Nirudie kusema kwamba Serikali iangalie wale ambao ni wababaishaji iwachukulie hatua na ikibidi wasiongezewe mikataba mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze.

**MHE. NASHON D. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Spika, naomba na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nishati, ndugu yetu Mheshimiwa Januari Makamba. Kwanza naomba nichukue nafasi hii kwa kusema kwamba, mimi naunga mkono hoja kwa sababu eneo hili ni eneo kubwa nani nyeti. Na kama mwenyewe Mheshimiwa Januari anavyoendelea kulizungumzia, ni kwamba kwa kweli, bila umeme nchi itasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nizunguimzie kwenye eneo moja, lile la vinasaba ambavyo kimsingi tulikwishakubaliana kwamba *TBS* ndio ambao wataendelea kuweka vinasaba kwenye mafuta. Mimi naomba kwenye eneo hili niendelee kusisitiza kwa sababu *TBS* pia ni Shirika la Serikali. Mheshimiwa Waziri aendelee kusimamia jambo hili kwenye eneo la *TBS, TBS* waendelee kuweka vinasaba kwenye mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwanza naomba nimpongeze Meneja wa *TANESCO* Wilaya ya Uvinza, anafanya kazi vizuri sana tena katika mazingira magumu. Kuna kipindi alikuwa hana hata gari la kubadilisha *transformer* kuweka nyingine; kwa sababu mradi huu wa *REA* ulianza na *transformer* ambazo ni ndogo kidogo ambazo zilikuwa ni 100, lakini yeye anaendelea kubadilisha kwa gharama za *TANESCO,* anapoomba fedha anapewa kufanya miradi na anabadilisha sasa kutoka 100 kwenda 150 mpaka 200. Kwa hiyo ni jambo la kumpongangeza sana kwa sababu, sasahivi wananchi wanaendelea kutumia umeme na wakati kwingine wanatumia kwa ajili ya mashine za kusaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine, katika jimbo langu kuna vijiji 61, vijiji 29 vilishapata umeme, vijiji 32 bado. Hata hivyo naomba nimshukuru Mheshimiwa Januari Makamba, sasahivi tunavyozungumza kuna vijiji sita vinaendelea kuwekewa umeme, ni jambo la kupongeza sana, na kwa hili naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Makamba. Lakini pia kuna njia ya umeme ambayo ni kilometa 104.6 ambao unatoka Kirando kwenda Karirani, ni umbali mrefu. Na umbali huo ndio ambao vijiji hivyo viliwekewa umeme wa jua, na siku zote wamekuwa wakilalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa unaweza kuona kabisa kwamba, hiyo *line* ambayo imeanza kujengwa ikikamilika itakuwa na uwezo wa kusaidia kuweka umeme vijiji 13. Kwa hiyo vijiji vyangu ambavyo ambavyo havina umeme vitazidi kupungua. Naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Makamba kwa kazi hiyo nzuri ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia naomba niseme; jana Mheshimiwa Makamba amezungumzia kwenye bajeti yake kwamba mwaka ujao wa fedha kwa eneo lile la Malagarasi, umeme ule wa *Kv* 49, kama sijakosea 49, utakwenda kuanza kujengwa. Na taarifa nilizonazo ni kwamba mkandarasi alikwishapelekwa *site*. Mkandarasi wa kujenga alishapelekwa *site,* lakini pia mkandarasi wa kujenga njia ya kupeleka umeme kule wilayani ameshapatikana.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, naomba nipongeze kwamba, umeme ule ambao unatoka Tabora ambao unakuja pale Nguruka kwenye eneo la pale Mganza ambapo *sub station* imeshajengwa, bado ku-*install,* naomba nikushukuru. Hata mkandarasi wa kuja kuifanya hiyo *sub station* ikamilike amekwishaletwa pale, na mimi taarifa ninazo na mimi nilimuona, hilo ni jambo jema sana. Pia mkandarasi wa kuleta njia ya umeme kutoka Tabora kuja hapo amekwishaletwa pale *site,* lakini wa kutoka hapo tena kupeleka kwenye eneo ambalo limeandaliwa ameshapatikana. Kitu ambacho naomba nimuombe Mheshimiwa ni kwenye hawa watu wanaoathirika na hiyo njia, kwenye kuwathamini. Naomba kusiwe na mgogoro kwenye eneo hilo, hawa wananchi wamekuwa na ridhaa na wameacha maeneo yao. Sasa ninaomba sana hao nao waweze kuthaminiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jingine ambalo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, ni kwenye eneo la Kijiji cha Nguruka na Kijiji cha Uvinza. Naomba sana, hili jambo nimekuwa nikimwambia siku zote kwamba hawa watu walipangiwa shilingi 320,000 lakini uwezo huo hawana, mimi ndiye ninayewajua. Nashukuru Mheshimiwa Waziri alituma tume, ilikwenda, na nadhani taarifa anayo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu atamke neno, Nguruka warudi kulipa shilingi 27,000 lakini pia, Uvinza warudi kulipa 27,000. Na kubwa sana hivi leo wako kwenye runinga wanaendelea kusikiliza jinsi ambavyo Mbunge wao anamwomba Mheshimiwa Waziri, na wangetamani aseme, ili waweze kusikia, naomba sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba niunge mkono hoja kwamba, hii bajeti iko vizuri na mimi nitakuwa tayari kuipitisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa sehemu ya kwanza ya kikao chetu cha leo.

Kwanza ni Wabunge ambao watachangia mchana; tunaye Mheshimiwa Maimuna Salim Mtanda, Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Rehema Juma Migila, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, na tutaendelea kwa namna hiyo.

Jambo la pili ni tangazo la wageni ambao wameingia baada ya tangazo lile la mwanzo kuwa limepita na lingine likjiwa limeshapita.

Tunao wageni 100 wa Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, ambaye ni Waziri wa Katiba na Sheria. Hawa ni wanafunzi wa Shule Kuu ya Sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wanafunzi 125 kutoka Chama cha Skauti Wilaya ya Ubungo na Shule ya Msingi ya Derbab. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Sasa hapa naona, ama wote wanatoka shule moja? Hebu hawa wanafunzi 125 kutoka Chama cha Skauti Wilaya ya Ubungo? Karibuni sana. Ama wote mnatoka shule moja? *(Makofi)*

Haya, naambiwa mmechanganyika shule na skauti. Basi simameni wote pamoja. Shule ya Msingi Derbab ambayo ipo Wilaya ya Ubungo. Karibuni sana Bungeni; mnaweza kuketi sasa *(Makofi)*

Haya, asanteni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, jambo la mwisho, nililetewa ujumbe hapa kama nilivyokuwa nimesema kuhusu akidi. Na kwa mujibu wa kanuni zetu ukiulizwa akidi inabidi kengele igongwe ili Wabunge waingine ndani ndipo hesabu ifanyike. Na kengele huwa ni muhimu kugongwa kwa sababu wako Waheshimiwa Wabunge wanakutana na wapiga kura hapo nje, wengine wanaonana na viongozi mbalimbali kwa ajili ya shughuli zao za majimboni, kwa hiyo inagongwa kengele ili wajue na warejee hapa ndani.

Baada ya kufanya hesabu, Kamati tatu, Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ina kikao kwa sababu kuna maazimio yanakuja hapa Bungeni, Kamati yetu ya Bajeti iko kwenye kikao pia kwa sababu ndicho kipindi chake hiki, na Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo pia iko kwenye kikao kwa ajili ya yale matrekta ya Ursus. Lakini hata hivyo baada ya kufanya hesabu baada ya kupiga ile kengele akidi tulikuwanayo, Waheshimiwa Wabunge 197 walikuwa Bungeni.

Kwa hiyo, kwa idadi ya Wabunge wa jumla ni 393 kwa hiyo, ukiwa na 197 ni akidi inayotosheleza kuendelea na kikao chetu kwa mujibu wa Katiba yetu na kanuni zetu za Bunge. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge, Nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11:00 alasiri, leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano; Mheshimiwa Maimuna Salum Mtanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, Mheshimiwa Rehema Juma Migilla ajiandae.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia afya. Kipekee nimshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya. Na katika Wizara hii amefanya mengi sana makubwa ambayo mengine yanaendelea kukamilika na mengine yanaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kipekee kukutakia heri sana wewe binafsi kwa ule mchakato ambao uko mbele yako, na *Insha Allah* Mwenyezi Mungu ataleta heri, kwa sababu Waswahili wanasema iliyonona inaanzia miguuni; huku Tanzania umenona, hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri mwenye dhamana aliyewasilisha hotuba yake pamoja na viongozi wake wote wanaomsaidia kazi; hongereni sana, hotuba ni nzuri.

Mheshimiwa Spika, nina mchango katika maeneo machache. Mchango wangu wa kwanza unakwenda kwenye suala la kukatika katika kwa umeme katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Niishauri Wizara kutafuta namna nzuri ambayo tatizo hili la kukatika katika kwa umeme litakwenda kukomeshwa kwa sababu linaathiri kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, katika hilo, hata kwenye Mkoa wa Mtwara suala la kukatika katika kwa umeme limekuwa sasa kama ni la kawaida. Lakini kipekee niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri, amekuwa msikivu, juzi tulikaa naye kikao yeye pamoja na wataalamu wake wote kwa saa zaidi ya mbili kwenye jando – maana lile tunaliita jando, na mambo ya jandoni hayasemwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, yale ambayo tumejadiliana yanayowenda kutekelezwa kwenye Mkoa wa Mtwara ili ku-*rescue* hali ya kukatika katika kwa umeme basi mkayasimamie. Na nishukuru kwamba zoezi lile nimesikia wameshaanza na kuna wengine wameniambia wanaondoka kesho wanakwenda kukaa huko wiki nzima. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri kilichobakia ni usimamizi wa yale ambayo tumekubaliana ili suala la kukatika katika kwa umeme na kuunguza vifaa vya watu liende likapotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa ninapoongea ukienda Mkoa wa Mtwara sasa kumedorora kwa sababu wafanyabiashara wengi vifaa vyao vimeharibika kutokana na tatizo hilo la kukatika katika kwa umeme, uwekezaji hakuna na watu wana hofu hiyo. Kwa hiyo yale ambayo mnakwenda kuyatenda, ikiwemo pia na kupeleka *grid* ya Taifa kwenye Mkoa wa Mtwara ikitokea Tunduru – Masasi kwenda Mahumbika, ni jambo ambalo litakwenda kuleta urahisi wa upatikanaji wa umeme katika Mkoa wa Mtwara ili sasa uwekezaji na uchangamfu wa mkoa, kwa maana ya kiuchumi, uende ukatekelezwe. Kwa hiyo nawatakia kila la heri katika usimamizi wa hilo ili Taifa liendelee na wananchi wapate uchumi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea ni suala la *REA*. Niwaombe Wizara, wenzetu wa afya wana *model*, ukienda kwenye hospitali zao kubwa wametenga, wale wagonjwa mahututi wana namna yao ya kuwatibu na wagonjwa wengine wa kawaida wana namna ya kuwatibu. Sisi Mtwara kwa suala la *REA* tuko mahututi. Kwa hiyo niombee *treatment* ya Mtwara kwenye suala la *REA* ichukuliwe kama

*special case,* ikasimamiwe. Tukiwasimamia wakandarasi hali ya upatikanaji wa umeme nadhani itakwenda kuwa nzuri.

Mheshimiwa Spika, nitolee mfano tu wa Jimbo la Newala Vijijini. Kwenye huu Mradi wa *REA III Round Two,* kulikuwa na vijiji 76. Kati ya vijiji 107 vya Newala Vijijini, vijiji 76 ndivyo vimlivyoingia kwenye mkataba na mkandarasi ambaye yuko *site*. Na mkataba ule ulikuwa ni wa *August*, 2021. Mpaka sasa *status* ilivyo vijiji 17 tu ndivyo ambavyo vimepata umeme, vijiji 17 viko kwenye *process*, vijiji 42 bado hawajafikiwa; na *deadline* ya mradi huu ni *December* mwaka huu. Sasa naona kama mzigo uliobakia ni mkubwa sana. Tusipowasimamia hawa watu watatuangusha, vijiji vile hawatapata umeme, tutapinduka 2024 bila ya kuwa na umeme. Niombe sana Wizara ikawasimamie.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wana suala wanasema wanaomba *LC* kutoka Serikalini, wapeni *LC* isije ikawa ndiyo kisingizio chao. Wapeni na wasimamieni kwa sababu nilicho-*study* kwa muda mrefu wa mkandarasi wetu ni kwamba anakosa usimamizi ule wa karibu. Kwenye mchezo wa mpira tunasema *man to man* – twende tukafanye *man to man* kwenye huu Mradi wa *REA* kule Newala Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, athari ya kutokuwa na umeme ni kubwa sana. ukienda leo tunazo shule za sekondari kwenye Jimbo la Newala Vijijini, lakini wanajifunzaje TEHAMA kama hawana umeme? Kwa hiyo wale watoto watamaliza bila ya kuwa na *knowledge* ya TEHAMA kwa sababu tu ya ukosefu wa umeme, lakini huku tumeshawapatayari miradi wakandarasi. Kwa hiyo ili tuokoe kizazi hiki cha watoto ambacho ni cha kidijitali, lazima umeme ukafike shuleni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, Wizara ya Elimu imetenga fedha na imeendelea kuboresha miundombinu ya *VETA* Kitangali. Tumetangaza kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwamba tutaoa ajira zaidi ya 8,000 ifikapo 2025. Ajira hizi zinatoka kwenye sekta iliyo rasmi na isiyo rasmi. Mategemeo yetu ni wale wanaotoka *VETA* wakajiajiri kwenye sekta zisizokuwa rasmi. Watoto wale wanajifunza useremala, uchomeleaji na mapishi

mbalimbali; vyote hivyo vinategemea umeme. Leo hii wanamaliza hawana kwa kwenda ku-*practice* kile ambacho wamejifunza kutoka kwenye chuo cha *VETA*. Maana yake ni kwamba tunawekeza fedha nyingi kuwafundisha watoto hawa lakini tija yake haionekani kwa sababu wanakwenda kwenye maeneo ambayo umeme hakuna, kwa hiyo *application* ya *knowledge* waliyoipata inakuwa haionekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, tunamshukuru Rais sisi Wananewala, Tandahimba na Nanyamba, ametuletea fedha shilingi bilioni 84.7 kwa ajili ya mradii mkubwa wa maji ambao sasa hivi umeanza kutekelezwa. Karibuni, ikifika 2024, Juni huko mradi unakwenda kukamilika; tutasukumaje maji yawafikie wananchi kama hatuna umeme wa uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niiombe sana Wizara, tunashukuru kwa yale ambayo mmekuwa mnayabuni kila siku, lakini tukasimamie suala la ufikaji wa umeme katika vijiji vyetu. Tumeona kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kuna kipengele cha kupeleka kwenye vitongoji 15 kila jimbo kufikisha umeme. Newala Vijijini naogopa, kwa sababu kama vijiji mpaka leo havijafikiwa, hivyo vitongoji vitafikiwa kesho? Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri na timu yako, mna kazi ya kufanya Newala Vijijini. Bahati nzuri tumeshakueleza kwa kina na wewe unatambua pamoja na *management* yako, ni kusimamia sasa tuone utekelezaji wa yale makubaliano, yaende yakatekelezwe kwa vitendo ili uchumi wa wananchi wa Newala Vijijini pamoja na Mtwara kwa ujumla, kupitia sekta ya umeme, ukaweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ninataka kuliongea kidogo; tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa suala lile la *LNG* pale Lindi. Uwepo wa mradi ule mkubwa utachechemua kwa kiasi kikubwa sana uchumi wa watu wa Kusini. Kwa sababu kama mradi utaanza kutekelezwa, akina mama wanaolima mbogamboga watakwenda kuuza, na mambo mengi sana ambayo yanategemea upatikanaji wa nishati ile kwa ajili ya uzalishaji wa uchumi kwa wananchi wa Mtwara na Lindi, kwa kweli yatakwenda kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe tu Wizara, kwamba tusimamie utekelezaji ili miradi hii ikaweze kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa mwananchi mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Kengele ya pili ilishagonga Mheshimiwa Mtanda.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi; naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Edward Kalogeris, atafuatiwa na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ajiandae.

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, na mimi nitumie nafasi hii vilevile kwanza kukupongeza kwa uthubutu kwa jambo ambalo liko ndani ya moyo wako na uhitaji wako. Kubwa zaidi, sisi kama Wabunge wenzako tuko nyuma yako na tunaendelea kukuombea Mungu katika dini mbalimbali Mwenyezi Mungu aweze kukamilisha hiyo azma na Taifa liendelee kung'ara kupitia wewe.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutoa fedha katika maeneo mbalimbali. Sisi Wabunge ni mashuhuda, tangu tumeanza kupitisha bajeti hapa za Wizara mbalimbali, kila Wizara iliyopitishwa kuna mambo makubwa yamefanyika.

Mheshimiwa Spika, na katika hili, hata katika Wizara ya Nishati kuna mambo makubwa; trilioni tatu na pointi si jambo dogo, ni jambo kubwa ambalo linahitaji uthubutu mkubwa, na Mheshimiwa Rais amefanya. Sasa hivi kazi kuwa iko kwa ndugu

yangu tu, Mheshimiwa January, kuhakikisha kwamba fedha hii inayokuja ikafanye yale matokeo ambayo yanatakiwa kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vilevile kukupongeza Mheshimiwa Waziri, Niabu Waziri, *management* ya Wizara na watendaji kupitia taasisi zote; *REA, TANESCO, EWURA* na kwingineko, kwa kazi kubwa ambayo mnaifanya, lakini kwa bajeti ambayo imekuja mbele ya Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vilevile kutoa pongezi kwa Meneja wangu wa *TANESCO* Mkoa wa Morogoo, *Eng*. Fadhili pamoja na Meneja wa *TANESCO* wa Wilaya ya Morogoro, kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, vilevile pongezi hizi ziende kwa Mkandarasi makini *Stagic International Services* ambaye ndiye amefanya kazi kubwa ya kupeleka umeme wa *REA* katika Halmashauri ya Morogoro. Alipewa vijiji 84, tunavyozungumza sasa hivi vijiji vyote 84 vinawaka; tuna kila sababu ya kupongeza katika hili.

Mheshimiwa Spika, kubwa zaidi, nimwombe Mheshimiwa Waziri, bado kuna vijiji vitano ambavyo havikuwepo katika ule mkataba, mkandarasi ameongezewa, tayari ameshakwenda *site*, anachosubiri nadhani ni kuanza kazi. Niombe, katika zile kilometa mbili mbili ambazo tumeongezewa, nikuombe mfanye kwa haraka – mkandarasi huyu yuko *idle* – apewe hiyo kazi afanye ili tumalize, kama vile ilani ilivyosema; mpaka kufikia 2023 tukamilishie vijiji vyote nchini. Kwetu sisi Morogoro tunaamini tutakuwa tumekamilisha; nikupongeze sana.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vilevile kukuomba, katika suala la kwenda kwenye vitongoji. Bado tuna changamoto kubwa, vitongoji ni vingi. Tunakushukuru kwa hivyo 15 lakini nikuombe, angalia uwezekano mwingine wa kuhakikisha kwamba umeme unawafikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana hamu kubwa ya umeme, na umeme ni nishati kubwa sana yenye uhitaji mkubwa kwa Tanzania. Nikuombe tu Mheshimiwa Waziri, angalia namna gani – tunakushukuru kwa hivyo 15 kwa sababu tuna kila sababu ya kuanza kushukuru kwa kile tulichopata – lakini tunahitaji vingine utusaidie.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri, Mkoa wa Morogoro ni mkoa wa kimkakati. Kuna uhitaji mkubwa katika *TANESCO* wa magari na watumishi. Naomba wasaidieni watumishi wa *TANESCO* Mkoa wa Morogoro wapate magari mapya ili waweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo vikubwa vitatu vya Kihansi, Kidatu lakini tunakwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere. Lakini mkoa ni mkubwa, wana uhitaji mkubwa wa watumishi pamoja na vitendea kazi. Nikuombe unapokuja ku-*wind up* uone jinsi gani ya kuwasaidia.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii vilevile kumwomba ndugu yangu, Mheshimiwa January, kwenye hili suala la vinasaba, hebu tuliache lilipotulia, tusianze mambo mengine mapya. Ninachojua nyuma kulikuwa na changamoto nyingi, lakini tulipoingia kwenye *TBS* changamoto zilizokuwepo tunahitaji Serikali kuisaidia *TBS*. *TBS* ni kampuni ya Serikali, ina utaalamu mkubwa, inafanya mambo makubwa katika nchi. Kwa hiyo nikuombe libakie hapohapo, hatutaki kwenda kwingine. Kwa sababu tukienda kwingine tunaanza kwenda kufukua makaburi ambayo hayana sababu.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kupongeza jitihada za dhati za Mheshimiwa Rais anazozifanya katika kuendeleza Bwawa la Mwalimu Nyerere. Bwawa hili Mheshimiwa Rais alipolichukua lilikuwa kwenye wastani wa asilimia 30/32. Lakini leo tunapozungumza mpaka kufikia Aprili tumefikia *almost* asilimia 88; tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa hii anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, ombi langu kwa Wizara, na hasa kwako ndugu yangu, Mheshimiwa January; ndani ya mradi ule kuna kitu kinaitwa *CSR* ambayo tangu mradi umeanza mpaka unafikia asilimia hiyo, hakuna fedha yoyote iliyokwenda katika Halmashauri ya Morogoro Vijijini au Halmashauri ya Rufiji. Nikuombe, katika Bunge lililopita ambalo tulikuwa tunapitisha mpango wa bajeti kulikuwa kunasemekana fedha ile inatakiwa ipelekwe Tanga, fedha ile inatakiwa ipelekwe Dodoma, Kigoma na Lindi. Nikuombe, fedha ile ni ya watu wa Morogoro, ni haki ya watu wa Morogoro, tunaitaka watu wa Morogoro, tuna shida nyingi Wanamorogoro ambazo kupitia fedha hii tunaamini tutaweza kuzitatua au kusaidia Serikali kufikia katika yale maendeleo tunayoyataka.

Mheshimiwa Spika, sasa kama suala ni kujenga chuo hicho cha TEHAMA ambacho mnadhani wataalamu mnakihitaji kijengwe Morogoro au kijengwe Pwani kwa sababu tuna maeneo makubwa ya kuweza kufanya jambo hilo. Lakini vilevile Morogoro juzi tuliambiwa kupitia TAMISEMI kwamba tupeleke mahitaji yetu kwenye suala la afya; tumefanya. Na hapo TAMISEMI, tunaomba yaheshimiwe.

Mheshimiwa Spika, lakini bado kuna suala la elimu, kwa sababu katika mradi huu fedha ya *CSR* zinakwenda kwenye elimu, zinakwenda kwenye afya. Morogoro kama Morogoro kiwilaya ina halmashauri mbili, wenzetu mjini wana *VETA,* sisi Halmashauri ya Morogoro Vijijini hatuna *VETA;* tunahitaji *VETA*. Tunahitaji *High School,* tunahitaji mabweni kutokana na jiografia ambayo tunaishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe, Waziri anapokuja ku-*wind up* aje na jambo la kutueleza Wana-Morogoro na Wanapwani. Najua jambo hili Mheshimiwa Mchengerwa hawezi kulisema, yuko kwenye *Cabinet;* je, tufanye nini kupata haki zetu sisi ambazo ni haki ya Kikatiba na ya kimkataba?

Mheshimiwa Spika, mara ya kwanza mlipeleka Dodoma kujenga uwanja, mkabdarasi kakataa kwa sababu anajua *CSR* ile ni ya Morogoro na Pwani. Sasa hivi kama mtapeleka huko maana

yake tunazidi kuchelewesha fedha ile, mnazidi kuchelewesha maendeleo kwa Morogoro na kwa Pwani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe sana, najua wewe ni kijana makini, na bahati nzuri umekulia Morogoro, unaijua Morogoro, unajua shida za Wana-Morogoro, nakuomba simama kuhakikisha kwamba haki ya Wana-Morogoro na Pwani ya *CSR* inabaki katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema maneno mengi, najua Mheshimiwa January ni mchapakazi, anajua kazi. Sasa nakuomba tu utakapokuja, sitaki kushika shilingi yako lakini nataka tu unipe majibu hayo na jioni baadaye mimi ni profesa unajua, nataka tukutane baadaye ili nikupe furaha na wewe ukafurahi baada ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru; naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko, Mheshimiwa Nicodemas Maganga ajiandae.

**MHE. REHEMA J. MIGILLA:** Mheshimiwa Spika, nianze kukushukuru kwa kunipatia nafasi nami ya kuweza kuchangia kwenye Wizara yetu nyeti ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai, lakini pia nimshukuru Rais wetu, mama yetu kipenzi, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwapigiania Watanzania, anakesha kila kukicha kuhakikisha wananchi wake wanaboreshewa miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nipende tena kumshukuru kaka yangu, Mheshimiwa January; mdogo wangu, Mheshimiwa Byabato pale, kazi mnayofanya siyo ya kitoto, tunaona mambo mengi sasa hivi yamekuwa mazuri. Lakini bila kuwasahau viongozi wangu wa mkoa *Eng.* wangu Khadija pale *Engineer* wangu wa Kanda na *Engineer* wangu wa wilaya, kwa kweli wanafanya kazi nzuri.

Wanatupa ushirikiano wa kutosha kiukweli hata tukiwapigia simu wana-*respond* kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya hizi salamu nianze mchango wangu kwa kuanza na *REA*. Ni kweli *REA* wanafanya kazi vizuri sana, sasa hivi hata ukipita huko kwenye maeneo yetu unaona kabisa taa zinawaka waka na mji unabadilika. Kwa kweli tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu na Wilaya yetu ya Kaliua tuna vijiji vipatavyo 100 lakini katika vijiji hivi 100, vijiji 82 tu ndivyo vina umeme lakini vijiji 18 bado. Kati ya hivyo vijiji 18 nina vijiji vyangu mimi kumi ambavyo havijapata umeme kabisa. Nina Kijiji cha Unsungwa, Silambo, Kabanga, Mwamashimba, Tupendane, Imagi, Busubi, Uhindi, Mpagasha na Lusanda. Mheshimiwa Waziri hivi vijiji kiukweli ndivyo vijiji ambavyo vina nibeba mimi kama Rehema na vinawapiga kura wengi sana. Hivyo niombe sasa harakati za kupeleka umeme kule na wakandarasi waharakishe ili wananchi wangu wasione tu umeme unatokea kwenye maeneo mengine. Taa wanaziona maeneo mengine, tunataka nao wawashe taa.

Mheshimiwa Spika, lakini tatizo kubwa la *REA* ni tatizo la uhaba wa nguzo. Hizi nguzo ni chache sana. Unaambiwa kilometa moja moja wanatoa nguzo 22 hazitoshi. Matokeo yake wanatwambia nguzo ni bure. Mheshimiwa Waziri mimi nikuombe tu *brother,* yaani tunaomba mtuambie ukweli hivi hizi nguzo ni bure au vipi. Nikiwa kama mimi ni Mbunge nilishanunua nguzo 350,000. Mimi kama mimi Mbunge nimenunua 350,000, hivi kwa nini sasa msiweke wazi kabisa wananchi wakajua kwamba hizi nguzo badala ya kuwaambia bure mkaweka bei elekezi. Kwamba labda kuanzia mita ngapi kutoka kwenye chanzo labda iwe laki moja au elfu hamsini. Watu wanatamani umeme wanatamani kuweka, mkiweka bei elekezi ya hizi nguzo na mkawa wazi. Mimi ninaimani wenye uhitaji watajichanga na kuweka umeme kwenye nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, lakini leo tunawaambia 27,000, hizi ni ela ndogo sana, wananchi wetu wana uwezo, akiuza kuku wake

wawili tu ameshapata fedha ya kuweka umeme; lakini shida ni nguzo. Mheshimiwa Waziri nikuombe nakujua wewe kijana sana mchapa kazi, hili suala naomba ulichukue, hebu wekeni wazi sasa bei ya nguzo. Mkae mfikirie mfanyie bei tu elekezi ili hawa wananchi wetu wenye uhitaji waweze kujichangachanga waweze kufikisha nguzo kwenye maeneo yao wapate umeme, na si tu kila siku kuona umeme kwenye maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu umeme kukatika katika; suala la umeme kukatikakatika bado lipo kubwa sana. Mbaya zaidi umeme unakatika kwenye maeneo ya wananchi wetu na hawapewi taarifa. Zamani kulikuwa na siku maalum ya kufanya matengenezo ndipo wananchi wanapewa taarifa kwamba umeme utakatika lini; lakini sasa hivi umeme unakatika mno na mgao upo wa kutosha. Kaka yangu kwa hiyo nikuombe, huku kukatika kwa umeme wananchi wetu wanaharibiwa vitu vingi sana, hawapewi taarifa. Tuombe sasa wananchi wawe wanapewa taarifa lakini hata ikitokea kuna tatizo basi wananchi waambiwe na lisichukue muda mrefu hili kushughulikiwa. Nimeona kuna kata yangu ya Uyowe kule vijiji vya Mnange, Kashishi wapi kule takribani mwezi mzima wananchi wangu wamekaa gizani lakini tunashukuru *process* zinaendelea. Tunaomba hizi harakati ziendelee, *maintenance* yafanyike kwa haraka ili wananchi watoke gizani.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu kumtua mama kuni kichwani. Nikupongeze kaka yangu Mheshimiwa Januari, tumeona hizi hatua za mwanzo. Tunaenda kupeleka majiko ya gesi kule vijijini kwetu. Hii ni *approach* nzuri sana. Lakini napenda nishauri jambo kidogo hapa. Mwananchi tunampelekea gesi lakini akishamaliza ile gesi hakuna *filling station* kule. Vijijini kwetu kule hata maduka ya kubadilisha gesi hayapo. Nadhani sasa kuna haja ya Wizara mkae chini mfikirie namna gani ya kuweza kuwaboreshea hao watu wa majiko bainifu lakini na hii mikaa jadidifu.

Mheshimiwa Spika, kuna tafiti mimi nimefanya kidogo, inaonesha kwamba mtu anayekata mkaa anatumia miti tani kumi mpaka kumi na mbili ambapo akichoma mkaa anapata mkaa

wa kawaida tani moja tu. Tunaona namna gani wanavyoharibu mazingira na miti inakwisha. Kwa hiyo nikuombe sasa *either* twende kuanzisha mashamba darasa ya kupanda miti inayokua haraka, kama walivyofanya watu kwenye *BBT*. Tuanzishe mashamba kuna miti inaota haraka sana. Kuna miti inaitwa mianzi, mabingobingo yale ndani ya miezi sita mpaka mwaka unatosha kabisa kutaka kutengeneza mikaa hii bainifu na mikaa ambayo ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ningeweza kupendekeza hapa. Hii gesi ishuke bei badala ya kuwapandishia naamini kabisa mwananchi hata akiuza mayai mangapi ataweza kwenda kunua gesi kuliko tukiacha gesi ilipo halafu tumewapa majiko, itakuwa *useless*; kesho tutakuta wameweka chuma chakavu. Nikuombe kaka yangu tupunguze hii bei ya gesi na hao wananchi wetu waweze kununua.

Mheshimiwa Spika, kwenye hiyo gesi ninafikiria sasa tuanzishe yale majiko ya kama mtu anavyokwenda kutumia luku. Tulifanyiwa semina kule tuliona; yaani mtu atumie gesi kulingana na uwezo wake na si mtu mtungi wa kilo kumi na tano ambao hawezi kununua kwa wakati. Tukiweka kama vile matumizi ya luku mtu ana buku anapika maharagwe na maisha yanaenda. Lakini kuachia mtungi wa 60,000 ishirini na ngapi wananchi wetu hawawezi kutumia hizi.

Mheshimiwa Spika, tumeona Serikali bado haijatenga bajeti. Tumeona asilimia 90 ya Watanzania wanatumia mkaa. Kwa hiyo kama wanatumia mkaa tuweke bajeti kuhakikisha kwamba hao wadau wetu wabunifu wadogo wadogo wanaweza kuingizwa kwenye mpango wa kutengeneza mkaa ambao unatumiwa na watu wengi. Kuna majiko mbadala, tumetoka kununua kule. Kwa hiyo kama tutawawezesha hawa wadau wetu wazawa wa ndani, na kule kwenye mabango yako kule kwenye mabanda tumewaona, hebu tuwatengee bajeti hawa, nina uhakika kabisa ile azma kaka yangu Mheshimiwa Januari uliyonayo ya kuwafanya wakina mama wawe wasafi wakipika yani wasichafue masufuria mazingira yawe safi nafikiri itatimia. Hilo nikuombe kaka yangu panga bajeti vizuri mambo yako yatakuwa safi. Leo sitarajii

kushika shilingi mambo yako yamekaa vizuri. Lakini, kama umeme hautafika kwangu kule nitashika shilingi, lakini leo sijadhamiria kwa sababu mambo yako makubwa nimeyaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunashukuru umenitengenezea *sub-station* pale kutoka Tabora mpaka Ulyankulu, tunatumia peke yetu. Pale mwanzo tulikuwa tunatumia Tabora, Kaliua na Ulambo. Kwa hiyo kaka yangu nikushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Nicodemas Henry Maganga, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava ajiandae.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia fursa hii na mimi kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati ambayo ni muhimu sana kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kukupongeza kwa kweli. Mimi ni mjumbe wa *IPU,* kwa hiyo kwa kipekee kabisa nikupongeze kwa nia lakini kwa dhamira ya dhati ya kuwaza kwenda kugombea Urais wa Mabunge ya Dunia na niwaambie tu Watanzania wenzangu pamoja na Wabunge kwa kweli tukuombee dua. Tukuombee dua kubwa kabisa ili njia iweze kufunguka na uweze kuwa *endorsed* hata kwa asilimia mia; kwa sababu tumeshaona kule *IPU* ulikuja kwa muda mfupi tu tukakuamini na tukakufanya ukawa Rais wa Ukanda wa Afrika, na sasa hivi tunaenda kukupandisha uwe Rais wa Mabunge ya Dunia. Kwa kweli kwa asilimia kubwa kabisa Wabunge wa Mabunge ya Dunia wanakukubali. Kilichobaki ni kutoa rai tu kwa Watanzania wakuombee lakini pia najua kuna Watanzania ambao hawako humu Bungeni lakini wana *connection* na Wabunge wa Mabunge mengine wakipata fursa basi waendelee kutuombea kura. Mwisho wa siku ni *pride* kwa Bunge hili lakini kwa nchi yetu kama Tanzania na kwa Afrika na zaidi kwa wanawake wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia. Kwanza kabisa kipekee ninakwenda ku-*acknowledge,* kwa Mkoa wetu wa Mara vijiji vyote vimefikiwa na umeme kwa asilimia mia moja, kwa hiyo hapa ninatoa *complement* kwa Wizara na kwa *REA*. Lakini bado kwa upande wa vitongoji tuko chini. Vitongoji vimefikiwa kwa asilimia 47 tu, kwa hiyo bado takriban asilimia 53 hawajafikia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najaribu kupitia nikaona takwimu za *NBS* 2019/2020 *of course* walionesha kwamba ufikaji wa umeme ulikuwa ni asilimia 69 lakini uunganishwaji ni asilimia 24 tu. Hili ndilo tatizo ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea hapa. Kweli utatoa takwimu kwamba umeme umefika lakini bado inabidi tuweke mtandao kuhakikisha Watanzania wote wanafikiwa na huu umeme. Sasa tumeona mpango mkakati wa Wizara hapa ameainisha kwamba ili kuweza kukamilisha *REA* ikamilike ndani ya miaka mitano na sio miaka 20 basi atahitaji kupata vyanzo vingine zaidi kuliko ambavyo tunavipata sasa hivi. Mojawapo aka-*suggest* kwamba ikiwezekana sasa na Bunge lako Tukufu likiweza kuona tuweze walau tuongeze ile waweze kupokea kutoka shilingi mia ambayo tunapokea sasa hivi iongezeke iende 150 na hata ingewezekana iende hata 200 ili tuweze kumaliza.

Mheshimiwa Spika, tukiweza kuimarisha na umeme ukapatikana vijijini kwanza tunaongeza kuchechemua uchumi huko vijijini lakini pia usalama utakuwepo, pia na kupandisha hadhi wawekezaji wengi waweze kwenda wa kuweza kuwekeza. Tunashuhudia wote kwamba huko vijijini kwenye vituo vya afya au kwenye taasisi mbalimbali tunatumia vibatali au hivi vi-*sola*r vidogo hata wamama wanataka kujifungua inakuwa ni shida sana. Kwa hiyo kwa kweli mimi ningetoa rai Serikali ione ni jinsi gani, huu mpango mkakati wa kuhakikisha umeme unapatikana kwenye vitongoji uweze kupatikana kwa uharaka Zaidi; hata isiwe hiyo miaka mitano, ikiwezekana iwe miaka mitatu au miwili, ambayo kwa kweli inakwenda kusaidia na maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi dunia, lakini hata kwa Tanzania, tulimwona Mheshimiwa Rais aliweza kuzindua mpango mkakati wa kwenda kwenye nishati safi. Sasa hii nishati safi haiwezi kufikiwa

kwa ukamilifu kama Watanzania hawatafikishiwa kwa huduma ya umeme ambayo itapelekea urahisi wa kuweza kutumia majiko sanifu ambayo yanaweza kuonekana yana nafuu zaidi kuliko majiko banifu na njia zingine za kuweza kupikia kwa nishati safi. Ukiangalia takwimu kwa wanaopata umeme hasa kwa mijini asilimia 40 watu wanaumeme lakini hawatumii nishati ya umeme kupikia. Tumeona kwamba asilimia tano wanatumia gesi, asilimia tatu tu ndio wanatumia umeme lakini asilimia 32 wanatumia hizi nishati ambazo ni chafu, na kati ya hizo asilimia 26 ni mkaa, na mkaa wa Tanzania ambao unavunwa asilimia 75 unakwenda kwa matumizi ya watu wa mjini ambao wana umeme; na asilimia 60 anayosema ni wanatumia kuni.

Mheshimiwa Spika,sasa hapa ina *trigger* kwamba kuna vitu vingine vya ziada tunatakiwa tufanye ili kujua kinachosababisha ilhali tuna umeme na tuna gesi, huku gesi ikiwa inatumika kwa asilimia tano na umeme unatumika kwa asilimia tatu. Hapa inaonekana kuna elimu ya matumizi bado haijatolewa; elimu haijatolewa ya kutosha ili uweze kuainisha kwamba ukitumia kwa mfano jiko sanifu unapunguza gharama kwa kiasi gani.

Mheshimiwa Spika, mimi nashukuru nilipata fursa ya kuweza kuhudhuria, walikuja watu wa *TaTEDO* na *SESCOM* sijui, na wakatupa semina baadhi ya Wabunge hapa, Wabunge wa Bunge lako kupata semina. Ikaonesha mfano kama unapika maharagwe kwa jiko hili la *pressure* ya kutumia umeme, inarahisisha mara tano zaidi kama vile ambavyo ungetumia mkaa. Kwa hiyo kama ungetumia mkaa ungepika labda kwa dakika sitini ukitumia lile jiko unakuta unatumia dakika kumi na mbili kuweza kuivisha hicho kitu. Lakini pia inarahisisha mara nne zaidi kama ambavyo unatumia gesi. Ina-*serve* muda lakini pia ina-*serve* na gharama. Sasa kama Watanzania ambao wana umeme wakielekezwa kwamba tukitumia hili jiko tuta-*serve* muda, tuta-*serve* fedha lakini pia itaturahisishia kuweza kuhakikisha kwamba hata zile *nutrients* kwenye chakula zinakuwa hazipotei kwa wingi wake.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna mambo kadhaa ambayo kama Serikali inahitaji kufanya. Moja ni hiyo ya kutoa elimu.

Tunaweza tukapeleka umeme kwa Watanzania wote lakini bado wakaendelea kukata miti, kuchoma mikaa kwa sababu watu hawajapata elimu ya kutosha. Kama tunataka tufikie hiyo *target* ya 2033 ya kuweza kufikisha asilimia 80 Wizara mnajukumu la kutoa elimu ya kutosha hasa kwa hawa wananchi ambao tayari wana umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini kingine tuhakikishe tunatoa *incentives* zingine. Kwa mfano Uganda bei ya umeme kwa ambao wanatumia majiko imepunguzwa. Umeme umepunguza ile *tariff*. Kwa hiyo ni *incentive* ya kuweza kuwavutia watu waweze kutumia haya majiko. Lakini pili tuweze kuhakikisha kwamba tunatoa kodi. Hizi kodi zitasaidia kuweza kupunguza bei ya kuweza kununua majiko sanifu ili Watanzania wengi waweze kuwa nayo lakini hata taasisi ambazo zinapika kutumia kuni na mkaa waweze kutumia hii, ambayo pia itasaidia kwenye ku-*protect* mazingira yetu. Tukiendelea kuacha wanakata miti tutaendelea kupata mabadiliko ya tabianchi ya hewa ukaa ambayo inazidi kudidimiza, na tutakuwa tunaenda kinyume na *Paris Agreement,* lakini pia tunaendelea kuhakikisha kwamba hata upatikanaji wa mvua tukikata miti sana tunakuwa hata hatuwezi kupata mvua wakulima wataathirika na wafugaji wataathirika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi nilikuwa nashauri, tuhakikishe tunatoa hizo *incentives* (ruzuku), tunatoa kodi ili Watanzania waweze kwenda kutumia haya majiko sanifu. Pia tusi-*rely* sana kwenye umeme wa maji tu. Natambua wametoa mkakati hapa, lakini twende kwenye *Biothermal*, joto ardhi, twende kwa kiwango kikubwa sana kwenye umeme wa jua na kwenye umeme wa upepo. Na tukiwekeza pia huko kwa zaidi huu umeme wa maji unakuwa kama ni *balancing* tu. Umeme wa jua hata gharama yake sio kubwa. Nina *acknowledge* ambavyo tumeshawekeza kwa kiwango kikubwa kwenye maji, tuji-*balance* sasa twende na kwenye hizo *source* zingine ambazo zitatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, ukiaangalia madhara mengine ya kuendelea kutumia hiyo nishati chafu sote tulielezwa, lakini kuna

takwimu ambazo zimetoka ambazo unaangalia siyo tu vifo kwa kupelekea upumuaji au *TB* lakini kunakuwa kuna *carcer*, kuna ku-*premature*, mimba zinatoka lakini pia ulemavu. Kwa hiyo kuna madhara mengi sana ambayo ukifanya *cost and benefit analysis* kama Taifa ni lazima tuwekeze kuhakikisha kwamba Watanzania sasa tunatoka kwenye kutumia kuni na mkaa tunakwenda kutumia kwa kiwango kikubwa majiko sanifu na banifu ili kuhakikisha kwamba tunalinda afya yetu lakini tunaweza kuwa *productive;* kwa sababu ukiwa unaumwa hata huwezi kwenda kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia sasa, kuhusu luku, niko na mwekezaji hapa. Kwenye *plot* ulivyoleta hizo luku tunakata hiyo kuweza kulipia kodi ya ardhi. Tulisema mita moja kama ni *plot* ndiyo itakayotumika kulipia. Lakini unakuta labda sehemu hiyo *plot* moja au kiwanja kina mita takriban 11 sasa kila mita inachajiwa tena elfu kumi na mbili kwa mfano wawe wanachaji elfu moja moja, kila mita 12,000. Hili liangaliwe, huu ni wizi. Ina maana *if you multiply* 12,000 mara 11 yaani mimi *plot* yangu unanilipisha laki moja na kitu ilhali nilitakiwa nilipe 12,000. Kwa hiyo hili mlipitie muweke kama luku mama iwe moja kwenye *plot,* kwamba hii ndiyo iwe inalipa hiyo chaji ili hata kama Salome hapa huyu Mheshimiwa Mbunge anayewekeza kwenye vitu vya *apartment* kama anawapangaji hao wengi mapangaji mmoja atakuwa anam-*refund* hiyo 12,000 hao wengine wasiwe wanachajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, mbona mwekezaji kama hajiamini vile. Haya Mheshimiwa Nicodemas Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Rose Busiga ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hii sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Muumba wa Mbingu na Nchi kwa kupata nafasi hii adhimu ya kuweza kuzungumza na watanzania wote kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mama yetu, Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita kwa kazi anazoendelea kuzifanya hapa nchini ikiwemo kupambana na miradi hii mikubwa iliyoachwa na mtangulizi wake. Kweli shukrani za dhati, wananchi wangu wamenituma nije ni mshukuru. Walifurahia sana walipomwona anazindua Ikulu maana ilikuwa kama vile ndoto, kwamba Ikulu ya Dodoma imekamilika tena kwa kiwango cha juu kushinda hata ile ya zamani. Kwa kweli Mheshimiwa Rais ubarikiwe sana. Pili nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa jinsi unavyotuendesha kwenye Bunge hili Tukufu. Na sisi maombi yetu tu, kwa niaba ya Machifu wa Kisukuma tunakuombea kwa Mwenyezi Mungu ili kusudi uweze kukamilisha dhima yako uliyokusudia. Na kwa niaba ya Watumishi wa Mwenyezi Mungu, kwa maana ya Makanisa yote Wakristo na Waislamu wamenituma kukwambia usome Zaburi 23:1 nakuendelea. Maneno haya yakutie ngunvu katika safari yako ya mapambano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nije kwenye hii sekta ya nishati na nianze na hii miradi ya *REA*. kwanza, nikiri wazi kwamba mimi ni mjumbe wa Kamati, na nikuombe Mheshimiwa Waziri, ushauri tuliokupa kama Kamati uuzingatie na uufanyie kazi sana maana umesomwa vizuri na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Kitandula pamoja na wajumbe ambao huwa tunakuwa wa wewe kwa pamoja, huwa tunakupa ushauri mzuri sana na ukiufuata utakuwa ni Waziri wa kiwango ambae utaacha historia kubwa hapa Tanzania kwenye hiyo sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, hii sekta yako ina changamoto nyingi na inafahamika katika historia ndio sekta ambayo huwa ni ngumu katika Wizara zote hapa nchini. Hata hivyo, nianze kwa kukushurukuru jinsi unavyonipa *support* kwenye Jimbo langu maana toka niingie madarakani nilikuwa nina vijiji 34 na kwa sasa bado vijiji 18 ambavyo bado havijapata umeme; naomba nivitaje. Kuna Kijiji cha Nyashinge, Kagongo, Isungabula

hiki ni Kijiji kimoja kikubwa sana na huwa kinanipa shida sana ninapoenda pale. Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo nikuombe wewe kwa vile mkandarasi yuko chini yako utoe msukumo, pale utakapofanya majumuisho mkandarasi huyu wa Geita afanye *faster* hapo Isungabula ili wawahi kulala peupe. Pia, kuna kijiji cha Bwendaseko, Kiseke, Nyashinge, Mgerere, Igalura, Burongo, Bushetu, Bukwimba, hiki ni kitongoji kikubwa, kimeamua kupewa Kijiji, na ndipo nilipozaliwa hapo. Pia, kuna Baguta, Kabanga, Buruhe, Ruhala, Mwagimagi, Mponda, Nhungwiza pale niliposoma Shule ya Msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, napenda nikwambie akupendaye lazima atakushauri kwenye Bunge kama hili. Mimi nakupenda sana kwa kweli Mheshimiwa Waziri; lakini kama nilivyotangulia kusema mwanzoni, sekta hii ni kubwa, unaongoza watu wenye akili, maprofesa, lakini hivyo wengine nia zao sio nzuri sana. Ninakuombea sana kwa Mwenyezi Mungu akupe ujasiri wa kutokusita kuchukua maamuzi pale unapoona mambo hayaendi vizuri. Nimeiona bajeti hii ina trilioni 3.48, kwa hali ya kawaida unaweza ukasema ni pesa nyingi lakini ni chache. Kwa kuwa mimi ni mjumbe wa Kamati na changamoto za sekta hii nazijua vizuri, bajeti hii ilitakiwa iende hata trilioni tano kwa jinsi mahitaji yalivyo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tukiangalia kwenye upande tu wa mafuta umetenga bajeti ili kusudi kuwasaidia vijana wanaojishughulisha na uuzaji wa mafuta holela mitaani. Kwanza, nipende kuwapa pole sana wenzangu kwa sababu na mimi ni zao ambalo linalotokana na kuuza mafuta huko mitaani. Niwape pole sana watu wangu wa Masumbwe ambapo tarehe 29 nyumba iliwaka kufuatia kuweka mafuta ya *petrol* ndani. Mheshimiwa *DC* wangu alishughulika vizuri sana, pamoja na Jeshi la Poliisi japokuwa hatukuwa hata na kizima moto, mchanga ulitusaidia na Mungu alismama na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwape pole pia wale waliounguliwa na vitanda vyao kwenye Mtaa huu wa Masumbwe Shinyanga B Mungu awasaidie. Kwa sababu hasara hii imetokea, na hata huyu mfanyabiashara yeye hakupanga kwamba nyumba hiyo

iungue. Kwa hiyo, Mungu awasaidie muweze kupata mitaji mingine maisha yaendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimpe pole mfanyabiashara mmoja tarehe 23 aliunguza nyumba yake kwa shoti ya umeme. Mheshimiwa Waziri hii nayo ni changamoto nikuombe wasiliana na Waziri mwenzako wa Mambo ya ndani ikiwezekana kila mnakopeleka umeme huko mtaani kuwepo na vifaa vya kuweza kuzima shoti za umeme pale zinapotokea. Ni kweli huduma hii ni nzuri lakini pale inapotokea shoti inakuwa ni majuto kwamba ni kwanini niliunganishiwa umeme huu. Mimi nimeyaona kwa macho nyumba za watu zinavyotekekea kwa shoti za umeme. Kwa hiyo, Serikali ilifikirie. Na kwa kuwa hapa nazungumza na Serikali yote mpo, mlifikirie hasa pale mnapowaunganishia umeme wananchi wa vijijini mkumbuke je, ikitokea shoti watazima na nini katika nyumba zao?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mji wa Masumbwe ni mkubwa na hatuna gari la zima moto japokuwa hoja hii nilitakiwa niiwasilishe Mambo ya ndani. Hata hivyo, kwa kuwa wewe Mheshimiwa Waziri uko makini unaweza ukaongea na ndugu yetu ili aweze kutusaidia ili nyimba hizi zinapopigwa shoti ya umeme ziweze kuzimwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoke jimboni nishauri jambo lingine la kitaifa. Hapa nchini tuna changamoto ya upandaji wa mafuta, na hili mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri kwa vile una uwezo mkubwa ukae na wataalamu wako uangalie ni jinsi gani mnamsaidia Mheshimiwa Rais. Kwa sababu sio kawaida Watanzania kununua bei za 3000/3000. Kwa sababu tusiseme maisha tumeyaweza sana, kero zilizoko mtaani nikubwa.

Mheshimiwa Spika, tuna bandari yetu, jinsi gani tunakwenda kuwasaidia wanyonge ili kusudi bei za mafuta na nauli zishuke bei; kwa sababu mafuta yakishuka bei ina maana na vitu vyote vitashuka bei, mabati yatashuka bei na kila kitu kitashuka bei. Kwa uwezo wako uliopewa na Mwenyezi Mungu kaa na wataalamu wako muangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano nchi ya Kenya tumesikia sasa hivi wao wanaagiza mafuta kwa fedha zao za Kenya. Kama Kenya inawezekana kwa nini sisi Tanzania ishindikane kuagiza mafuta kwa fedha zetu? Vile vile, uagizaji wa mafuta zile Sheria zilizopo ni ngumu. Tuachieni Machinga tufuate mafuta wenyewe nje ya nchi ili kusudi muone bei zitakavyoporomoka ili Watanzania waweze kuishi maisha wanayoyataka.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana imani kubwa na Chama cha Mapinduzi lakini pale maisha yanapoonekana kuwa magumu halafu tukawa kama vile hatuwajali inaonekana kama tumewasahau. Mkumbuke Sera yetu ni kuwasaidia wanyonge. Sasa wanyonge hawa bei za nauli zinapopanda wanashindwa kuelewa kwamba Serikali hii ilitutangazia kutusaidia ama kutukomoa? Kwa hiyo, nikuombe Kaka yangu January kaa na wataalamu wako pamoja na bodi inayohusika kupanga wale waingizaji wa mafuta Sheria hizo zifutwe na watu tuingize mafuta kwa uwezo wetu ili kusudi tuweze kuilinda nchi yetu na kuweza kuileta manufaa mazuri ili watu waishi kwenye maisha mazuri ya kupendeza.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, Mheshimiwa Waziri nizidi kukushukuru tu, lakini pale Masumbwe zile *transformer* zilishazidiwa. *Transformer* zilizopo Wilaya ya Mbongwe zilikwisha zidiwa, maana kipindi umeme unapita nyumba zilizokuwa zinaunganishawa zilikuwa chache. Hivi sasa kuna viwanda vya mchele kwa hiyo, pale wanapowasha mashine hizi za kukoboa mchele umeme unazima**.** Utufikirie kutuongezea t*ransformer* nyingine kupitia bajeti yako hii ya Trilioni 3.4. kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nikuombe sana na ukipata nafasi utembelee kwenye jimbo langu ili kusudi uje u–*solve* matatizo yangu. Kwa sababu wewe ni rafiki yangu na urafiki mzuri ni ule wa kujaliana wakati wa shida sio kusubiriana tu huku kwenye raha. Kwa hiyo, nakukariobisha sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa vile na yeye ni Mbunge mwenzangu kila mara huwa anapita. Naibu Waziri, nikuombe mji wa Masumbwe usipopita kwenye chocho ni lazima wewe uukanyage ili ufike Bukoba. Siku

moja utenge nafasi uweze kuzungumza na wafanyakazi wa *TANESCO,* hawana magari, hawana vitendea kazi vijana hawa wanasumbuka sana kufanya kazi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana ahsante. Nitaleta mchango wangu wa maandishi kwa yale niliyoacha.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Timotheo Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Rose Busiga, Mheshimiwa Prof. Paramagamba Kabudi ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango kwenye bajeti hii ya Wizara ya Nishati. Nianze kwa kuungana na wenzangu waliotangulia kusema kukutakie kila la heri katika jambo hili kubwa na zuri ambalo liko mbele yako. Tuko pamoja na wewe na tunakuombea heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, watendaji wa Wizara hii na taasisi zao zote. Sisi sote ni mashahidi wa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya. Miaka kadhaa nyuma iliyopita tulikuwa tukikutana kwenye Bunge hili kujadili Bajeti ya Wizara ya Nishati tulikuwa tunatumia muda mwingi kwenye eneo la *REA,* lakini leo kuanzia kwenye hotuba ya Waziri, taarifa ya Kamati lakini hata Michango ya Wabunge inatambua kazi kubwa na nzuri inayofanywa kwenye uzalishaji wa umeme kwenye maeneo mengine na kwenye vyanzo vingine. Leo tutazungumzia gesi, umeme wa upepo, umeme wa jua na vyanzo vingine mbalimbali. Niwapongeze Wizara kwa maono hayo ni jambo zuri tunaliunga mkono endeleeni nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina mchango kwenye maeneo mawili. Eneo la kwanza ni eneo la usambazaji wa umeme vijijini lakini eneo la pili nitazungumza kidogo kuhusu gesi.

Mheshimiwa Spika, kama kuna miradi ambayo imesaidia kuipa heshima Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwenye nchi hii ni pamoja na mradi wa kusambaza umeme vijijini. Wananchi wamefurahi ni mradi unaogusa maisha yao moja kwa moja, ni mradi unaokwenda kubnadilisha maisha ya watu wetu kule vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye eneo hili mimi nilitaka nizungumze tu kuhusu Jimbo la Korogwe Vijijini. Sisi Korogwe vijijini tuna vijiji 118, vijiji 54 havijapata umeme kabisa. Tulikubaliana kwamba vijiji hivi vitapata umeme kupitia mradi wa *REA* awamu ya tatu mzunguko wa pili. Kwa bahati mbaya sana baada ya zoezi kufanyika na kutafuta wakandarasi kuna *lots* tano ambazo zilikosa wakandarasi ikiwemo *lot* moja ambayo ilikuwa ina Wilaya za Korogwe, Mkinga pamoja na Pangani. Tukachelewa kwa muda mrefu lakini baadae wizara, Serikali na *REA* wakatusaidia tukapata mkandarasi na tukaamini kwamba kazi ya kupeleka umeme kwenye vijiji inakwenda kuanza kwa kasi na wananchi wetu wapate umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya sana tukapata mkandarasi ambaye kwa kweli uwezo wake ulikuwa si wa kurudhisha na hivyo hajaifanya kazi hii Vizuri. Kipekee nishukuru sana Kamati yetu ya Bunge ya Nishati na Madini kwa kutembelea eneo la Korogwe kama eneo la kujifunza. Walipofika Korogwe waliona kazi aliyoifanya mkandarasi yule. Katika vijiji 54 mpaka Kamati inakwenda ilikwenda kuwasha umeme kwenye vijiji viwili na vijiji vilivyokuwa vinakaribia kuwa tayari na maeneo mengine yote kulikuwa hakuna kazi iliyofanyika. Jambo hili lilitusikitisha sana na limewaumiza sana watu wa Koropgwe na limewacheleweshा watu wa Korogwe kupata huduma ya umeme

Mheshimiwa Spika, lakini nimshukuru Mheshimiwa Waziri, baada ya Kamati kutoka tumekaa vikao kwa maelekezo yake Mheshimiwa Waziri na kwa usimamizi wake kwa kweli tumeanza kuona ile *speed* ya yule mkandarasi imeanza kubadilika. Katika vijiji 54, vijiji sita tayari tumekwishawasha umeme, vijiji viwili wanasubiri ratiba ya Mbunge tukawashe umeme kwa wananchi na kuna vijiji 21 tayari nguzo zimekwisha simikwa na kazi

inaendelea. Pia yako makubaliano ambayo tumekubaliana na mkandarasi huyo chini ya *REA* na ninyi wenzetu wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba niwashauri kwenye eneo hili la *REA* katika maeneo matatu.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa kwanza, makubaliano tuliyokubaliana kwenye vikao vyetu na yule mkandarasi ayatimize, na ayatimize kwa kasi; na tukiona hayaendi kama tulivyokubaliana tunaomba msisite kuchukua hatua nyingine za kisheria ili kazi zikamilike na wananchi wa Korogwe waweze kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tumesema kuhusu vitongoji. Mimi Korogwe tuna vitongoji 610. Kwenye hotuba yako Mheshimiwa Waziri kwenye ukurasa wa 36 umesema vizuri kwamba tunahitaji shilingi trilioni 6.7 ili kukamilisha kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote ambavyo havina umeme. Fedha hii ni nyingi sana, na wewe mwenyewe umesema tukienda kwa utaratibu wa kawaida tunaweza kuchukua miaka 20. Hata hivyo, kwenye kitabu chako umetuahidi kwamba mnakamilisha mpango wa kupeleka umeme kwenye vitongoji hivi angalau ndani ya miaka mitano kazi iwe imekamilika.

Mheshimiwa Spika, ninamwomba Mheshimiwa Waziri kazi hiyo waifanye kwa kasi. Kuna vijiji ambavyo vina vitongoji vikubwa na vina hadhi hata ya kuwa vijiji havijapata umeme. Kama shida ni fedha kaeni Serikalini huko wekeni utaratibu na ifanyeni hii kama mradi kama ilivyo miradi mingine. Kama tulivyo na mradi wa kupeleka vijijini tuwe pia na mradi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji vipate umeme tuwe tumemalizana na jambo la umeme kwenye vijiji na kwenye upande wa vitongoji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nilitaka nimshauri Mheshimiwa Waziri na wizara na hili kwa kiasi mmeanza kulifanyia kazi ni hii namna ya kupata wakandarasi. Utaratibu uliozoeleka na ambao umekuwa ukitumika mkandarasi anapatikana kwa njia ya ushindani. Mnazingatia vigezo vya kifedha na vigezo vya

kitaalamu kwa maana ya vigezo vya kiufundi. Huo ndio utaratibu ambao umekuwa ukitumika muda mrefu na kiukweli ndio ambao umehusika kutuchelewesha kufika hapa tulipofika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, tumeona maelekezo yako kwa *REA* kwamba vigezo hivi viwili visiwe vigezo pekee vya mkandarasi kupata kazi ya kupeleka umeme vijijini. Pamoja na kuangalia uwezo wa kifedha, uwezo wa kitaaluma na uwezo wa kiufundi umewambia *REA* waangalie historia ya Mkandarasi, utendaji kazi wake kwenye miradi mingine ambayo tayari alishaifanya huko nyima au ambayo anaendelea kuifanya. Ninashukuru nimesikia angalau *REA* wamesema kwa saa ili mkandarasi apewe kazi nyingine au mpya afike angalau asilimia 60 au 80. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba jambo hili lisiwe maneno likasimamiwe vizuri ili litusaidie kuendelea kupata wakandarasi wazuri ambao watafanya kazi vizuri ya kupeleka umeme kwenye maeneo ya vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nilitaka kulichangia kidogo ni eneo la gesi. kipekee tumshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali na kufufua tena ndoto za watanzania kufanya kazi ya utafutaji na uza.ishaji wa gesi ndani ya nchi yetu. Manufaa ya gesi ni makubwa, tangu Mheshimiwa Rais alipoamua mwaka 2022, nchi yetu sasa imeanza kukaribia kuingia kwenye ramani na kwenye nchi za uchumi wa gesi na mafuta. Tunampongeza sana Mhe shimiwa Rais kwa jambo hili kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, jambo hili limesemwa vizuri na hata kwenye hotuba Mheshimiwa Waziri amelieleza vizuri. Halikufikia maamuzi haya kwa bahati mbaya jambo hili ni la muhimu sana na lina sababu. Sababu ya kwanza ni Mheshimiwa Rais mwenyewe kutengeneza mazingira wezeshi na mazingira rafiki ya uwekezaji kwenye nchi hii hasa kwenye eneo la gesi, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili, jambo la gesi halikwepeki. Duniani sasa hivi gesi ni sekta inayokua kwa kasi. Sekta ya gesi inakuwa kwa zaidi ya asilimia 7.5 kwa mwaka sio jambo la kudharau. Vile vile, mahitaji ya gesi yamekuwa ni makubwa sana. Hata hivyo, kwa tafiti na taarifa tulizonazo tuna gesi za kutosha lakini pia tuna faida ya jiografia yetu. hapa tulipo ni rahisi kutoa gesi hapa kwa urahisi zaidi na kuipeleka maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoomba nishauri mambo mawili kwenye eno hili la gesi. kwanza, Mheshimiwa Waziri umesema kwenye hotuba yako ukurasa wa 50 kwamba mnaelekea kukamilisha kazi kudurusu mkataba kifani. Niwaombe sana jambo hili lifanyike kwa haraka ni jambo muhimu. Mkataba huu utatusaidia kutuwekea uwazi wa sisi tunafaidika nini? Nini wanafaidika wenzetu lakini pia itatuondolea uwezekano wa yeyote anayekuja kwenye Serikali au kwenye nafasi za Serikali kuamua anachokitaka kwa sababu tayari mkataba huu unao mwongozo wa kunufaika na mapato haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini jambo la pili nataka nishauri. Ukisikiliza michango humu ndani, ukamsikiliza Mheshimiwa Waziri, ukawasikiliza watendaji wa Wizara kuhusu jambo la gesi linasemwa kwa matarajio makubwa na faida kubwa na watu wana matumaini makubwa. Vile vile, gesi hii kuna hatua. Niwaombe jambo moja tu la muhimu sana, jiandaeni kama Serikali kufanya *expectation management*. Watu huko wanajua matrilioni, mabilioni yanakuja lazima wajue kuna hatua za kwenda, kuna hatua za kufuatwa mpaka uchimbaji unaanza na kunufaika moja kwa moja kunaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Rose Busiga, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, Mheshimiwa Boniphace Butondo ajiandae.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adhimu, Mungu akubariki sana. Pia, ninakuombea sana, umekuwa mwema sana, umekuwa ukiendesha shughuli za Bunge kwa uaminifu mkubwa sana. Sisi kama Wabunge tunakuombea katika mchakato wa uchaguzi. Naweza nikasema neno moja, Wamtumainio Bwana ni kama mlima sayuni hawatatikisika milele na milele. Tuna imani kubwa na wewe na tuna mwamini Mwenyezi Mungu atakwenda kutuvusha katika mchakato huo wa uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unanijua vema mdogo wako, kwamba ukinipa nafasi siichezei. Nafasi hii adhimu ninamuomba Mwenyezi Mungu anisaidie niongee ukweli ulioko moyoni. Unanifahamu mdogo wako ni mkweli tupu. Ilikuwa ni juzi, wakati wa wiki ya nishati, nilipata bahati ya kutemebelea mabanda, nikaenda moja kwa moja kwenye mkoa wangu nikiwa na maswali mengi. Nilipofika kwenye mkoa wangu kuna vijana ambao wamepikwa walinipokea vizuri nikaanza kuuliza maswali ya umeme. Katika Mkoa wangu wa Geita nina takribani vijiji 474 lakini viiji vyenye umeme ni 389 na vijiji 85 viko kwenye mpango wa *REA* mpaka sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba ufikishaji wa umeme kwenye Mkoa wa Geita ni asilimia 82. Kwa hiyo ni asilimia 18 tu ambayo umeme haujafika. Nani kama Mheshimiwa Rais? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naipongeza sana Serikali yangu ya Awamu ya Sita kwa namna ambavyo inaendelea kufanya kazi kwa uaminifu hapa ndipo ninapokuja kusema kazi iendelee; na hapa ndipo ninapokuja kusema tena hakuna kilicho simama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si jambo dogo, naomba niwaambie Watanzania si jambo dogo. Nakupongeza sana kaka yangu Mheshimiwa January Makamba, hongera sana kwa kazi ambayo unaendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais. Mimi ninaona vyema, ni Dhahiri, pamoja na naibu wako na wizara nzima na Katibu Mkuu kwa jinsi ambavyo mmeweza kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Spika, lakini ninarudi kwenye vitongoji, kuna kupeleka umeme katika vitongoji vyetu. Mkoa wangu wa Geita nina takribani ya vitongoji 2,261. Kati ya vitongoji hivyo ambavyo vina umeme ni vitongoji 965, vitongoji 1,296 havijafikiwa na umeme. Kwa heshima hiyo hiyo Kaka yangu January nilipokuwa nimetembelea lile banda, nikafika, wakasema Mheshimiwa Mbunge tunapomaliza kupeleka kwenye vijiji tunashuka mpaka kwenye vitongoji. Ninakuamini kabisa Mheshimiwa January Makamba tunapoenda kumaliza hii bajeti ninaomba vitongoji vya Mkoa wa Geita vikafikiwe na umeme. Sina shaka na wewe, na ninaamini wewe ni mtu mwema sana, ni mtu bingwa sana, hivyo utaenda kufikisha katika vitongoji hivyo 1296 ili wananchi waone Serikali yao jinsi inavyochapa kazi.

Mheshimiwa Spika, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Kiukweli niwadhihirishie Watanzania, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya kazi kwa nguvu zote. Ninaomba tumuamini Watanzania wenzangu. Kwa nini nasema hivyo? Ninasema hivyo kwa sababu ladha ya chakula anaijua mpishi, mimi mwenyewe wakati nikiwa kwenye banda lile nilifika Rufiji nikiwa hapahapa Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kwa sababu tu Kanuni za Bunge haziruhusu; lakini nilitama niwe humu humu Bungeni na wananchi wananiangalia waone ambavyo nimefika Rufiji. Mambo ambayo niliyoyaona, mafundi wako kazini wanaendeea na kazi, mambo ambayo niliyoyaona nilipofika pale Rufiji ujazo mkubwa wa maji unaendelea. Jamani Watanzania asiyeshukuru kwa kidogo hata kikubwa hawezi kushukuru. Mimi binafsi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ninamshukuru sana Kaka yangu Mheshimiwa January Makamba kwa sababu lile bwawa Mama alilipokea likiwa na asilimia takribani 30 leo tunazungumzia asilimia 88, nani kama Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Spika, tukienda mbele zaidi utaona upelekaji wa umeme kwenye migodi. Kaka yangu Mheshimiwa January unanisikia; kule kwetu Geita unajua kabisa sisi ni wachimbaji, ninakuomba kwenye migodi ambayo haijafikiwa na umeme kwa heshima hiyo hiyo kaka yangu ninaomba uweze kufikisha umeme

kwenye migodi ya Nyakafuru, Mwabomba na migodi mingine ambayo sijaweze kuitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana sana sana kwa nafasi hii ambayo umenipa. Nina imani wananchi wangu wa Mkoa wa Geita hasa akina mama walionichagua, ninawaambia ya kwamba tuwe na imani kubwa na Serikali yetu. Serikali yetu iko kazini, Serikali yetu si ya mchezomchezo, na Mheshimiwa January Makamba kanifikisha Rufiji nikiwa hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo ninamshukuru sana na kumpongeza Meneja wangu wa *TANESCO* Mkoa wa Geita pamoja timu yake nzima. Lakini kuna kaka mmoja ambaye sasa alikuwa ananipa hiyo elimu nilipotembelea, anaitwa *Engineer* Seif Abdul amenielewesha vizuri na ndio maana nimeweza kuchangia vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana baada ya kusema haya ninaunga mkono hoja, hongera sana Waziri wangu January Makamba hongera nyingi Naibu Byabato.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Palamagamba Kabudi, atafuatiwa na Mheshimiwa Boniphace Butondo, Mheshimiwa Byabato ajiandae.

**MHE. PROF. PALAMAGAMBA J. A. M. KABUDI:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu Rahim kwa ruzuku ya uhai na afya. Nichukue pia fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika bajeti ya Wizara ya Nishati. Nami niungane na wale wote wanaokutakia kila lakheri katika azma yako ya kugombea nafasi ya Rais wa *IPU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajua una hakika miongoni mwa watu ambao wanafuraha kubwa ya wewe kupanda katika nafasi hiyo ni mimi. Fahari ya Mwalimu yoyote yule ni kumuona mwanafunzi wake aliyemsomesha, aliyemlea anapanda na kupanda na kupanda zaidi. Kwa hiyo mimi ambaye nilipata bahati ya kuwa

Mwalimu wako katika ngazi mbalimbali nakuombea kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuipa kipaumbele na kuiwezesha sekta hii ya nishati kwa hali ya juu. Ila nimpongeze Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Nishati pamoja na Stephen Byabato, Naibu Waziri, Katibu Mkuu *Eng*. Mramba, Naibu Katibu Mkuu, Mbutuka kwa kazi nzuri mnayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utakuwa katika maeneo matatu nikipata fursa. Kwanza ni Wilaya ya Kilosa, pili Mradi wa Julius Nyerere na tatu Umeme wa Joto Ardhi. Mradi wa *REA* ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu na watu wake, na ndio mradi ambao unabadili hali ya maisha ya watu wetu vijijini. Na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais na Wizara ya Nishati kwa kutoa fedha zote kwenye Jimbo la Kilosa lenye kata 25 na vijiji 37 ambavyo havina umeme. Nishukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa tumepata mkandarasi ambaye utendaji wake wa kazi hauridhishi kabisa. Lakini katika hilo nikushukuru sana wewe mwenyewe Mheshimiwa Waziri, niwashukuru sana Mtendaji Mkuu wa *REA* Eng. Hassan Said, Meneja wa Mkoa wa Morogoro Mhandisi Fadhili Chilombe, Mameneja wa Kilosa, Meneja wa Mvomero na wale waratibu vijana wawili ambao sasa wamechukua hatua za kuhakikisha kwamba jambo hili sasa linashughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mkandarasi amepewa *deadline* ya tarehe 30 Juni awe amepeleka umeme katika vijiji 20 asipofanya hivyo achukuliwe hatua. Mheshimiwa Waziri naomba msukumo wako mkandarasi huyu atekeleze mkataba. Amepewa fedha zote na kwa hiyo hana sababu ya kuendelea kusuasua; na kama hatafanya hivyo ifikapo tarehe 30 Juni basi hatua zichukuliwe. Hatuwezi kuendelea kuwa na mkandarasi ambaye ana fedha na hafanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hilo ya *REA* na ugoigoi wa mkandarasi nimeletewa simu leo kutoka Kijiji cha Matongolo – Dumila kwamba inaelekea *transformer* imezidiwa. Mimi naamini kabisa Meneja wa Mvomero ambaye ndiye anayesimamia huko atalichukulia hatua ili liweze kurekebishwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo nije kwenye Bwawa la Mradi wa Mwalimu Julius Nyerere. Huu ni mradi ambao Watanzania wote hatuna budi kuwa na fahari nao na kuuenzi sana. Ni mradi ambao aliuasisi Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Na mnapokuwa na mradi huo ambao umeanzishwa na muasisi wa Taifa lenu na akashindwa kuutekeleza ninyi ambao mnapata heshima ya kuukamilisha mnapata baraka nyingi sana za Mwenyezi Mungu. Kwa hiyo mimi ninahakika kabisa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, wewe Waziri, watendaji wa *TANESCO* na wote waliohusika katika mradi huu Mwenyezi Mungu atawapa baraka kwa sababu mmetekeleza mradi ambao ulikuwa ndani ya moyo wa muasisi wa Taifa letu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kutekeleza mradi huu nchi yetu, *TANESCO,* wahandisi na wataalamu ewote wa Tanzania tumepata uzoefu na utaalamu wa kujenga kwa ufanisi zaidi miradi ijayo ya umeme wa maji kama vile Rumakali na Ruhuchi. Tajiriba hii tuliyoipata, tajiriba kwa kiingereza ni *experience*, tajiriba hii tuliyoipata kama nchi itatusaidia sana huko tuendako kuwa na muala katika kutekeleza miradi hii ya maendeleo na muhala maana yake ni *coherence*.

Mheshimiwa Spika, mradi huu una upekee wa aina yake na ni lazima tuuenzi kwa kadri tunavyoweza. Ukubwa wa bwawa hili kwa kweli ni ziwa, kwa sababu ni bwawa ambalo lina ukubwa wa kilomita za mraba 1,194.4 ni kubwa zaidi ya Ziwa Eyasi lenye kilomita za mraba 1,050 ni kubwa zaidi ya Ziwa Natroni lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,040 na ni kubwa zaidi Ziwa Manyara lenye kilomita za mraba 470. Kwa hiyo bwawa hili kwa kweli linatupa heshima ya Ziwa na Bwawa hili ni muhimu sana kama ambavyo alilifikiria Baba wa Taifa. Moja ni kuzalisha umeme lakini moja ilikuwa ni kudhibiti mafuriko ya Mto Rufiji. Na mimi

naamini kabisa sasa tatizo la mafuriko ya Mto Rufiji yamekwisha, lakini pia bwawa hili litatusaidia katika kilimo, katika Utalii.

Mheshimiwa Spika, katika utalii nimeambiwa kwamba bwabwa hili baada ya kuwa limejaa katika ujazo wake litakuwa na visiwa visivyopungua sita litakuwa ni bwawa la aina yake Duniani lenye utalii pia wa visiwa ndani ya bwawa hilo. Nishukuru sana kwa juhudi kubwa zinazochukuliwa mpaka sasa katika mikoa yote kumi na wilaya 26 zenye mito inayopeleka maji katika bwawa hili. Ni vizuri kabisa tujue hilo hiyo mikoa 10 na wilaya 29 zenye mito inayopeleka maji katika bwawa hili zinawajibu mkubwa sana wa kutunza mito hiyo, vyanzo hivyo vya maji ili kuhakikisha maji yanaendelea kutiririka. Watu waendelee kuelimishwa katika maeneo hayo na wajue maji yanatoka sehemu nyingi. Maji yanayokwenda kwenye hili bwawa yanatoka Chunya, Sikonge, y Manyoni, Tunduru, Kilombero, Chamwino, Chemba, Songwe, Mbeya na Makete; na zaidi kabisa ni kutunza *Wetland* ya Kilombero bila *Wetland* ya Kilombero kutunzwa bwawa hili itapata shida.

Mheshimiwa Spika, mimi niombe kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri January Makamba kwa kushirikiana na wenzako katika Ofisi ya Rais, Makamu wa Rais Mazingira, Wizara ya Maji, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya TAMISEMI kuhamasisha watu wote katika mikoa hii kumi na Wilaya hizi 24 kujua wajibu mkubwa walio nao wa kutunza mito na vyanzo vya maji ili bwawa hili liendelee kwa manufaa yetu. Na tutakapoata hizi *megawatt* 2115 tutakuwa tumepata umeme mwingi wa kutuwezesha kuleta maendeleo makubwa.

Mheshimiwa Spika, bila umeme huwezi kuwa na viwanda, miundombinu na huwezi kufanya chochote. Ndiyo maana Mwasisi wa *Soviet Union Vladimir Lenin* alipochukua uongozi alipochukua uongozi wa *Soviet Union* kazi yake ya kwanza ilikuwa ni kupeleka umeme. Kazi ya kwanza aliyoifanya Kwame Nkrumah Ghana baada ya Ghana kupata uhuru ilikuwa ni kujenga Bwawa la Umeme la Akasombo ili aweze kuleta maendelo kwa Ghana. Kwa hiyo suala la bwawa hili ni suala muhimu sana. Kwa hiyo ningeomba Wizara zote na wadau wote na sisi Wabunge tuone

fahari na bwawa hili lakini sasa tuongeze juhudi katika kutunza mazingira ili mradi yaweze kwenda katika bwawa.

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyofika kwa Mheshimiwa January Makamba sasa ni sawasawa na *pilot* ambaye ametangaza ndege kutua. Tunaitakia ndege hiyo itue salama na kama kutakuwa na *landing turbulences* basi *pilot* ashike usukani ndege itue salama.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ambalo ningependa kulichangia ni hili la umeme wa joto ardhi. Katika maonesho haya nimepata elimu kubwa sana kuhusu joto ardhi. Na mimi naomba Wizara, Mheshimiwa January Makamba, jambo hili ambalo mmelianza sasa na mtakalolianzia kule Ngozi na yale maeneo mengine manne mliongeze juhudi kubwa sana. Kama tu pale Ngozi kwa awamu ya kwanza tutapata *megawatt* 70. *Megawatt* 70 si umeme mchache tunaamini katika maeneo mengine 52 tutafanikiwa kupata umeme mwingi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kenya sasa wanazalisha *megawatt* 1000 kutokana na joto ardhi, sisi kwa vyanzo vyote tulivyonavyo tutapata umeme mwingi sana naomba kuunga mkono hoja na kwa asilimia zote.

Mheshimiwa Spika, kila lakheri katika mbio zako za unakoelekea. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Boniphace Butondo, atafuatiwa na Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, mtoa hoja ajiandae.

**MHE. BONIPHACE N. BUTONDO:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu ya Nishati, Wizara ambayo Wabunge takribani wote hapa tumekiri wazi kwamba ni Wizara ambayo ni ya muhimu kabisa kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na hata leo napata nafasi ya kuchangia kwa ajili ya mambo muhimu kabisa yahusuyo nishati. Lakini la kwanza nikupongeze wewe kwa uthubutu wako na kuamua kugombea nafasi hii katika Bunge la *IPU*. Nataka nikuhakikishie sisi Wabunge tutaendelea kukuombea wakati wote ili mradi haya aliyoyazungumza Mheshimiwa Matiko kama mjumbe wako kuhakikisha kwamba na sisi maombi yanaungana pamoja na nyinyi kuhakikisha kwamba unapata ushindi wa kishindo katika uchaguzi huo unaokuja.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nimpongeze Mheshimiwa January Makamba Waziri katika Wizara hii ya Nishati kwa namna ambavyo amekuwa akifanya kazi nzuri ya kuisimamia Wizara hii; na mabadiliko makubwa katika kipindi chake cha uongozi sisi wenyewe tumekuwa mashuhuda na Watanzania wamekuwa mashuhuda katika mapinduzi makubwa ambayo umekuwa ukipambana wakati wote ili kuhakikisha kwamba azma ya Watanzania na Serikali inaweza kufikiwatena katika kiwango kinachotakiwa.

Mheshimiwa Spika, nimpengeze sana Mheshimiwa Byabato ambaye ni Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji katika Wizara hii. Pia naomba nitumie fursa hii kumpongeza sana Meneja wangu wa *TANESCO* Mkoa wa Shinyanga pamoja na Wilaya yangu ya Kishapu kwa namna ambavyo wamekuwa wakisismamia vizuri suala zima la umeme katika Wilaya yangu ya Kishapu na Mkoa mzima wa Shinyanga.

Mheshimiwa Spika, kuna kampuni hii ya Suma JKT ambaye ndiye mkandarasi anayesambaza umeme katika Wilaya yangu ya Kishapu. Naomba nimpongeze kwa sababu kwa kweli kazi inayofanyika ni kubwa na changamoto ilikuwa ni kubwa kwa sababu tulikuwa na idadi kubwa ya vijiji ambavyo havikuwa na umeme kabisa, na sasa tunaona mabadiliko makubwa yanayoendelea katika sekta hii muhimu katika Jimbo langu la Kishapu.

Mheshimiwa Spika, na moja kwa moja naomba niunge mkono hoja kwamba bajeti hii yenye thamani ta trioni tatu iweze kupita kwa asilimia 100 kwa manufaa ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, la kwanza katika mchango wangu naomba Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana kwa kusimamia suala zima la Mradi wa Umeme wa Jua ambao tarehe 29 Mei tumeweza kusaini mkataba huu na kuushuhudia sisi Wabunge pamoja na Kamati ya Kudumu ya Nishati ya Bunge kwa namna ambavyo mradi huu unakwenda kuwanufaisha Watanzania.

Mheshimiwa Spika, Mradi huu upo katika jimbo la kwangu la kishapu katika Kata ya Taraga Kijiji cha Ngunga; na tunakwenda kuzalisha *megawatt* tano na mradi huu ni wa thamani ya zaidi ya bilioni 275. Kwa kweli mradi huu ukishakuwa umekemilika hizi *megawatt* tano zinaweza kuongezwa katika *Grid* ya Taifa, na kwa hali hito tunaenda kupunguza pakubwa sana tatizo la umeme hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu niseme kwamba mradi huu ni mradi mkubwa wa kwanza, na kwa maana hiyo tunatarajia makubwa yatakuwa yanakuja kwa sababu Mkoa wa Dodoma nao unaenda kupata bahati ya mrado huu mkubwa wa Umeme wa Jua. Sasa kwa msingi huo naomba niipongeze sana Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano kwa jitihada kubwa anazozifanya kuhakikisha kwamba Watanzania tunaondokana na changamoto kubwa ya umeme katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo kubwa ambalo naliona katika mpango huu wa umeme huu wa jua ambao katika Wilaya ya Kishapu tunaenda kunufaika nao; kwanza tunaenda kupata *service levy* kwa ajili ya Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kishapu ambayo tunakwenda kuongeza mapato ya ndani ya halmashauri yetu kwa sehemu kubwa sana. Lakini tunashuhudia kwamba tunakwenda kupata *CSR* ambayo itakwenda kusaidia sana maeneo muhimu. Kwa mfano, tunakwenda kunufaika na ujenzi wa hospitali ambayo itajengwa katika eneo hilo, tunaenda

kunufaika na ujenzi wa bwawa kubwa litakaloenda kujengwa eneo hilo, na pia kuna ujenzi wa shule ambao tunarajiwa utafanyika katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengine mengi ambayo tumekaa kwa pamoja na mikakati imeshaanza kusimamiwa na Mheshimiwa January kuhakikisha kwamba miradi hii inayokwenda kusaidia wananchi inaanza kufanya kazi vizuri; haya ni manufaa makubwa ambayo tunaenda kufanikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na changamoto kubwa ya kukatika umeme katika Wilaya yetu ya Kishapu; na kwa sababu tuna Mgodi wa Almasi wa Mwadui, lakini tuna migodi katika Mkoa wetu wa Shinyanga, kwa maana ya migodi iliyopo Wilaya ya Kahama. Haya matatizo ya kukatika kwa umeme baada ya suluhisho hili mimi naamini kwamba sasa tunaenda kuondokana na changamoto hizo. Na kwa hali hiyo ninaomba nikutakie kila la kheri ili usimamizi katika utekelezaji wa mradi huo uende vizuri na manufaa tuyaone kwa ajili ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumzie eneo la *REA*. Wilaya ya Kishapu mpaka sasa kwa mwaka wa fedha huu ambao tunakwenda kumalizia tumeweza kuwasha vijiji 13, na hii kazi imesimamiwa na SUMA JKT. Kwa hiyo, nawapongeza sana kwa jitihada kubwa ambayo wamekwenda nayo.

Mheshimiwa Spika, lakini bado tuna vijiji 28 kati ya vijiji 51 ambavyo vilikuwa havijapata umeme; vijiji 28 bado havina kabisa umeme. Kwa hiyo, naomba kasi hii iweze kuongezwa, na SUMA JKT chini ya *Engineer* Meja Mohammed nawaomba waongeze kasi ili suala la kuwasha umeme katika maeneo haya yaweze kuafanyika. Nimeshuhudia nguzo zimesambazwa katika vijiji vyote na tulikuwa tunasubiri nyaya ndiyo changamoto kubwa. Naamini kwamba kama hili nalo litasimamiwa maeneo haya yote yanaweza kupata umeme kwa wakati. Mimi naomba sana SUMA JKT muongeze kasi ili mradi suala hili liweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba tu niyataje baadhi ya maeneo ambayo hayana kabisa, ni kata ambazo hazina kabisa umeme, ambazo ni Kata za Lagana, Mwasubi, Mwamashele pamoja na Bunambiu. Hizi ni kata nne ambazo hazina kabisa umeme. Kwa hiyo, nilikua naomba hata mkandarasi atazame kwa macho maeneo haya muhimu na hasa ile Bunambiu na Mwasubi kwa sababu ni maeneo ambayo maji yanapita mengi na ikifika nyakati za masika inawezekana changamoto ikawa kubwa sana, hivyo waongeze kasi kuhakikisha kwamba wanaharakisha katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine ninaomba nipongeze sana kwa jitihada kubwa ambazo Mheshimiwa Waziri umekuwa ukisimamia suala zima la mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Tumeshuhudia kabisa kwamba sasa imefikia asilimia 80. Kazi hii ni kubwa unayoifanya; na mimi naomba nipongeze hata Kamati yenyewe ya Nishati kwa namna ambavyo mnasimamia kuona kwamba mradi huu unakamilika kwa wakati na hivyo Taifa liweze kuondokana na changamoto ya umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala zima la vitongoji, nina zaidi ya vitongoji 145 katika Wilaya ya Kishapu. Vitongoji ambavyo tayari vimeshapata umeme ni vitongoji kama 55, vitongoji zaidi ya 90 bado vina changamoto kubwa ya umeme. Pamoja na kuongezewa idadi hii ya vijiji 15 ambao ni mpango ambao unakwenda kutekelezwa lakini bado jitihada zinatakiwa ziongezewe ili kuhakikisha kwamba vitongoji vyote vinapata umeme. Maeneo haya Watanzania wamekubali kubadilika, na kasi ya wananchi wanavyojitokeza kujisajili kwa ajili ya kuwekewa umeme ni mkubwa sana. Ninaomba Serikali, kwa maana ya Wizara, Mheshimiwa January ongeza kasi ili vitongoji vyote tuweze kupata umeme kabla ya mwaka 2025.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa namna ya pekee, sasa naomba nizungumze mambo machache ambayo ni changamoto nikishauri kwamba tuweze kusaidia katika maeneo haya. La kwanza, ni eneo la usafiri. Jimbo la Kishapu na Wilaya ya Kishapu ina tatizo kubwa la usafiri, lakini la pili ni watumishi, naomba eneo hilo na lenyewe litazamwe. Tuna tatizo kubwa la

watumishi katika eneo hili; panapotokea *emergency* tatizo linakuwa ni kubwa sana kwa ajili ya kutatua matatizo ya aina hii.

Mheshimiwa Spika, ninakushuru sana kwa kunipa nafasi naunga asilimia mkono hoja 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nilikuwa nimeshamtaja Naibu Waziri lakini wako wageni walioingia mchana huu Bungeni hapa.

Tunao watumishi wa Wizara ya Nishati na taasisi zake walioshiriki katika Maonesho ya Wiki ya Nishati yaliofanyika katika Viwanja vya Bunge Jijijini Dodoma, na hawa ni watumishi kutoka Wizara ya Nishati. *(Makofi)*

Wapo watumishi kutoka *EWURA, PURA, TPDC, PBPA, TGDC, REA* Makao Makuu, Waratibu wa Miradi ya *REA* kutoka mikoani, *TANESCO* makao makuu, Mameneja wa *TANESCO* wa Kanda na Mameneja wa *TANESCO* wa mikoa wote wasimame kwa pamoja, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambaye anatoka Jijini Mwanza, na huyu ni Ndugu Bujiku Kaswahili, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni 35 wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni Wanafunzi wa Chuo cha Biblia Sajaranda kutoka Itigi, Mkoa wa Singida, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 23 wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma kutoka Manyoni Magharibi, Mkoa wa Singida, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Nishati, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu, na hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025 /2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kupitia Wizara ya Nishati kwa kuendelea kutekeleza kwa ufanisi mkubwa miradi ya umeme ikiwemo Miradi ya Kusambaza Umeme Vijijini *(REA)* na ujenzi mkubwa wa Bwawa la Julius Nyerere *(JNHPP)* litakalozalisha umeme wa megawati 2,115. Miradi hii ya Kusambaza Umeme Vijijini umeiweka Tanzania katika nafasi ya juu Afrika na umeweza kuchochea kasi ya ukuaji wa viwanda na uchumi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za vita ya Ukraine na Urusi na kupelekea kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli, napongeza Serikali kushirikisha Wizara ya Nishati, Wizara ya Fedha, *EWURA* na wadau wengine kuweka mkakati wa kuanzisha Mfuko wa Kudhibiti Mabadiliko ya Bei za Mafuta *(Fuel Price Stabilization Fund)* ili kukabiliana na kupanda kwa bei za mafuta. Pia Serikali ichukue hatua stahiki za kuanzisha Hifadhi ya Taifa ya Kimkakati ya Mafuta *(Strategic Petroleum Reserve-SPR)* ili kukabiliana na dharura na kuimarisha usalama na uhakika wa mafuta kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za upatikanaji wa dola za Kimarekani *(USD)* kwa kipindi kirefu sasa, makampuni yanayoagiza mafuta yanapata changamoto za kulipia mafuta kwa wakati na kulazimika kulipa faini kwa Shirika la *PBPA*. Kutokana na ukame wa *USD* kwenye soko la fedha za kigeni, makampuni yamelazimika kukopa kwenye mabenki kwa namna tofauti *(post import loans, swaps, forward contracts etc)*. Kutokana na changamoto za upatikanaji wa dola, makampuni yameshindwa kuagiza mafuta ya kutosha na hali hii ni hatarishi kwa uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na makampuni kulazimika kununua *USD* kwa gharama kubwa zaidi ya bei elekezi ya Benki Kuu, makampuni yameshindwa kulipia na kupelekea kushindwa kupokea mafuta.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuchochea upatikanaji wa *USD* hasa kutoka vyanzo vya madini na kilimo na ikiwezekana kuanzisha utaratibu wa biashara ya Serikali kwa Serikali na nchi rafiki zinazozalisha mafuta kwa makubaliano kulipa baada ya makusanyo ya mauzo ya madini na kilimo. Serikali inaweza kuratibu mfumo mzuri wa kununua dhahabu yote toka kwa wachimbaji wadogo kwa shilingi na kulipa bei nzuri zaidi kuliko hata ya soko na ikifanya hivyo kwa mazao ambayo yamekuwa yanatoroshwa kinyemela nje ya nchi. Dhahabu na mazao yaliyonunuliwa kwa shilingi yapate soko zuri kwa wanunuzi kwa dola za Kimarekani kusaidia uagizwaji wa mafuta. Kwa taarifa za makampuni yanayoagiza mafuta yanahitaji zaidi ya *USD* bilioni moja ili kulipia mzigo uliofika nchini ila haujapokelewa na kila mwezi inatakiwa kutenga *USD* milioni 250 kwa ajili ya kuagiza mafuta ya ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kununua mafuta kwa pamoja *(BPS)* umeonesha mafanikio makubwa na napendekeza uendelee ikiwa ni pamoja na kuvutia kutumika kwa mahitaji ya mafuta kwa nchi jirani. Mfumo huu uboreshwe hasa katika kuweka vinasaba kwa kutumia mashine *(automation)* na pia kuwepo na ulinganifu wa taarifa ya kila siku kati ya kiasi cha vinasaba vilivyotumika na kiasi cha mafuta yaliyopakiliwa. Na pia

magari ya kubeba vinasaba yafungwe kamera kwa ajili ya udhibiti mafuta yanayoenda nchi za nje pasipo kutorudi kinyemela kutumika nchini.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto za kupakua mafuta bandarini, napendekeza kupanua na kuboresha miundombinu ya kupakulia na kupokelea mafuta ikiwemo kupakua mafuta kwa saa 24. Napendekeza pia kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwa matumizi ya ndani na pia kwa nchi jirani, na usafirishaji uwe wenye tija kubwa ikiwemo kusafirisha kwa treni. Pia Serikali iangalie uwezekano wa kujenga bomba la mafuta kwenye MKUZA wa *TAZAMA* na kujenga miundombinu ya kuhifadhi mafuta kwenye bandari kavu eneo la Inyala, Mbeya kwa matumizi ya mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na nchi jirani za DRC, Zambia, Malawi na hata Zimbabwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na *REA* kutekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye makao makuu ya karibu vijiji vyote vya jimbo la Mbeya Vijijini, bado kuna uhitaji mkubwa wa umeme kufika kwenye vitongoji vyote. Napendekeza kuendelea kwa kasi utekelezaji wa Awamu ya Pili ya Mradi wa *REA III (REA III, Round II)* na kufikisha umeme katika vijiji vyote vilivyobakia na pia kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujazilizi *(Densification)*. Napendekeza utekelezaji utoe kipaumbele kwa Kata za Itawa na Shizuvi na pia kwenye vitongoji vinavyolizunguka Jiji la Mbeya, ikiwemo Mina na Lusungo Kata ya Iwindi, Kijiji cha Shongo, Kijiji cha Wambishe, kwenye shule zote ikiwemo Shule ya Sekondari Iwiji.

Mheshimiwa Spika, katika vijiji vilivyopatiwa umeme kwa kiasi kikubwa imechochea ukuaji wa viwanda hasa vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo. Nashauri *TANESCO* iongeze *speed* ya kuunganisha umeme na pia kushughulikia maombi ya wateja wengi wanaosubiria umeme ikichukuliwa hii ni fursa pia kwa *TANESCO* kuongeza mapato ya shirika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na vyanzo vya sasa, napendekeza Serikali itekeleze miradi ya vyanzo vingine kama vile vyanzo vya Jotoardhi, Umeme wa Jua, Upepo na Mkaa wa

Mawe ili nchi yetu iendane na mahitaji makubwa ya umeme kwa hapa Tanzania na hata kuuza kwa nchi zingine za Afrika. Ni muda mrefu sasa, *TANESCO* kupitia Kampuni Tanzu ya Uendelezaji wa Jotoardhi nchini *(TGDC)* inaendelea na tafiti katika maeneo mbalimbali nchini kama vile eneo la Ziwa Ngozi lililoko Mkoani Mbeya ambapo ndipo yalipo makutano ya Bonde la Ufa la upande wa Mashariki na lile la Magharibi.

Napendekeza Serikali iharakishe utekelezaji wa miradi huu wa Jotoardhi na ule wa Mkaa wa Mawe wa Mchuchuma na Kiwira ili tuweza kuzalisha umeme zaidi kwa mahitaji ya ndani na nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Wizara kwa ushirikiano wao mzuri na pia kwa kusogeza huduma hasa za Taasisi kama vile *REA* na *TANESCO* hapa Bungeni, hii imetusaidia sana Wabunge kupata ufafanuzi wa papo kwa papo katika masuala ya majimbo yetu.

Mheshimiwa Spika, nina masuala mawili tu; moja ni kuhusu bei hasa maeneo ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji yanasomeka kuwa yapo mjini, lakini uhalisia wa maisha na kipato ni maisha ya kijijini. Kwa mfano Halmashauri ya Mji wa Mafinga, ni mji lakini ina vijiji kumi na moja rasmi katika kata tatu. Lakini pia yapo maeneo ya pembeni mwa mji ambako maisha na kipato ni ya kijijini. Mfano wa maeneo haya ni mengi, hapa Dodoma ni Jiji lakini katika kata 41 ni kata kama 20 tu ndizo maisha ya mjini, kata nyingine 21 maisha na kipato ni ya kijijini. Kwa sababu hiyo mara kadhaa kupitia maswali na majibu nimeshauri kwamba tutizame upya bei ile ya shilingi 340,000 ndani ya mita 30.

Mheshimiwa Spika, nafahamu kwa maeneo ya vijiji yanayohudumiwa na *REA* bei ni shilingi 27,000. Naomba nieleweke vema, simaanishi kwamba maeneo ya vijiji lakini ambayo kwa mujibu wa sheria yanasomeka kuwa ni miji yatozwe shilingi 27,000, hapana, ushauri wangu ni kwamba tuwe na makundi kwa mfano ziwepo bei tofauti tofauti, tunaweza kusema

kwa mfano maeneo ya pembezoni ya mji ikawa Kundi A bei shilingi 150,000; Kundi B ikawa ni vijiji ambavyo kwa mujibu wa sheria viko mjini lakini kimaisha na kipato ni kijiji, mfano pale Mafinga maeneo kama Ndolezi, Luganga, Mkanzaule na kadhalika maisha yao ni kijiji, kundi hili tukasema walipe shilingi 97,000.

Mheshimiwa Spika, hizi bei ni mfano tu lakini ninyi kupitia wataalam wenu mnaweza kuchakata mkaona namna bora ya kulifanikisha suala hili ambalo kwa mujibu wa majibu hapa Bungeni, mara kadhaa tumeelezwa na Wizara kwamba suala hili liko katika hatua za mwisho za kufanyiwa kazi. Naomba kama litawezekana basi tupate majibu kamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kuhusu nguzo; Kamati ya kupitia sekta ya uzalishaji na upatikanaji wa nguzo za umeme; kwanza nawapongeza Serikali kwa ushirikishwaji pale ilipokuja taharuki kwamba Serikali itaanza kuagiza nguzo kutoka nje ya nchi. Tulikaa na Waziri na timu yake pamoja na viongozi wa Serikali na Chama wa Mikoa ya Iringa na Njombe, kikao hiki kilihusisha Waziri, Katibu Mkuu, Kamishna wa Nishati na watendaji wa *TANESCO* na *REA* kwa upande wa Wizara na kwa upande wa mikoa ilihusisha Wenyeviti wa CCM wa Mikoa ya Iringa na Njombe na Wenyeviti wa Wilaya zote, Wakuu wa Mikoa, Wabunge, Wakuu wa Wilaya, Wenyeviti wa Halmashauri, Wakurugenzi, baadhi ya Waheshimiwa Madiwani na wadau wa sekta kwa mana ya wazalishaji na wasambazaji.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uzito wa suala hilo na jinsi ambavyo linagusa maisha ya watu na uchumi wao, ilishauriwa paundwe Kamati ya Wizara na wadau ili kupitia mnyororo mzima wa suala la nguzo kuanzia upatikanaji wake na suala zima la ubora. Kamati hiyo iliundwa kwa nia njema yq kupata muafaka kuhusu suala la nguzo kuhusu upatikanaji, masuala ya manunuzi, ubora na kadhalika. Nia miradi ipate nguzo kwa wakati na kwa ubora na wakati huo huo wananchi waendelee kunufaika kama ilivyo katika suala zima la *local content*.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu Kamati hiyo ikamilishe kazi yake ili mapendekezo ya Kamati yawafikie wadau na Serikali kwa nia ile njema ya kuhakikisha nguzo zinapatikana kwa wakati na kwa ubora. Bado naamini tunaweza kuzalisha nguzo hapa nchini, kwa hiyo, Kamati hiyo kuhitimisha kazi yake ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Makamba na Naibu wake Mheshimiwa Stephen Byabato pamoja na jopo la wataalam wa Wizara kwa kazi kubwa wanazofanya kupeleka umeme na nishati nyingine muhimu kwa wananchi wetu hapa nchini Tanzania.

Mheshimwa Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuongeza bajeti ya Wizara hii kutoka shilingi trilioni 2.91 kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 hadi shilingi 3,048,632,519,000 kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utahusu kukosekana umeme katika baadhi ya maeneo ya Jimbo la Moshi Vijijini ambayo hayajaunganishwa.

Mheshimwa Spika, pamoja na juhudi kubwa zinazofanywa na Serikali kupeleka umeme vijijini, bado wananchi wengi wa Jimbo la Moshi Vijijini hawajapatiwa nishati ya umeme.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ninaiomba Wizara ya Nishati isaidie kutatua changamoto za nishati ya umeme katika Jimbo langu la Moshi Vijijini kwani bajeti iliyotengwa ni kubwa na Wanamoshi Vijijini watafurahia kufikiwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo yenye changamoto ya umeme katika Jimbo la Moshi Vijijini ni kama ifuatavyo; Kata ya Mabogini; kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, katika Kata ya Mabogini sehemu ambazo hazijapata umeme hadi sasa ni Vitongoji vya Sanya "*Line A*" na Mjohoroni vilivyopo katika kijiji cha Mabogini.

Pia katika Kitongoji cha Uru - katika Kijiji cha Muungano; katika Kijiji cha Maendeleo, Vitongoji vya Mshikamano na Uarushani; Mgungani - katika Kijiji cha Mtakuja; katika Kijiji cha Mserekia, hakuna umeme katika Vitongoji vya Mbeya Kubwa, Mbeya Ndogo, Remit, Mkwajuni na Mafuriko. Kijiji cha Mji Mpya, Kitongoji cha Utamaduni hakijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Arusha Chini kwenye Kijiji cha Mikocheni, Vitongoji vya Masaini na Mashimo ya Mchanga hakuna umeme. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye maeneo haya.

Aidha katika Kata ya Kimochi, Kitongoji cha Kiwalaa kilichopo Kijiji cha Sango; Kitongoji cha Iryaroho kilichopo katika Kijiji cha Mowo; na Kitongoji cha Maryaseli katika Kijiji cha Lyakombila havina umeme. Ninaiomba Serikali ikamilishe ujenzi wa miundombinu ya umeme katika maeneo niliyotaja hapo juu.

Katika Kata ya Kibosho Mashariki kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, Kata ya Kibosho Mashariki inahitaji huduma katika Kijiji cha Sungu Vitongoji vya Kyareni na Nkoitiko havijaunganishwa; katika Kijiji cha Singa, Kitongoji cha Singa Juu hakijaunganishwa; katika Kijiji cha Mweka, Kitongoji cha Mweka Juu na Omi havijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji na vitongoji vilivyotajwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kibosho Kati kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, katika Kata ya Kibosho Kati, vijiji vya Uri na Otaruni umeme una nguvu kidogo *(low voltage)* na kunahitajika transfoma. Katika Kijiji cha Otaruni, Kitongoji cha Ngoroshi hakuna umeme, na tunaomba wananchi wapatiwe huduma.

Katika Kata ya Okaoni - Vijiji vya Sisamaro, Omarini na Mkomilo vinahitaji kuunganishwa japo baadhi ya maeneo nguzo zimepita ila bado kuunganishwa.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Kindi, Kijiji cha Chekereni Weruweru, Vitongoji vya Miembeni na Kisiwani havina umeme kabisa. Pia baadhi vitongoji vya vijiji vya Kindi Juu na Kindi Kati havijapata umeme, ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye vijiji na vitongoji hivi.

Mheshimiwa Spika, katika Kata ya Uru Mashariki, kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, Kijiji cha Materuni, Kitongoji cha Wondo hakijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye kitongoji hiki.

Mheshimiwa Spika, Kata ya Mbokomu ni kama nilivyoomba kwenye bajeti ya mwaka jana na mwaka juzi, Kitongoji cha Mmbede Kyaroni, Tema na Masanga na baadhi ya maeneo ya Korini Kati havijaunganishwa. Ninaiomba Serikali ipeleke huduma kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kwa uhai pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya katika Taifa letu, hakika Mungu ampe afya njema.

Mheshimiwa Spika, pongezi nyingi ziende kwa Waziri na Naibu wake wa Wizara hii ya Nishati pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, niende katika Jimbo la Temeke; niwapongeze sana kwani kazi imewezakufanyika kwa ufanisi, tunashukuru umeme umeweza kuwa *stable* kuliko miaka ya nyuma, lakini niombe kwa kuwa jimbo letu la Temeke limekuwa ni jimbo la viwanda vingi na umeme umekuwa bado ni mdogo kwani hautoshelezi kwa viwanda na matumizi ya majumbani, lakini pia umeme bado tunapata kutoka Ilala. Tunatamani kupata ongezeko la transfoma kubwa ambayo itatuongezea umeme ukizingatia bado hatupati umeme mfululizo kwani katika wiki tunaweza kukosa, baadhi ya kata ukakatika kwa masaa kadhaa

na ukirudi unarudi mdogo na wakati mwingine unarudi kwa baadhi ya mitaa ya kata moja na mitaa mingine ikakosa ndani ya kata hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, niombe sana muangalie upya umeme unaopita chini ya ardhi, tupate vipuli vyake ili urekebishwe maana kila umeme unapokatika tunaambiwa hitilafu kubwa inatoka kwenye Kituo cha *TOL* pale *Pugu Road,* naamini mnapafahamu hivyo niombe sana Wizara ituangalie sana Jimboni Temeke, ni jimbo tunategemea sana mapato yetu ya ndani kutoka kwenye viwanda hivyo visipopata umeme kazi hazitafanyika na pia wafanyabiashara wadogo wadogo waweze kufanya biashara zao ili mapato yaongezeke na Watanzania wa jimboni wafaidike na kazi nzuri ya matunda ya uongozi mzuri wa Mama Samia, Rais msikivu na myenyekevu.

Mheshimiwa Spika, nawapeni hongera sana kwa maonyesho ya Bungeni yamenifungua na mengi nimejifunza, naunga mkono hoja.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nianze na nguzo za zege; maeneo ya hifadhi yamekuwa na changamoto ya mara kwa mara kuungua kwa nguzo. Mkoa wa Rukwa tuingizwe kwe Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo Namanyere tuondolewe kwenye gharama ya umeme wa shilingi 320,000 kwani haiendani na uhalisia wa maisha yao.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Watanzania wenzangu wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia baraka zake katika nyanja mbalimbali za ustawi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na wananchi wa Jimbo langu la Mbulu Mjini kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali nzima ya Awamu ya Sita kwa jinsi wanavyoliongoza Taifa letu na kutatua changamoto nyingi

sana zinazowakabili wananchi hususan utekelezaji wa Ilani ya CCM yam waka 2020 - 2025 kwa kila sekta. Hivyo basi tuendelee kuliombea Taifa letu kwenye nguzo kuu ya amani, upendo, uchumi, baraka, utulivu, diplomasia ya kisiasa, na mshikamano kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe, Naibu Spika na Wenyeviti wetu wote kwa kuliongoza Bunge letu katika kuzigatia Kanuni za Bunge kikamilifu na kwa busara ya hali ya juu hongereni sana.

Mheshimiwa Spika, aidha, sisi Wabunge wako tunaungana wote kukuombea mafanikio mema katika nafasi unayogombea, Mwenyezi Mungu awe kiongozi katika kufungua mapito yako upate kuchaguliwa kwa maslahi makubwa ya Taifa letu.

Aidha, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa January Makamba, Waziri wa Nishati Naibu Waziri na watendaji wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kupitia mapendekezo na maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge na kupitia maoni ya Mheshimiwa Dunstan Kitandula, Mwenyekiti wa Kamati yetu na hotuba ya Mheshimiwa January Makamba Waziri wetu wa Nishati.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuelezea hali halisi ya jiografia ya Jimbo la Mbulu Mjini; eneo la Mbulu Mjini tuna kata 17 kati ya hizo kata 11 ni maeneo ya vijiji na kata sita ni eneo la mitaa 58 ya miji. Hapa naomba kutoa maelezo ya hali ya uunganishaji wa umeme katika vijiji, mitaa na vitongoji. Ninaishukuru sana Serikali, tayari tumeweza kuunganisha laini kubwa kwenye makao makuu ya kila kata, kwa upande wa vijiji bado hatujaweza kuwasha umeme kwenye vijiji 11 hali inayowafanya wananchi kutopata huduma hii muhimu ya kuwaunganishia umeme. Mbaya zaidi katika maeneo mengi ya mitaa ya mji pembezoni kuna wateja wengi sana waliofanya kuunganisha waya kwenye majengo yao kwa lengo la kulipia shilingi 27,000 lakini wameshindwa kwa kuwa hawana uwezo huo

wa kulipia gharama ya shilingi 320,000. Kwa hiyo, Serikali iangalie namna ya kuwaunganishia huduma ya umeme.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali; Serikali yetu iangalie kwa kina suala la kuunganisha umeme kwa shilingi 27,000 katika maeneo ya mitaa ya miji yenye sura ya vijiji ili kuwezesha wananchi hao wenye uhitaji mkubwa kupata huduma hiyo muhimu. Serikali iangalie upelekaji wa umeme kwenye vitongoji kwa kuangalia vipaumbele maeneo ya taasisi za Serikali, binafsi, migodi ya madini na makazi mengi ya wananchi ili kutumia fedha kidogo kunufaisha watumiaji wengi zaidi. Kwa kuwa maeneo ya vijijini majengo mengi yako mbali mbali Serikali iangalie kutafuta kile chombo cha Umeme Tayari (UMETA) ili kuwapatia wananchi hao ambao hatutaweza kuwaunganishia kwa muda wa miaka mitano ijayo kutokana na umbali kati ya makazi na makazi mengine.

Aidha, Serikali ijitahidi sana kutoa fedha za bajeti ya Wizara hii kama ilivyoomba kwenye bajeti hii ili kufanikisha utekelezaji wa vipaumbele vyote vilivyoainishwa kwenye mapendekezo ya Wizara na maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ili kujibu kiu ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika muhtasari wa utambulisho wako wa wakuu wa taasisi zilizo chini ya wizara hii kuna nafasi nyingi za watendaji wakuu zinazokaimiwa, hivyo basi tunaiomba Serikali nafasi hizo zijazwe na watendaji wenye sifa stahiki ili kuleta ufanisi wenye tija kwa manufaa mapana ya Taifa letu.

Mwisho, naomba nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri na watendaji wakuu wa Wizara yake kwa kutupatia mitungi 100 ya gesi ambayo itafanikisha kampeni ya kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na kupunguza athari ya mabadiliko ya tabianchi, hongera Mheshimiwa Waziri ubarikiwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na naomba kuwasilisha.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi za pekee kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiangalia kwa jicho la kipekee Wizara hii na kuisaidia hasa katika miradi ya kipaumbele, *LNG, Mwalimu Nyerere Hydro Power* na mengineyo. Pongezi kwa Wizara, Waziri Mheshimiwa January Makamba, Naibu Waziri Wakili Mheshimiwa Stephen Byabyato, Katibu Mkuu *Engineer* Mramba, Naibu Katibu Mkuu Bwana Mbutuka pamoja na watendaji wakuu wote wa mashirika na taasisi mbalimbali bila kusahau watumishi wenzangu kwa kazi kubwa na nzuri inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, maombi; kwanza pamoja na shukrani za kutuongezea umeme katika vitongoji *(Underline T/F)* jambo ambalo litaongeza ustawi, ubunifu na uchumi kwa ujumla. Pamoja na shukrani hizo nina maombi rasmi ya kupeleka umeme katika vitongoji viwili vilivyopo mpakani na nchi ya Msumbiji. Ni muhimu kwa ajili ya usalama, ni muhimu kwa ajili ya uchumi kwani maeneo hayo yana dhahabu na pia ni *centers* za kibiashara. Vitongoji hivyo ni Nindi na Ngeapori. Kwa kuwa Wizara ya Nishati ni sikivu, basi naomba mnisikilize katika ombi langu hili la kuhakikisha kuwa maeneo haya ya mpakani yanasaidiwa.

Pili, napongeza mradi wa nishati safi ya kupikia. Nashauri pia kuwepo na mradi maalum wa ku-*supply* mitungi ya kilo 30 katika vituo vya afya na zahanati japo tutaanza na michache tuliyopewa kwa ajili ya uhamasishaji. Nawatakia utekelezaji wenye mafanikio.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kuiwezesha Wizara hii kuipatia fedha kuweza kupata kuendeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopo kwenye Wizara hii. Nampongeza sana sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu bila kumsahau Naibu Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu kwa leo sina zaidi ya kuipongeza Wizara hii. Ukiangalia tulikotoka na tulipofikia Serikali

imepiga hatua kubwa sana. Nilikuwa na maneno mengi siku za nyuma lakini sasa sina maneno zaidi ya kupongeza. Napongeza pia kuja na mkakati wa nishati bora ya kupikia, kweli ni ukombozi kwa mwanamke, shukrani kwako Mheshimiwa Waziri na timu yako yote kwa jambo kubwa mlilofanya la kuwajali wakina mama wa Tanzania, mbarikiwe sana.

Mheshimiwa Spika, ombi langu naomba mradi wa usambazaji wa gesi asilia utengewe fedha ya kutosha, gesi ifike Mbagala, Tandale, Gongo la Mboto na maeneo ya pembezoni. Nawashukuru sana sana na kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yako, endeleeni hivyo na Mungu atasimama na ninyi.

**MHE. TUMAINI B. MAGESSA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi kubwa inayoendelea nchini ikiwemo jimbo langu pendwa la Busanda mkoani Geita, mambo kadhaa naomba Wizara iyafanyie kazi; moja, mkandarasi jimboni Busanda aongeze kasi. *REA* na Geita *Nyakanazi Projects.*

Pili, transfoma kwenye maeneo ya wachimbaji wadogo zibadilishwe kwa kuweka zenye uwezo mkubwa, mfano Kijiji cha Nyakagwe na taasisi za umma ziwekewe umeme, kwa mfano shule, zahanati na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ahadi za Waziri mwaka jana mwezi Julai, 2022 jimboni Busanda zitekelezwe, kama vile *solar panel* katika Zahanati ya Shilungule Kata ya Busanda, taa za barabarani Mji Mdogo wa Katoro (Kata ya Katoro, Kata ya Ludete na Nyamigota).

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi na mimi niweze kutoa mchango katka Wizara hii ya Nishati na awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mungu kwa baraka na neema zake na kwa kunijalia uzima na afya njema. Niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake imara na kazi nzuri anayoendelea kuifanya ya kuleta mabadiliko makubwa katika Taifa letu. Nitumie nafasi hii

kumpongeza sana Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Makamba, Naibu wake Mheshimiwa Stephen Byabato na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa ya kuhakikisha nchi yetu inapata nishati ya kutosha, hongereni sana! Napenda kuwatia moyo endeleeni kuchapa kazi na sisi tupo nyuma yenu.

Mheshimiwa Spika, nitachangia maeneo yafuatayo; nianze na Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, niipongeze sana Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi imara wa Jemedari Mheshimiwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan kwa jitihada kubwa za kuendelea kutekeleza mradi huu kwa weledi mkubwa na kuhakikisha unakamilika kwa malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameonesha nia ya Serikali ya kukamilisha mradi kwa sasa mradi huu umefikia 87%; ni jambo kubwa na la kujivunia uzinduzi wa kujaza maji kwenye mradi huu wa Bwawa la Mwalimu Nyerere uliofanywa na Mheshimiwa Rais unatoa dira kama nchi tumeamua kuondokana na giza na kukaribisha mwanga kuliwezesha Taifa letu kupata nishati ya kutosha kwa kuwa mradi huu umegharimu fedha nyingi. Niishauri Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa mradi huu ili thamani ya fedha iweze kuonekana. Ninaamini kumalizika kwa mradi huu utakuwa ni kichocheo kikubwa cha kuleta maendeleo na kutavutia wawekezaji wa kutoka ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo ningependa kulichangia ni mradi wa *REA;* niipongeze sana Serikali kwa kuendelea kusambaza umeme kuhakikisha umeme unafika kila pembe ya nchi yetu vijijini, lakini bado jitihada kubwa zinatakiwa kufanyika ili vijiji vyote na vitongoji vyote viweze kupata nishati ya umeme. Katika mkoa wangu wa Singida kuna vijiji 441 kati ya vijiji hivyo vijiji 114 havijawashwa umeme, Ikungi vijiji 24, Iramba vijiji 10, Wilaya ya Manyoni vijiji 26, na Wilaya ya Singida 18. Niiombe Serikali iharakishe na vijiji hivi viweze kupata nishati ya umeme kwa haraka na wa kati.

Mheshimiwa Spika, niungane na Wabunge wenzangu pamoja na kwamba umeme umefika vijijini lakini bado vitongoji

vingi havijafikiwa, niishauri Serikali ije na mpango mkakati wa kuhakikisha vijiji na vitongoji vyangu vyote vya mkoa wa Singida vinapata umeme, lakini pia Serikali iangalie upya bei za umeme hususan maeneo ya Miji Midogo kwani miji yangu ya Iguguno, Nduguti, Ikungi, Ilongero na Kiomboi hali zao ni za chini na hawana uwezo wa kulipa gharama ya shilingi 320,000 ili malengo mazuri yaliyowekwa na Serikali yaweze kutimia.

Mheshimiwa Spika, suala la mwisho ambalo ningependa kulichangia ni matumizi ya gesi majumbani yaani nishati safi majumbani, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa maono makubwa ya ustawi wa jamii hususan kwa kundi la wanawake kwani ndio wahusika wanaotumia gesi hii majumbani, kwa sasa ni asilimia ndogo sana ya Watanzania wanaotumia nishati safi kwa kupikia yaani gesi, niiombe Serikali ije na kampeni kubwa ya kuelimisha jamii juu ya matumizi ya nishati safi ya gesi majumbani ili wananchi wetu wengi waweze kuachana na nishati chafu ambayo kwa kiwango kikubwa imeharibu mazingira na vyanzo vya maji na ningependa kushauri kampeni hii iitwe "Achia Shoka, Kamati Gesi," lakini niiombe sana Serikali ili maono makubwa ya Mheshimiwa Rais yaweze kutimia ni lazima gesi ipatikane kila mahala kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza watendaji wote wa *TANESCO* na *REA* wakiongozwa na *Engineer* Florence Godfrey Mwakasege Meneja wa Mkoa wangu wa Singida kwa kazi nzuri na naunga mkono hoja.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Spika, awali nichukue fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa sana anayoifanya ya kuwatumikia wananchi wa Tanzania kwa uzalendo mkubwa sana na hasa namna anavyojali na kupeleka fedha nyingi kwenye Wizara ya Nishati.

Pili, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika wa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan kugombea nafasi kubwa na nyeti ya kuwa Rais wa Bunge la *IPU*. Mimi nikuombee heri na mafanikio makubwa kwenye hatua hiyo.

Tatu, nimpongeze sana Waziri wa Nishati Mheshimiwa January Makamba kwa kazi nzuri wanayoifanya akisaidiwa na Naibu wake Mheshimiwa Stephen Byabato, hakika kazi yao ni njema, nami nawatakia heri katika kufanikisha malengo waliyoaminiwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo utajikita kwenye malalamiko au masikitiko yangu makubwa sana juu ya hali ya kusuasua ya utekelezaji wa mradi wa *REA* Mkoa wa Rukwa. Namba ya Mkataba ni *AE/008/2020 -21/HQ/W/31 – LOT 24;* Mhandisi Mshauri ni *Mercados Aries International;* msimamizi ni *TANESCO Ltd* Mkoa wa Rukwa; Mkandarasi ni *M/s JV Pomy and Qwihaya Partnership;* muda wa utekelezaji ni miezi 18; gharama za mradi ni shilingi 36,549,180,653.61; wigo wa kazi kwa mkoa mzima.

Mheshimiwa Spika, mradi huu unatekelezwa kwa ushirika wa kampuni ya Pomy na Qwihaya, kwa taarifa za nyuma Qwihaya ni kampuni ya nguzo ila kwa sasa ni mkandarasi wa umeme pia, Pomy ni mkandarasi wa umeme tangu kipindi cha nyuma hadi sasa. Mkandarasi Pomy alishawahipewa kazi ya mradi wa umeme kwa mkoa wa Tabora, alitekeleza mradi huo kwa kiwango kisichokubalika na hakumaliza, lakini adhabu na lawama ilielekezwa kwa wafanyakazi wa *TANESCO* akiwemo Meneja wa Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mwaka uliofuata baada ya kazi ya Tabora kutoisha na kuwa na mgogoro na kukawa na miradi mingine iliandaliwa na *REA* kwa mikoa mbalimbali ikiwemo Rukwa, sasa wakati wa mchakato huo watumishi wa *REA* walikataa kumpa nafasi ya kupata mradi mwingine baada ya kuona Tabora kazi iliharibika na maneno ni mengi, hata hivyo alipenya na baadae akapewa mradi kwa Mikoa ya Rukwa na Kagera zikiwa ni *lot* mbili tofauti. Kwa mkoa wa Kagera vijiji vilivyokwishawashwa umeme ni 36 kati ya vijiji 137 kwa mkoa mzima na kwa mkoa wa Rukwa ni jumla ya vijiji 49 kati ya vijiji 140 kwa kipindi chote hadi mwisho wa mwezi wa nne mwaka huu ikiwa ni miezi minne zaidi ya mkataba wake wa awali.

Mheshimiwa Spika, tangu anaanza mradi huu wa Rukwa kwa kushirikiana na Qwihaya, kumekuwa na migogoro kati yao isiyoisha na kusababisha mradi kutokwenda kwa wakati na kuwa na dalili zote za kutokamilika na huenda mgogoro ukawa ni sawa na kilichotekea Tabora. Tutambue kuwa mradi huu wa Rukwa ulianza kutekelezwa tarehe 9 Julai, 2021 na mwisho wa mradi huu ilikuwa ni tarehe 8 Januari, 2023 na alikuwa amefikia asilimia 38, *REA* wakaongeza muda wa miezi minne hadi tarehe 30 Aprili, 2023 ili kukamilisha mradi, lakini hadi mwisho wa mwezi wa nne utekelezaji wa mradi ulifikia asilimia 41. Kwa sasa *REA* wameongeza muda wa kutekeleza mradi huu hadi tarehe 31 Oktoba, 2023.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikifuatilia kwa ukaribu sana juu ya maendeleo ya mradi huu ambao unatupa wakati mgumu sana kwa wapiga kura na nimebaini mambo mengi ya kusikitisha. Pamoja na *TANESCO* kufanya vikao mbalimbali vya maendeleo ya mradi, lakini hakuna juhudi zozote za makusudi kuhakikisha mradi unakamilika, isipokuwa nilichobaini Mkandarasi Pomy (Eva Fumbuka ambaye ni Mkandarasi Mkuu) kuwa na maneno ya kufajiri bila ya utekelezaji, sababu anazotoa ni kuwa *Covid-19* imeathiri upatikanaji wa vifaa, *REA* hawawalipi na wanaibiwa vifaa *site*.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO* Rukwa kama msaidizi wa mradi wamekuwa na vikao vya kikazi na mkandarasi kuhusu mradi huu, lakini kwa upande wa mkandarasi mara nyingi wamekuwa wanahudhuria mainjinia tofauti tofauti tena wasio na mikataba ya kazi kwa mujibu wa mkataba wa mradi, kikubwa zaidi ni kuwa Meneja wa Mradi hapatikani eneo la kazi na hata vikao si mhudhuriaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuona usumbufu mkubwa sana na kelele ya wananchi kuwa kubwa niliomba mpango kazi na maelezo toka kwa Meneja wa *TANESCO* Mkoa wa Rukwa ambaye alini-*brief* kwamba kuna kikao kiliitishwa tarehe 27 Aprili, 2023 kujadili tatizo hilo la Mkoa wa Rukwa na kilifanyika Ofisi ya *REA* Makao Makuu Dodoma, na Menejimenti ya *REA* ilikuwa Dar es Salaam hivyo iliwakilishwa katika kikao. Waliohudhuria ni

wawakilishi wa Menejimenti ya *REA,* Mshauri wa Mradi, *TANESCO* Rukwa na Makao Makuu, Mkurugenzi wa Pomy na Mkurugenzi wa Qwihaya.

Mheshimiwa Spika, katika kikao hicho cha tarehe 27 Aprili, 2023 walijadili changamoto zinazopelekea mradi kusuasua, kama ifuatavyo; mgogoro wa ndani kati ya Mkurugenzi wa Pomy na Mkurugenzi wa Qwihaya katika mambo mbalimbali na kusababisha mgawanyiko wa kiutendaji kama vile suala wa wafanyakazi, usafiri *(transport),* kugawana vijiji, mvutano wa kufikisha vifaa eneo la kazi, mvutano wa kimaslahi na mvutano wa kimaamuzi.

Mheshimiwa Spika, mgongano wa kimaslahi kwa kuwa mmoja wa Wakurugenzi (Eva Fumbuka) kuwa ni Meneja wa Mradi na kusababisha kuwepo na mgongano wa kimaslahi na wa kimaamuzi, kwenye mkataba kama huu hasa kunapotokea wenye kampuni kutoelewana, Meneja wa Mradi hayupo eneo la kazi ingawa ni mmoja wa Wakurugenzi ni shida mno kupatikana hata kwa njia ya simu, na hashiriki vikao vya kazi kwa mujibu wa mkataba, pamoja na mgawanyiko uliopo wa kiutendaji bado hali ya mradi si nzuri, kubwa zaidi ni kuwa hakuna mawasiliano mazuri kati ya wafanyakazi (wahandisi) wa Pomy na Qwihaya na kupelekea *TANESCO* pia kuwa na sintofahamu ya mradi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na hali ya kubadilisha au kuacha kazi kwa wafanyakazi (wahandisi waliochini ya Pomy anaowaweka kama *joint venture)* bila taarifa yoyote na inapelekea kuharibu mwenendo wa mradi.

Mheshimiwa Spika, baada ya uwasilishaji huo na kuwa na mjadala juu ya hoja hizo, *REA* walikiri kupokea hoja hizo na kuzifanyia kazi na kwa vile Menejimenti ya *REA* iko Dar es Salaam basi watawasilisha na kuandaa ripoti ya kikao kwa yale tuliyoyajadili, lakini mpaka leo hii ni mwezi umepita hatuoni chochote kinachoendelea kwani mkandarasi alikuwa kafikia asilimia 41 ya ukamilishaji wa mradi na alikuwa ameomba haraka haraka kwa sababu ya kikao hicho nyongeza ya muda hadi mwisho wa mwezi wa nane, lakini *REA* kwa sasa wameshatoa

nyongeza ya muda hadi tarehe 31 Oktoba, 2023 hii ikiwa ni pamoja na kuongezewa kazi zaidi, nyongeza ya kazi ya kilometa mbili kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Spika, jambo la kumuongezea huyo mkandarasi muda *(extension of time)* kila wakati pamoja na ukweli wote huo wa kusuasua na usumbufu huo wote bado linatupatia jeraha kubwa Wabunge wa Mkoa wa Rukwa. Binafsi sikuona sababu tena za kumuongezea mkandarasi wa aina hii kilometa mbili nyingine kwa kila kijiji kwani ni msumbufu sana na uwezo wake ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kumshauri Mheshimiwa Waziri ambaye pia nitamuomba aje Rukwa kwa mara nyingine kujione hali hii. Kwa kifupi mkandarasi Pomy amekuwa ni tatizo kubwa kutekeleza mradi na ni dhahiri kuwa muda wa mradi utaisha hata hiyo Oktoba, 2023 aliyopewa na kazi haitakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Spika, nimuombe Mheshimiwa Waziri awaagize *REA* kuupitia mkataba wa mradi na kuona mapungufu yaliyopo na kufanya mabadiko stahiki kwa kuangalia matakwa ya kimkataba, lakini uwepo na utoshelezi wa timu iliyoko Rukwa na Kagera na yote yanayohitajika, kuwataka Wakurugenzi waajiri Meneja wa Mradi kwa upande wa Rukwa na Kagera kama mkataba unavyotaka, ikiwezekana na kwa vile Qwihaya amekwishaona ni tatizo na anachafuliwa na Pomy na anajutia kuingia kwenye hii *joint venture* na Pomy na kwa sasa kulazimika kuwa na timu yake na kutekeleza mradi, basi timu ya Qwihaya itekeleze mradi kwa Mkoa wa Rukwa na timu ya Pomy itekeleze mradi kwa Mkoa wa Kagera, kuliko ilivyo sasa maana wanalaumiana pia kuwa mmoja anamcheleweshа mwingine kuendelea na mradi kwa sababu fulani hajakamilisha kipande fulani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja na nawasilisha, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Lujwahuka Byabato, Naibu Waziri wa Nishati, mtoa hoja ajiaandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi nianze kwa kuunga mkono hoja bajeti ya Wizara ya Nishati na nikiwaomba Waheshimiwa Wabunge wote muipitishe, na ni kwa sababu hizi chache kwa muda niliopata nitakazozisema.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa *Dkt*. Samia Suluhu Hassan, namshukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais pamoja na Waziri Mkuu, na hasa kimahsusi Mheshimiwa Rais kwa kuniruhusu sasa ninasoma Bajeti ya Wizara ya Nishati au ninahudhuria au inasomwa nikiwepo kwenye Wizara hii kwa mara ya tatu; ninamshukuru sana kwa kuendelea kuniamini. Na mimi ni moja wapo kati ya wale wachache ambao wanaweza wakaeleza jitihada na mwelekeo mzuri wa Wizara hii kwa kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe na ninakupongeza kwa jitihada zako na uongozi wako mzuri nakutakia kheri katika lile ambalo wenzangu wote wamelisema. Nawashukuru sana Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, Waheshimiwa Wabunge lakini kipekee namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, January Makamba kwa malezi yake kwangu mimi kama mdogo wake lakini kwa kutuongoza vyema Wizarani mimi pamoja na wenzangu ambao tunamsaidia kazi nawapongeza pia. Mwisho lakini si kwa umuhimu, nawashukuru waajiri wangu wa Jimbo la Bukoba Mjini kwa kuendelea kuniamini na kunipa ushirikiano nikiendelea kutekeleza majukumu ya kitaifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imepokea shukurani na pongezi nyingi sana. Hapa mwanzo kabisa nieleze, shukurani hizi na pongezi hizi ni za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi ni wawakilishi, ni wajumbe na ni watenda kazi wake kwa niaba ya Watanzania; na tutaendelea kufanya kazi hii kwa sababu tunaipenda na tunaiweza na tuko tayari kuendelea kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, lakini kama raia na wananchi wa kawaida tu na mimi naomba nitoe shukurani zangu kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuamua kwa mara ya kwanza kuruhusu fedha itengwe kwa ajili ya kupeleka Gridi ya Taifa kwa Mkoa wa Kagera kwa kujenga *line* ya kutoka Benako kwenda Kyaka. Kwa hiyo na sisi watu wa Kagera tunafurahia matunda mazuri na wito wake mzuri kwa kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye hoja mbili ambazo nitamsaidia Mheshimiwa Waziri kujibu na kwa muda nitakaokuwa nao naamini nitafanikiwa. Maeneo hayo ni gharama za kuunganisha umeme lakini pia nitaenda kwenye gharama za umeme vijijini au umeme vijijini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge takribani wote wamezungumzia kuhusiana na gharama za kuunganisha umeme. Tumewasikia na tunawaelewa na tunatamani jambo hilo litokee kwa sasa, lakini si rahisi na hatuwezi kulifanya kwa haraka sana namna hiyo. Sababu ni kwamba tunahitaji fedha zaidi.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuunganisha umeme halisi ni wastani wa shilingi 700,000 kwa wale ambao wapo ndani ya mita 30. Kwa hiyo, pale ambapo tunaunganisha umeme kwa shilingi 320,000 kwa mjini maana yake Serikali ya Awamu ya Sita imeweka ruzuku ya takribani shilingi 380,000 ili iweze kuunganisha umeme. Kwa wenzetu wa vijijini ambao wanaunganisha kwa 27,000 imewekwa takribani ruzuku ya shilingi 670,000 ili waweze kuunganisha umeme.

Mheshimiwa Spika, gharama za sasa zina ruzuku kubwa ya namna hiyo. Sasa, ruzuku maana yake ni fedha ambayo inalipwa na mwingine ili mwingine apate huduma. Kwa hiyo, *it's either* ilipwe na mwananchi au ilipwe na *TANESCO* au ilipwe na Serikali. Tulivyofanya hesabu baada ya mabadiliko ya kurudi kwenye bei ambazo tulikuwa tukizitumia zamani Januari mwaka jana, *TANESCO* ilibaini ongezeko la shilingi bilioni sita katika makusanyo ya gharama za kuunganisha. Kwa maana hiyo kwa mwezi *TANESCO* inahitaji bilioni sita ili kuunganisha watu kwa gharama

ya shilingi 27,000 kwa mjini na inahitaji takribani bilioni kama saba kuunganishwa wale wa vijijini. Kwa maana nyingine tukitaka kuunganisha Watanzania wote wanaohitaji umeme tunahitaji takribani bilioni 13 ya ruzuku ili kuweza kuunganisha kwa shilingi 27,000.

Mheshimiwa Spika, ukiipiga hii kwa mwaka ni takribani bilioni 156. Sasa jambo hili tunalielewa na tunatamani litokee lakini sasa bilioni 156 inatoka wapi? Tunawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge mturuhusu tuendeelee kuchakata tuone namna ya kujibana hapa na pale ili fedha hii ya ruzuku ipatikane, gharama hizi ziweze kupunguzwa kwa wananchi ili tuweze kupata huduma hiyo vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kabisa Mheshimiwa Rais anayonia, na pale ambapo tumekuwa tukikabwa sana amefanya. Alitoa bilioni 100 kuweka ruzuku kwenye mafuta na amekuwa akitoa ruzuku kwenye mbolea na kwenye maeneo mengine. Tunaamini kwa kujibana na kwa kuweka viapumbele mbele hili nalo utalifanikisha. Kwa sasa shughuli ya kubaini maeneo ni yapi kwa uwezo wa wananchi kwa uwezo wa kiuchumi linaendelea, na litakapokamilika tutakuja kuliunganisha pamoja na hili ili sasa tuweze kufikia sehemu ambapo tutaunganisha wananchi wetu kwa gharama nafuu. Ni jambo zuri lenye kuleta kheri lakini linahitaji mjadala mkubwa Serikalini kuweza kubaini sehemu ya kupata fedha hiyo, na mimi naamini kwamba tutalifanikisha.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye jambo la pili la umeme vijijini. Waheshimiwa Wabunge takribani wote waliposimama wamelizungumzia jambo hili, na ni jambo la muhimu kweli na katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya uchaguzi imeelekeza ifikapo 2025 vijiji vyote viwe vina umeme. Sisi hatuna wasiwasi hata kidogo, wala 2025 hatutafika jukumu hili na sharti hili la ilani litakuwa limekamilika. Mwaka huu tutahakikisha kwamba vijiji vyote vinapata umeme. Kwa sasa *overall* tumefikia asilimia 72 ya Mradi wa *REA III Round II.* Yapo maeneo ambapo tumefanya vizuri sana. *Lot* namba 30 ya Simiyu yenye Wilaya ya Maswa na Meatu tumemaliza asilimia 100. *Lot* namba 18 ya Morogoro vijijini

asilimia 100, *lot* namba 23 ya Pwani wilaya zote asilimia 100. *Lot* namba 38 ya Tanga, Wilaya ya Kilindi, asilimia 100, *lot* namba 14 ya Mkoa wa Mara, na wamesema hapa, asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini tunakiri kwamba bado kuna sehemu hatujafanya vizuri. Na mpaka sasa baada ya jitihada zilizoanza Januari mwaka huu tumebakiza Lot nne ambazo tunaona hatukaa sawa. *Lot* namba moja, *lot* namba 27, *lot* namba 39 na *lot* namba 25. Waheshimiwa Wabunge humu wamesema, tunaomba mtuamini, tumeweka mikakati, tuemeweka jitihada na tunakimbizana na wakandarasi hawa, tutafanikisha. Lakini si maneno tu, Waheshimiwa humu wengine wamesema tufungue *LC, LC* tayari zimefunguliwa na wale ambao wanakidhi vigezo watachukua pesa ili waweze kupata vifaa kwa wakati mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongeza wasimamizi. Waheshimiwa Wabunge wote mnafahamu vijana wameripoti kwenye majimbo yetu kwa ajili ya kuendelea kutoa taarifa za siku hadi siku ili mradi uweze kusimamiwa vizuri. Tumeongeza wahandisi wa *REA* kwenye *level* za mikoa, tumeongeza *speed* kwenye taratibu za malipo, maana malipo yanakwenda *REA,* yanakwenda *TANESCO* na yanakwenda Wizara ya Fedha; yalikuwa yanachukua muda. Tume-*develop mechanism* ambayo itatufikisha kwa haraka mwishoni.

Mheshimiwa Spika, lakini hatujaishia hapo tu, tumeweka *mechanism* mpya ya miradi mipya inayokuja ili tusiingie kwenye matatizo ambayo tumekutana nayo. Moja wapo ya sharti ni kwamba kama hujafikia asilimia fulani za mradi mwingine hauto *qualify* kupata mradi mpya, na hii tayari tumeanza kuitekeleza; na katika hili hatutazamani usoni, tunahakikisha kwamba tunalisimamia vyema.

Mheshimiwa Spika, kuna mkandarasi ambaye alitajwa hadharani si vyema tukaliacha hivi hivi. Mkandarasi anayefanya kazi ya Tanga kwenye maeneo kadhaa lakini ana kazi pia Mkoa wa Kahama. Mkandarasi huyu hakufanya vizuri Tanga, anaitwa *Tontan*. Kwa upande wa Kahama Mheshimiwa Iddi na

Mheshimiwa Cherehani wametoa Ushahidi; anajitahidi sana kufanya kazi nzuri kwenye eneo la Kahama.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa Korogwe tuna shughulika naye na hatua zimeshaanza kuchukuliwa *liquidated damage* tumeshaanza kukata. Kwa hiyo, tunaichukua *Lot* ya Korogwe kama ameshindwa kufanya kazi tunashughulika naye huko. *Lot* ya Kahama ambayo anafanya kazi vizuri kwa kujitahidi tunaendelea kumtazama kwa karibu. Lakini ilisemwa kwamba amepata kazi nyingine *TANESCO;* ni kweli amepata kazi ya kujenga *line* ya kutoka Ubungo kwenda Ununio, na alipata kazi kabla hatujajua haya mengine. Alikuwa ameonekana atapata kazi nyingine mbili lakini zimesitishwa kwa sababu alionekana atatusumbua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini aliwahi kufanya kazi nyingine, aliwahi kujenga *line* ya Dege kuja mpaka Kurasini, aliifanya vizuri. Kwa hiyo, matatizo aliyoyapata sisi hatuyatazami kama ni matatizo ya jumla, tunatazama kwenye mradi husika. Kwenye mradi wa Korogwe tutashughulika naye kisawasawa mpaka tupate haki yetu na yeye apate haki yake. Huko kwingine tutaendelea kuhakikisha kazi inafanyika vizuri. Hii *Lot* ya kutoka ubungo kwenda Ununio ameshaleta *bank guarantee*. Akianza kusuasua tunakula kichwa kwa sababu kazi yetu ni kuhakikisha kwamba huduma inawafaikia wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi niombe mtupe nafasi tena tuendelee kusimamiana na hawa wenzetu. Umeme vijijini ni siasa kwa kila mtu lakini ni huduma kwa wananchi, na tutahakikisha tunaweza kulifanya hili vizuri. Lakini pia pale ambapo mkandarasi amesua sua leo tusifute na *record* zake za jana na juzi, huenda ikawa watumishi labda walikuwa wamepitia njia ambazo si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alisema mkandarasi aliyefilisika kwenye Kinyerezi *I Extension,* mkandarasi huyo huyo alitujengea Mradi wa Kinyerezi *I* vizuri kabisa na ukakamilika, unafanya kazi mpaka leo. Mkandarasi huyo huyo alitujengea mradi wa Kinyerezi *II* vizuri kabisa umekamilika mpaka leo unafanya kazi kwa zaidi ya dola milioni 300. Alipoingia kwenye Kinyerezi *I Extension* yaliyomkuta

yalimkuta akapata shida. Isionekana tulikuwa na mkandarasi wa hovyo na ambaye hafai alifanya kazi nyingine lakini huko tupaache Kinyerezi *I Extension* imekamilika na *Mega Watt* 135 zimeshaingia mradi unafanya kazi vizuri na umeziba ma-*gap* ambayo tulikuwa tuna matatizo katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, eneo la umeme wa vitongojini nitamuachia Mheshimiwa Waziri aje aliseme kwa upana wake kwa sababu lina kishindo kikubwa. Kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri tulisema nia ya kuendeleza Wizara ni kuifanya sekta ya nishati kushamirisha shughuli za biashara, uzalishaji na maendeleo ya sekta nyingine zote za kijamii na kiuchumi, ndivyo tunavyoiona Wizara ya Nishati. Na jukumu hilo kama nilivyotangulia kusema kazi hii sisi tunaipenda na tunaiweza. Tunaomba muendelee kutuamini na mtupe nafasi ya kufanya hii kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, waipitishe bajeti hii ambayo kama ilivyosemwa na wenzangu ina *component* kubwa ya miradi, ina *component* ndogo sana ya *OC* na kwa ajili ya mambo mengine. Tukishafanikiwa hili tunaamini baada ya bajeti kupitishwa shughuli itaanza kwa kasi. Ari na moyo tunao na tunaweza kufanya kazi hii kama mnavyotuona na jinsi mlivyotupongeza na kutupa hamasa na shukurani ambazo nimesema zote zielekezwe kwenye mwenye nazo, Mheshimiwa Rais. Tunawashukuru sana, na kwa nyuso navyoziona naamini shughuli ilishakamilika na namuomba Mwenyezi Mungu aibariki iwe hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo ninaomba kuunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu awabariki wote, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimwite sasa Mheshimiwa January Yusuf Makamba, Mtoa hoja ya Wizara yake ya Nishati aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, inaelekea Waheshimiwa Wabunge wanataka twende kwenye Kamati ya

Matumizi moja kwa moja, lakini kwa kuwa kuna masuala waliuliza na waliyachangia basi kwa heshima na taadhima na kwa kibali chako ningependa kujielekeza kwenye baadhi ya hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani kubwa sana kwako na shukrani kubwa na nyingi kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii kwa kuzungumza na kwa maandishi. Tumefarijika sana kwa sababu michango ni mizuri sana, michango iliyotupa elimu kubwa, iliyotuhamasisha, iliyotutia moyo, iliyotuelimisha, iliyotufikirisha. Kwa hiyo tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kweli kwa kuitendea haki hoja yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia ni wengi, wamezidi 70, nadhani ni rekodi katika hoja za hivi karibuni, na hatutaweza katika muda huu tulionao kutoa majibu yote na kwa wote; ila tumefanya jambo kidogo tofauti kwamba mkienda kwenye visimbuzi vyenu tayari hivi ninavyozungumza majibu tumeshayatoa kwa Waheshimiwa Wabunge wote. Nimshukuru pia Naibu Waziri naye kwa kunisaidia na kusaidia kujibu baadhi ya hoja vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nijielekeze kwenye baadhi ya mambo yaliyozungumzwa na Wabunge wengi kwa makundi. Kwanza ni kuhusu suala la *LNG*. Hili ni jambo kubwa sana, na sisi tumefarijika kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumzia. Katika bajeti yetu hii, kutokana na nchi yetu kuingia kwenye mradi huu Bajeti ya Wizara ya Nishati inatazamwa na Dunia ya Nishati. Kwa sababu Mradi wa *LNG Tanzania* ni mradi wa usalama wa nishati duniani; ni *Global Energy Security Project*. Kwa sababu hii gesi inapelekwa kwenye masoko ya nchi kubwa zenye viwanda zilizoendelea zenye njaa ya nishati, kwa hiyo uhakika wa upatikanaji wa gesi hii ni suala linalotazamwa na wengi. Kwa hiyo wenzetu dunia nzima walikuwa wanatazama Tanzania tunasemaje kuhusu huu mradi?

Mheshimiwa Spika, lakini siyo bajeti yetu tu, hata michango ya Wabunge ilikuwa na yenyewe inatazamwa. Je, hao wawakilishi wa wananchi na wenyewe wanasemaje? Huu mradi

wanauchukuliaje? Naomba niwape mrejesho kwamba wenzetu wamefarijika sana kwamba kuna hamasa kubwa, kuna uelewa mkubwa na kuna hamu kubwa miongoni mwa viongozi wa nchi yetu, kwa sababu ninyi ndio viongozi, kuhusu mradi huu. Kwa hiyo tumefarijika sana kwa mchango wenu na umetupa nguvu sisi tunaosimamia mradi huu kwamba si mnaona? Mradi huu una *support* ya wananchi kupitia wawakilishi wao. Kwa hiyo tunapenda niwashukuru sana kwa hilo na tutapenda pia kuwaomba katika hatua zinazokuja ikiwemo sheria mahususi ya mradi huu; kwa sababu kama nilivyoeleza kwenye hotuba yetu tutatengeneza *project law* ya *LNG* tutaleta Bungeni hapa sheria mahususi ya mradi ili muone vitu gani vitasaidia kuendesha mradi huu ili uwe na tija na manufaa na maslahi kwa nchi. Kwa hiyo Bunge litakuwa na nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba pia tutakapokuja wakati huo pia moyo mliouonyesha katika hatua hii pia muendelee kwa sababu wataendelea kutazama. Kwa hiyo nawashukuru sana sisi tumeyapokea ushauri mlioutoa kwamba tuharakishe utekelezaji, na tutayafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni suala la kukatika katika kwa umeme. Hili Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza, na labda niseme tu kwamba suala hili ni changamoto ya muda mrefu. Kwenye bajeti yetu lilizungumzwa pia na siku za nyuma pia limezungumzwa. Tunafarijika kwamba sasa hivi ni kwa maeneo mahususi. Kwenye bajeti ya mwaka jana ni Wabunge wengi zaidi lilikuwa linawagusa katika maeneo yao, lakini kadiri muda unavyoenda maeneo yanapungua, hatusemi tumemaliza lakini maeneo yanapungua.

Mheshimiwa Spika, hili suala ni la kihistoria, labda nichukue muda kulieleza kidogo. Utakumbuka kwenye miaka ya 1990 nchi yetu iliingia kwenye hamu ya ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Na ikawa ikiamuliwa kwamba shirika libinafsishwe linawekwa kwenye kundi la makampuni yanaitwa *specified* na linakuwa *gazetted* kabisa. Na ikishaamuliwa hivyo, Serikali inasimamisha uwekezaji katika shirika hilo na inasimamisha hata ajira. Kwa hiyo moja ya shirika mwaka nadhani 1993/1994 lililowekwa kwenye

kundi la ubinafsishaji ilikuwa ni *TANESCO* miaka hiyo. Baada ya uamuzi ule kufanyika ajira zilisimama, uzalishaji wa umeme ulisimama, ujenzi wa miundombinu ulisimama, ukarabati wa miundombinu ulisimama kwa sababu tulikuwa tunasema tutalibinafsisha.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya uamuzi wa kulibinafsisha ukachukua muda mrefu, takribani miaka 10 haukufanyika. Baadaye uamuzi ulipofanyika ulikuwa hatubinafsishi tena, libaki shirika la umma. Lakini katika kipindi ambacho uamuzi huo ulikuwa unatafakariwa, ni kipindi ambapo uchumi ulikuwa una kua kwa kasi sana, idadi ya watu inaongezeka, tumefungua uchumi wetu kwenye dunia na wawekezaji wanakuja. Kwa hiyo katika kipindi ambacho uzalishaji wa umeme umesimama, ujenzi wa miundombinu umesimama ndipo ambapo nchi ilikuwa inaenda mbele kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ile historia ya miaka 10 ya kutokuwa na ukarabati, uwekezaji wala uzalishaji malipo yake ndiyo tunayalipa sasa. Ndiyo, kwa hiyo lazima historia tuwe nayo sahihi. Sasa kwenye umeme, kama nilivyosema, kuna uzalishaji wa umeme, kuna usafirishaji kwenye yale mawaya makubwa na kuna usambazaji. Hivi vitu vyote lazima viwe sawa ili uweze kupata umeme wa uhakika. Tukiwa wakweli wa nafsi zetu, na kwa sababu sisi ni viongozi tuna wajibu wa kusema ukweli, hatukuwa na umeme wa kutosha. Nchi yetu yenye watu milioni 60, sisi tunao safiri duniani ukiwa Waziri wa Nishati swali la kwanza vipi mna megawati ngapi na kule wanatumia *gigawatt,* 1,800 wanasema *1.8 gigawatt.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nchi yetu tunasema tuna umeme *1.8 gigawatt.* Mimi huwa nawaambia watu wangu tusitumie neno *gigawatt,* tutumie neno *megawatt* angalau zionekane nyingi, 1,800. Kwa sababu kwenye nchi nyingine umeme wa nchi yetu 1.8 *gigawatt* au *megawatt* 1,800 ni umeme wa sehemu kama Kisesa, mtaa sio umeme wa nchi. Sasa kwenye nchi ambayo ina malengo makubwa ya maendeleo kama yetu, watu wanaongezeka kwa kiasi kikubwa, shughuli zinapanuka, lazima tuondoke katika hali hii. Na katika uamuzi wa kijasiri

uliowahi kufanyika katika nchi hii ni uamuzi uliofanywa na Rais wa Awamu ya Tano ya kujenga Bwawa la Julius Nyerere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ule utatupunguzia aibu ya kusema 1.8 *gigawatt.* Na ilani yetu imetuelekeza kwamba ifikapo 2025 walau tuwe tumefika 5,000; 5.0 *gigawatt.* Bado, bado. Na sisi sasa hivi tunadhani tuna umeme wa kutosha, lakini ni kwa sababu; ninaenda kwenye jambo la pili la usafirishaji na usambazaji; umeme huu tunaona unatosha kwa sababu haujawafikia wote wanaouhitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo tunaingia jambo la pili, la miundombinu. Leo hii tukiweza kutimiza mahitaji ya Mheshimiwa Dotto Biteko na wamezungumza Wabunge wa Geita, Wabunge wa Kahama rafiki zangu Kassim na Cherehani na Dada Rose pale. Tukiweza kuipa migodi yote inayotumia *diesel* leo umeme ni *megawatt* 1,200 kwa mpigo. Naomba nirudie. Tukiweza kuipa migodi yote nchini sasa hivi inayotumia *diesel* tukiweza kuipa umeme itatumia umeme sawa na umeme wote tulionao siku ya leo, mwaka huu katika kipindi hiki. Maana yake ni kwamba bado hatujawafikia Watanzania wengi wanaohitaji umeme, acha kwenye nyumba hata kwenye maeneo ya kilimo, uzalishaji na migodi.

Mheshimiwa Spika, usambazaji; umeme unaenda kwenye mitaa yetu na kwenye wilaya zetu. Na kitaalamu umeme wa usafirishaji una nyaya zake, umeme wa usamabzaji una nyaya zake. Nyaya za umeme wa usambazaji ni za bei nafuu, za usafirishaji ni za bei ghali. Sasa ili huko nyuma tuweze kupeleka umeme kila mahali, tukawa tunasafirisha umeme kwa njia za usambazaji. Matokeo yake Mheshimiwa Simbachawene pale, *line* inayotoka hapa Zuzu inaenda Mpwapwa, inaenda Kongwa, inatokea Gairo inaenda Kiteto ni *line* hiyo hiyo moja kilometa zaidi ya 1,000 wakati ilipaswa kwenda kilometa 100 tu.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba nguzo ikianguka hapo Mvumi huko kwenda umeme unakatika mpaka Kiteto. Sasa ndiyo changamoto tuliyonayo na ndio ukweli wenyewe na ni maeneo mengi. Tabora pale mji mzima wa Tabora una waya

mmoja tu mrefu, mpaka Urambo, ulikuwa ni waya huo huo mmoja kilometa 1,200. Sasa Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita alivyoingia madarakani akatupa hii kazi umeme ukawa unakatika tukaanza kunyoshewa vidole, ni yule Bwana Kipara pale ndiye anakata umeme. Ni Bwana Maharage pale ndiyo anakata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tulichofanya tukakaa tukajifungia na wataalamu wale mnaowaona tukawaambia hebu tuambieni ukweli. Maana kulikuwa na dhana kwamba ni hujuma. Mimi siamini kabisa mtu ameajiriwa *TANESCO* ahujumu kukata umeme kuzima umeme kwa sababu ndiyo maisha yake. Ndipo wakasema wakuu, unajua Serikali tunaitana wakuu. Wakasema mkuu, nikwaambia hebu acheni mambo ya mkuu, hebu semeni tu kinachoendelea. Ndipo tukapewa uchambuzi wa hali ilivyo, na sisi tukapendekeza mpango mahususi mkubwa, unaitwa *Grid Imara,* wa gharama kubwa sana wa kubadilisha nyaya za zamani kuweka nyaya nene zaidi. Pia kuvalisha nguo zile nyaya, kubadilisha *transformer,* kujenga na *line* nyingine mpya. Tukauita Mradi wa *Grid* Imara wa trilioni 4.4 tukaenda kwa kiongozi wetu Mheshimiwa Rais tukamuwasilishia ule mpango akasema sawa nitawaanzia na shilingi bilioni 500, tukaja Bungeni mkatuidhinishia. Tukaenda tukaanza awamu ya kwanza tukatafuta wakandarasi 26 sasa hivi miradi inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,Hii ni safari. Sitaki kuwadanganya kwamba umeme utaacha kukatika mwakani au mwaka unaofuatia. Ambacho nawaahidi tumeweka jitihada kila mwaka tutakuwa tunapunguza changamoto hii. Mpaka mpango huu ukamilike. Hakuna watu wanaoumia kunapokuwa na changamoto ya kukatika kwa umeme kama sisi tunaosimamia sekta kama wataalamu kule *TANESCO.* Kwa hiyo tunafahamu madhara kwa uchumi, kwa vifaa vyetu kutokana na kukatika kwa umeme ila naomba muiamini Serikali. Na mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, mara moja alielewa, mara moja aliridhia, mara moja aliidhinisha na Bunge hili tunalishukuru kwamba mara moja na nyie mlielewa na mara moja mliridhia na mkaidhisha ule mpango.

Mheshimiwa Spika, tunaomba sasa, mwaka huu tumeomba zaidi shilingi bilioni 400 zaidi kwa kuendelea na ule mpango. Kwa hiyo sasa sisi hapa nchini ili umeme uwe imara walau kila wilaya iwe na kituo cha kupozea umeme *(substation)*. Ninyi mnatoka huko wilayani, nchi nzima kuna vituo 46 tu, wilaya 46 tu ndizo zina vituo katika wilaya zetu zote. Tumekuja na mpango mwingine wa kujenga *substation* kwenye kila wilaya.

Mheshimiwa Spika, safari ya kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme itakuwa ni safari siyo tukio, ni safari. Tunachoomba ni subira na uvumilivu; na wakati mwingine tupeane nafasi.

Mheshimiwa Spika, siku moja hapa umeme umekatika Bungeni kulitokea hitilafu, ghafla bana fukuza Waziri, fukuza *TANESCO*. Kumbe kuja kuchunguza wala; umeme umekatika kwenye uwanja wa mpira, fukuza Waziri, fukuza *TANESCO,* kumbe ni mambo mengine. Kukiwa na mkutano watu wakichezea chezea huko umeme ukikatika fukuza. Jamani si wakati wote ni *TANESCO* na si wakati wote ni Wizara. Sisi tutachukua wajibu wetu pale linapotokea na moja ya hatua ni kuimarisha shirika lenyewe linalofanya kazi hii ili liwe na weledi. Na mmeona mliotembelea pale mabadiliko makubwa yanayoendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye hili la kukatika kwa umeme tutapunguza, lakini sitaki kuwaambia kwamba kesho itaisha. Wote tutawapa na tutaweka *dash board* muingie muone maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa *Grid* Imara. Tutawapa *link* muone wapi tumebadilisha, wapi hali imebadilika, wapi tatizo lipo ili muweze na ninyi kufuatilia, ili na nyie mtusaidie kusema kwa wananchi. Hilo tutalifanya katika kipindi cha miezi miwili ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa Julius Nyerere ni mradi wa kihistoria kama nilivyoeleza na umezungumzwa sana hapa na tunawashukuru sana kwa kuunga mkono. Tulileta ile teknolojia ili muone maendeleo kwa sababu walau inaitwa *virtual reality* yaani unakaribiana na ukweli wenyewe. Naomba nitoe tangazo hapa kwenye Bunge kwa ridhaa yako, sisi tuko tayari, si tu kusafiri kutokea hapa Bungeni kwa kuvaa miwani, kwa ratiba

Mheshimiwa Spika atakayoweka, kwa *logistics* zitakavyokuwa tuko tayari kuwasafirisha Waheshimiwa Wabunge wote kwenda kwenye mradi mkauone wenyewe wakati wowote ili tusiishie hapa; na hilo tutaongea na Ofisi ya Mheshimiwa Spika ili tuweze kuliweka vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kuna suala la mradi umechelewa, mradi umechelewa, mradi umechelewa, kwa nini hatujamkata mkandarasi limezungumzwa. Miradi hii ya kuzalisha umeme kwa kutumia maji ina ukubwa tofauti. Huu ni mradi mkubwa katika ukanda huu. Mkataba wa kwanza ulikuwa miaka mitatu ya ujenzi lakini ukiangalia miradi mingine, ukienda Kihansi, Mtera, Hale, *Pangani Falls* hamna mradi kati ya hiyo na ni midogo megawati 80, megawati 200, 180 hakuna uliojengwa chini ya miaka mitano. Naomba nirudie, mradi wa megawati 80 hapa Mtera umejengwa miaka sita.

Mheshimiwa Spika, mradi wa Julius Nyerere sisi tulipanga kuujenga; fikiria ni megawati 2,000; tulipanga kuujenga kwa miaka mitatu. Sasa *CAG* alitusema kwamba hakukuwa na ukadiriaji sahihi wa muda wa ujenzi wa mradi, na alikuwa sahihi kabisa. Hakuna mahali popote unaweza kujenga megawati 2,115 kwa miaka mtatu, hakuna. Kwa hiyo ndio ukweli. Mchungu lakini ndiyo ukweli. Sasa muda umeongezeka, muda ukiongezeka mkataba uliowekwa una namna za kushughulikia mambo hayo ndani ya mkataba. Hadi leo hatujavunja mkataba kwa sababu hata hiyo nyongeza imeelezewa ndani ya mkataba itafanyikaje.

Mheshimiwa Spika, kuna habari kwamba watu wanakwenda mahakamani si kweli. Na kuhusu malipo kwa hiyo nyongeza. Kuna hoja hapa kwa nini hamumkati mkandarasi kwa kupitisha muda. Hiyo dhana ya kumkata siyo sahihi kwa sababu fedha tunazo sisi si kwamba anazo yeye, tunazo sisi. Sasa haki ya kubaki nazo hatujaipoteza. Naomba nirudie, haki ya kubaki nazo hatujaipoteza. Ilikuwa ni suala la busara, tu kwamba je, ile Juni mwaka jana mradi ukiwa asilimia 60 ndipo ufanye fujo wakati ule? Au utumie busara usiipoteze haki yako mradi usonge mbele hadi huko mbele? Kwa sababu hupotezi ile haki mpaka siku ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna baadhi ya watu hapa wanasema hakuna kamata hao, zuia, zima, ondoa, leta mwingine. Mnajua *mobilization* ya mkandarasi mpya pale inavyokuwa?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo wakati mwingine maarifa, weledi, mkakati unahitajika kusimamia hii miradi mikubwa. Mradi leo uko asilimia 87 haikutokea kwa ajali imetokea kwa maarifa, kwa weredi na kwa mkakati, hakuna hata siku moja kazi imesimama pale na mambo yanaendelea. Kwa sababu tumeamua kutofautisha, kushughulikia mikataba na kusimamia mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mradi huu pia ulianza pia kama sehemu ya mahusiano kati ya nchi na nchi, marais wawili walizungumza, kwa sababu ni mradi mkubwa. Mkandarasi kutoka Misri, haiwezekani mkandarasi kutoka Misri wa mradi mkubwa kama kuu viongozi wasiwe na mahusiano katika kuuzungumzia. Kwa hiyo pia mradi huu unalelewa na mahusiano mazuri yaliyopo kati ya nchi zetu mbili Misri na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu mimi nimeingia katika nafasi hii Mheshimiwa Rais wetu amekutana na Rais wa Misri mara tatu na mimi nikiwepo. Mheshimiwa Rais wetu ametuma Mjumbe maalum Misri kwa barua maalum kuhusu mradi na Rais wa Misri ametuma Mjumbe maalum hapa kuhusu mradi huu. Kwa hiyo mradi huu pia unalelewa na mahusiano kati ya nchi zetu mbili, hauwezi kufeli. Na katika kushughulikia mradi huu lazima tulizingatie na hilo, hatuwezi kuliacha; ndiyo maana hamna mambo ya Mahakamani haitotokea. Juzi tu tumepokea mjumbe maalum pia mwingine wa Rais wa Misri kuhusu mradi huu. Kwa hiyo naomba mtuamini, *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeweka sayansi ya usimamizi wa miradi, tunaizingatia, tumefika pazuri sana, mradi huu utakwisha salama kwa kibali cha Mwenyezi Mungu na tutawapeleka mkaone, mtafurahi na mtapata fahari ya uwezo wa Watanzania wenzenu kufanya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo yanapaswa kutuunganisha Watanzania ni huu mradi. Hii dhana kwamba kuna watu wanataka kuhujumu, kuna watu hawautaki, kuna watu wamefanya kosa hapa, kuna watu nini na nini; mimi naomba huu mradi tusiutumie kupata sifa ya siasa kabisa. Kwamba mimi ndiyo mbabe zaidi, ndiyo naweza kuusimamia kuliko watu wote waliyopewa dhamana ya kusimamia mradi huu. Naomba siasa iwekwe pembeni na mradi huu kabisa, mradi huu ni mkubwa wa heshima na wa bei kubwa sana kwa fahari ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *CSR* imezungumzwa hapa ni sehemu ya makubaliano ya mradi huu. Tulikubaliana wakati tunausaini kwamba asilimia 3 itatumika kwa miradi ya kijamii, lakini tukimlipa kwa wakati kwa miaka miwili tutapata asilimia moja ya ziadi, kwa hiyo imekuwa asilimia 4 ambayo ni sawa na shilingi bilioni 262. Sasa zile fedha kwenye yale makubaliano kulikuwa na makubaliano zitumike wapi? elimu na afya lakini baadaye ukafanyika uamuzi kwamba hapana tujenge uwanja wa mpira na barabara.

Mheshimiwa Spika, sasa tukakorofishana na mkandarasi kwa sababu yeye alisema siyo mkataba. Kwa hiyo kile kipindi cha mabishano kilikuwa kirefu mno na hatukufikia mwisho ndiyo maana miradi hii imechelewa kwa sababu kuna sababu mbona hamjafanya? mbona mmechelewa? kwa sababu sisi wenyewe tuliamua kuamua tofauti. Kwa hiyo tukabishana tukaenda mbele, nyuma baadaye busara ikatamalaki kwamba jamani ee pia afya na elimu ni muhimu. Kwa hiyo turudi kwenye makubaliano ya awali, hapo muda ulikuwa umeisha kwenda pia vilevile.

Mheshimiwa Spika, baada ya pale sasa vikaanza vikao, na kwa sababu ni elimu na afya sisi tukatafuta vikao na wenzetu, kwamba jamani nyie sekta ya elimu, sekta ya afya vitu gani muhimu kwenu ili tuweze ku-*finance* huu mradi? Tukaletewa vyuo vya juu vya ufundi na maeneo tukaletewa na kwa sababu yalikidhi haja na kwa sababu katika vyuo hivi watasoma vijana wote wa Kitanzania kutoka kila kona ya Tanzania. Sisi suala la pahala hatukuliona ni suala kubwa, kiwe Rufiji, kiwe Dar es salaam, kiwe Morogoro kama chuo cha *UDOM* hapa kipo

Dodoma lakini asilimia ngapi ya watu wa Dodoma wanasoma hapa? Watanzania wote wanasoma pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tukaona kwamba tusiingie kwenye *changu*, *changu,* leta kwangu na nini? ila kitu ambacho tunakili ni kwamba wenzetu ambao mikoa yao, wilaya zao, maeneo yao yapo kwenye mradi wanao wajibu mahususi, wanayo majukumu mahususi. Kwa hiyo pia tutazingatia hilo vilevile. Pamoja na kwamba imeamuliwa kwamba tujenge hivi vyuo vikuu vitatu vya juu vya ufundi siyo *VETA* juu ya *VETA very technical* lakini tutafanya Morogoro, Pwani na kwingineko tutafanya vitu kwenye afya na kwenye elimu kwa sababu hatuwezi kutoka hapo. Kwa hiyo katika fedha upya tumewasikia Mheshimiwa Kalogeris tuandikieni, Waheshimiwa Pwani vilevile nimemuona Kuchauka naye anasema Liwale pia ni Rufiji sawa na yeye tumepokea, tumepokea kuhusu miradi mingine ya elimu na afya katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba hii fedha ya *CSR* imeliwa, imeibiwa si kweli, fedha ipo kwenye mkataba na ipo na tayari chuo cha kwanza Lindi tumeishaona mahala, watu wameishakwenda, watu wameishapima, michoro imeishafanywa na Mungu akijalia mwezi wa saba tutaweka jiwe la msingi pale na kazi itaanza kuonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi kama nilivyosema Mheshimiwa Rais alipokea Mjumbe maalum wa Rais wa Misri akiwa na barua maalum kutoka kwa Rais wa Misri na moja na ya mambo tuliyozungumza ni utekelezaji wa Miradi ya *CSR*. Kwa hiyo liko hata kwenye ngazi ya juu litafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la nishati ya kupikia sisi tunafarijika sana kwamba tumefanikiwa. Kama Bunge kama Serikali kupika na namna ya kupika inachukua takribani asilimia 30 ya mazungumzo ya Bajeti ya Nishati. Hiyo haijapata kutokea. Kwa sababu siku zote tukizungumza nishati, tunazungumza mafuta, umeme, gesi. Sasa ukiweza kuingiza ajenda mpya inayowagusa watanzania kwenye masuala ya Serikali umefanikiwa jambo kubwa. Wakati tunaanza sisi ilikuwa ni mashambulizi jambo gani

hili na nini? lakini tume – *force* mpaka nishati ya kupikia ni mjadala sasa hivi. Kwa hiyo tumeanza mjadala, tumekuja tafakuri sasa tunaenda kwenye hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumefurahi sana kwamba Waheshimiwa Wabunge wamehamasika, wameelewa, wameibeba ajenda hii kwa sababu inagusa watu wao. Na pia tumepanua wigo wa masuala sisi wanasiasa ya kuzungumzia kuhusu wanawake, kwa sababu nyuma ilikuwa ni unyanyasaji wa kijinsia, uwezeshaji wa kiuchumi, maji. Kwa hiyo masuala ya wanawake tulikuwa tunazungmza siasa na kwenye majukwaa ilikuwa ni *narrow,* sasa tumeongeza jambo jipya juu ya nishati ya kupikia ambalo tukilifanya vizuri wote tunapata manufaa ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Lakini pia tunamwezesha mtoto wa kike na yeye kufikia pale anapostaili kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili jambo ni gumu, si jepesi ni gumu. *Substation* tutajenga, umeme tutaweka mkandarasi atapeleka vijijini sijui bwawa litajengwa ni mambo ya kiufundi ukiwa na hela, ukiwa na mkandarasi linaenda. Suala linalohusu tabia, linahusu mazoea, linalogusa kila nyanja siyo jepesi kwa sababu linahitaji elimu sana, uwekezaji mkubwa, mabadiliko ya sera, mtazamo na kadhalika. Kwa hiyo siyo jepesi, linahitaji sisi sote tuunganishe nguvu. Ndiyo maana Mheshimiwa Rais alivyoamua kuongoza jambo hili sisi tumepata Faraja, na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge na nyie mlipo libeba tumepata faraja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sasa tumeamua kufanya jambo hili kwa sababu hiyo hiyo, kwamba ni gumu. Wakati mwingine unaamua majambo siyo kwa sababu ni mepesi bali kwa sababu ni magumu ili kupima kiwango na nguvu yenu kama Chama kama Serikali ya kuleta mabadiliko chanya kwenye jamii. Kwa hiyo hili ni kipimo chetu kuchukua jambo ambalo ni *it intellectually challenging* ni *challenging* kisera, kiutamaduni lakini linaleta ustawi wa watu. Kwa hiyo ningependa Waheshimiwa Wabunge tulibebe wote ili tuweze kuwasaidia akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu na kumpongeza kwa sababu yeye ndiye Mwenyekiti

wetu wa Kamati ya Kitaifa ya kufanya jambo hili. Ametuongoza, tumekaa vikao vinne. Sasa hivi tunayo rasimu ya mwisho ya dira, tunayo rasimu ya mwisho ya mpango mkakati unao elezea hatua kwa hatua nani afanye nini na kwa wakati gani ili tufike kwenye yale maelekezo ya Mheshimiwa Rais ya asilimia 80 ya Watanzania watumie nishati safi ndani ya miaka 10. Sasa moja ya mathalani tuliyofanya tunataka, tutagawa nishati hii mitungi, tutafunga mifumo ya kupikia kwenye Taasisi zetu mbalimbali hatuoni aibu, hatuogopi kuwapa Waheshimiwa Wabunge nyenzo ya kuhamasisha. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wana ushawishi. Ukitaka jambo lako lifike nchi nzima kwa wakati mmoja wape Wabunge kwa sababu wanafanya mikutano na wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulisema hata kwenye bajeti mwaka jana, tulitenga na fedha hapa hapa mkapitisha ya mitungi laki moja. Hii tuliyowapa ni sehemu ya mitungi laki moja tuliyoipangia kwenye bajeti. Na utaratibu wa manunuzi umefanyika watu wameshindanishwa. Mtapata mitungi, kama msambazaji wa Kanda ya Ziwa ni fulani na anauwezo na kanda ile tutafanya, kwa wengine watagawiwa na mtu nyanda za kusini kama kampuni fulani ni u-*strong* upo. Kwa hiyo wale waliyokuwa wanasema hakuna maeneo ya ujazaji yapo kwa sababu waliyoshinda katika maeneo yenu ni wale wenye mtandao wa usambazaji katika maeneo yenu; kwa hiyo limefanyika, kwa hiyo tutaendelea leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la wafanyakazi wa *TANESCO* limezungumzwa na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge hapa. Naomba niseme tu kwamba Shirika linapitia katika mabadiliko. Kuna masuala ambayo *TANESCO* tunaka ifanye, kuna matarajio tuliyonayo juu ya *TANESCO,* lakini vilevile kuna mahitaji ya uchumi mpya ya teknolojia mpya. Sasa, haya mabadiliko niseme wazi hapa hayana nia ya kupunguza mtu, hatutapunguza mtu, hatutapunguza mtu kazi *TANESCO*. Ila tutawahitaji wawe tayari kupokea ujuzi mpya na majukumu mapya yanayoendana na mahitaji ya dunia mpya vilevile, waondoke katika *comfort zone* kwasababu dunia ya huduma inabadilika, umeme ni huduma. Kwa hiyo tutawa-*retrain*, tutawawezesha lakini tutakuwa nao. Mtu

ataacha kazi kwa kutaka yeye mwenyewe, hatoondelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na wao wanajua wafanyakazi wa *TANESCO,* kwa mara ya kwanza katika miaka 17 tumewapandishia mshahara juzi. Miaka 17 hatukupandisha mshahara, sasa hivi tunapimana kwa matokeo, na *jam* ndiyo dunia ya kisasa, tunapimana kwa matokeo. Kwa hiyo naomba msiwe na wasi wasi mambo yatakuwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu vinasaba tumelisikia lipo Serikalini linashughulikiwa, tutahakikisha kwamba suala hili linakaa mahala ambapo litakuwa na tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, umeme vitongojini. Waheshimiwa Wabunge hili ni jambo kubwa vilevile, ndoto yetu sisi ni kupeleka umeme kwenye kila kona ya nchi yetu. Mnafahamu vijiji vyote tutamaliza, vimebaki vijiji 2,000. Kila kijiji kina mkandarasi na kazi inaendelea. Lakini kama mnavyofahamu kila kijiji kina wastani wa vitongoji vitano. Kwa hiyo tunaposema tumepeleka vijiji vyote ni maana katika kitongoji kimoja katika vitongoji vitano kwenye kila kijiji. Sasa mtu atakupa kura kwa kumletea umeme karibu na alipo. Kura ukimwambia bana ule palee *you know* usiwe na wasi wasi umeuona ule tumefanya kazi nzuri; Hapana, lazima uwe pale, na huo ndiyo mwelekeo. Uwekezaji wa kuusogeza ili tuupeleke kwenye vitongoji kwa sababu lazima utue kijijini ili usambae. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi kubwa sana imefanyika chini ya Serikali ya Awamu ya Nne ya Tano na ya Sita, kazi kubwa sana imefanyika lazima tujisikie fahari kwamba tumemaliza vijiji lakini kazi kubwa ipo mbele yetu. Sasa sisi tulifanya utafiti tulipoingia tu kwenye nafasi hii, ni nini kinahitajika kupeleka umeme vitongoji vyote? fedha, vifaa, muda, rasilimali watu; tukapata huo uchambuzi tukatengeneza mpango lakini kwa kujua kwamba hatuwezi kwenda Hazina kusema haya hiyo tupeni fedha, tukaja pia na maarifa ya chanzo cha kugharamia pia huo mradi. Tukajadiliana ndani ya Serikali na kuchakata na kuangalia mahitaji mbalimbali. Tulikuwa tuanze mwaka huu wa fedha

unaokuja lakini busara ikatamalaki kwamba chanzo kile kitumike jambo jingine, mambo mengine muhimu zaidi na sisi tuanze *program* yetu mwaka kesho kutwa unaofuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninapenda niwape Waheshimiwa Wabunge faraja kwamba mpango wa kupeleka umeme vitongoji vyote haujafa tumeuharisha kwa mwaka wa fedha unaokuja tutaenda kwenye mwaka unaofuatia. Ila sasa tumeona basi walau tuwape *starter (appetizer)* ndiyo maana ya vitongoji vipo kumi na tano. Tunajua havitoshi, lakini sisi vitatusaidia kuangalia utaratibu na namna bora zaidi tutakapofanya ule mradi mkubwa ya kufika. Imani yetu ni kwamba katika vitongoji 15 tutachagua maeneo yenye mahitaji zaidi, maeneo ya huduma, maeneo ya uzalishaji mali, maeneo ya uchumi kwenye minara ya simu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii ya vitongoji 3,000 kwa ujumla ukipiga si vidogo kwa sababu mahitaji ni sawa na yale yale ya nyuma ya kupeleka umeme katika vijiji. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge naomba tukubali kwamba tutaendelea na utaratibu wa kujiandaa kwa mwaka unaofuatia. Bahati nzuri sisi tuko tumeishaweka mipango yote ikiwemo namna ambavyo vifaa vitapatikana, namna ambavyo vitasambazwa, utaratibu mpya wa manunuzi tutakapokuja kwenye huo mradi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni masuala mbalimbali ambayo ni mahusisi yaliyozungumzwa. Watu wa Mtwara tumewasikia Msimbati, Madimba kwa kweli tutaleta maendeleo pale kwa sababu hakubaliki kwamba panatoa gesi halafu pako vilevile. Ule mtambo tuliyoahidi kwenda Mtwara umeishafunguliwa mafundi wako Mtwara kazi inaendelea. Wahadzabe Mheshimiwa Flattey nimeona umesema weka historia wapelekee Wahadzabe umeme. Niseme tu kwamba kabla ya Desemba tutawapelekea umeme wa *solar* uko waliko. Tutaanza na *solar* kwanza tuone, kwa hiyo tutawapelekea *solar.* Mheshimiwa Cherehani timu nzima na Mheshimiwa Iddi Kassim timu nzima ya *TANESCO* na *management* itakuja Kahama na kukaa na Uongozi wa Mkoa na Wilaya kuangalia mahitaji mahususi ya pale. *Cable* Zanzibar tutaweka *cable* mpya Zanzibar ya kutoa umeme Bara na

kupeleka Zanzibar. Tunafanya upembuzi yakinifu ili kuongeza uwezo wa umeme kutoka Zanzibar. Naomba nirudie; tutaweka *cable* mpya ya kupeleka umeme Zanzibar chini ya Bahari. Mheshimiwa Bidyanguze tumepokea, tumesikia waambie watu wako wasiwe na wasi wasi *greed* Katavi inakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho tu niseme kwamba Waheshimiwa niongee na Wananchi wa Tanzania moja kwa moja kupitia Mheshimiwa Spika kwamba mmewasikia Wabunge wenu na kwa bahati mbaya hapa sikuweza kuwajibu wote ila naomba niwahakikishie kwamba tumewajibu Waheshimiwa Wabunge wenu kwa majibu yanayotatua changamoto walizozisema kwetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kama Waheshimiwa mnatusikiliza, mmemsikia Mheshimiwa Mbunda pale amezungumza umeme, Kapinga kule Mbinga kwa sababu sijamtaja lakini nimemjibu na nimemueleza lini umeme utafika. Kwa hiyo majibu hayo tumeshawafikishia, kwa hiyo msiwahukumu Waheshimiwa Wabungwe wenu kwamba mbona Waziri kasimama hajakutaja. Muda hautoshi ila tumewajibu Wahehsimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, mwisho kulikuwa na maneno mengi ya faraja kwetu katika mjadala huu; yametutia moyo, tumeyapokea, tumefurahi. Hatukutegemea kwamba Bajeti yetu ingekuwa na hamasa na shamra shamra na pongezi kiasi hiki, tumefurahi. Tumesikia maneno Mheshimiwa Mzee wangu Mzee Deo Sanga, mdogo wangu Mheshimiwa Tauhida kwamba hayo maneno yanayosemwa msiyasikilize kabisa.

Mheshimiwa Spika, sisi tunayasikiliza. Naomba nitofautiane nao, tunayasikiliza kwa sababu yanatusaidia. Tunayasikiliza, hayatutoi relini ila tunayasikiliza. Tunayasikiliza kwa sababu kwanza yanatuongezea umakini. Unajua mtu akiwa anakusema kwa maneno ya uongo, anakusingizia mambo, mnakaa na wenzako jamani mnaona haya. Hebu tusije tukafanya mambo ya hovyo halafu ikaja ikaonekana ni kweli. Kwa hiyo tunashikana, na inatusaidia kuwa makini. Unajua ukiwa unamulikwa unakuwa

makini. Kwa hiyo haya maneno yanatufanya saa zote tuwe macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili haya maneno yanatuongezea hamu na hamasa ya kupata matokeo. Sisi hamasa yetu ni imani ya Mheshimiwa Rais kwetu, hamasa yetu ni matokeo ya kazi yetu kwa uhai wa chama chetu, hamasa nyingine ni kuwasaidia Watanzania kwa majukumu tuliyopewa. Lakini hamasa ya mwisho ni maneno haya, kwa sababu si unataka upate matokeo? Mtu akikusema wewe hufai, maana yake unajitahidi ili uonekane unafaa. Kwa hiyo haya maneno yanatusaidia ndio maana tunayasikiliza. Lakini pia haya maneno yanatusaidia kwa sababu yanawaamsha wanaotupenda na wanaotutakia kheri ili watuombee dua na sala. Kwa sababu ukisemwa sana, rafiki zako, ndugu, jamaa watasema Mungu msaidie, msaidie, wanaamka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hii pia inatusaidia sala na dua zinaongezeka. Kwa hiyo tunayapenda. Lakini mwisho yanatusaidia kwa sababu yanatufundisha kuwa na subira, yanatufundisha kuwa na ukomavu, yanatufundisha kuwa na uvumilivu ili tuwe viongozi bora zaidi. Maneno haya yanatusaidia kwa sababu yanatufundisha ukomavu, yanatufundisha kuwa na subira, yanatufundisha kuwa na uvumilivu na yanatujenga kuwa viongozi bora zaidi. Kwa hiyo sisi tunasema waendelee kwa sababu yanatusaidia.

Mheshimiwa Spika, sisi kisasi chetu ni matokeo, ndio mwisho. Naomba nirudie, hatutabishana, hatutatupa maneno, hatutajitetea, tutalipa kisasi kwa matokeo. Na tunaomba Mwenyezi Mungu atupe afya na uhai tuendelee kuruzukiwa na imani ya Mheshimiwa Rais na tutapata matokeo, tutakuwa tumetimiza mchango wetu kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**: Mheshimiwa Spika, naafiki

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Nilikuwa nasubiri kuwe na utulivu ndipo niseme tukae. *(Kicheko)*

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 5,090,722,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na makofi yote yale naona kuna majina hapa yanataka ufafanuzi, sijui wanataka kufafanuliwa nini; lakini ni haki yao. Kifungu hiki kina mshahara wa Waziri na kuna Waheshimiwa Wabunge wanahitaji ufafanuzi kila mmoja wao jambo moja la kisera na liwe mahususi. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya kwamba ujumbe wangu umechelewa, nilikuwa nataka ufafanuzi kwenye eneo la *CSR* kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere, lakini limefafanuliwa vizuri, naomba kujiondoa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Jana wakati nachangia niliongelea habari ya mradi wa *LNG,* nikipongeza juhudi kubwa za Serikali ambazo zimefanyika kwa sababu ni mradi wa kihistoria ambao utatutoa hapa. Niki-*refer* katika hotuba ya Waziri amesema tayari kuna mikataba ambayo imeandaliwa mkataba wa nchi hodhi na mkataba wa uendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu na *TPDC* ni mbia katika mradi huu, hasa katika upande wa uendeshaji, nilitaka kujua *commitment* ya Serikali, kwamba mmejipangaje hasa kwenye kulinda maslahi ya umma, ili tuweze kupata faida nzuri Zaidi kama Taifa, hasa kwenye hiyo mikataba ambayo umesema inaandaliwa inataka kufanyikwa kazi baadaye. Mimi langu ni hilo tu, nipate ufafanuzi hapo.

**MWENYEKITI:** Nilikuwa najaribu kuwaza ungependa kujua yaani kwamba ule mkataba una vipengele vya kulinda hicho unachokisema?

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ninachotaka kujua, kwa sababu amesema tayari mikataba imeandaliwa, wao kama Wizara; yaani vipengele, kwa sababu tulikuwa na shida ya mikataba hapo nyuma, ambapo unakuja kukuta baadhi ya maslahi ya umma hayajazingatiwa; sasa nataka kujua wao katika mikataba hii ambayo anasema imeandaliwa wamezingatiaje maslahi ya umma kwa ajili ya manufaa ya watanzania kwenye mradi huu mkubwa wa gesi?

**MWENYEKITI:** Sawa, sasa kwa sababu Bunge linayo mamlaka likitaka hiyo mikataba, nachelea, kwa sababu Waziri siye anayeshughulika na vile vipengele vya mikataba, tukimwambia hapa vimeandikwaje vile na yeye akatujibu, halafu baadaye tuje tuitishe ile mikataba tukagundua mambo mambo. Nadhani tujipe muda, kama tunahitaji hiyo mikataba kuitazama sheria inaturuhusu tunaweza kufanya hivyo.

Lakini nachelea kumwambia Waziri hapa halafu apige maneno ambayo tunaweza tusiyaelewe kwenye ile mikataba

halafu bado tukawa na taarifa huku Bungeni kwamba aliyewahi kuzungumzia hii mikataba na tukamuelewa na wewe ukaacha hoja yako kwa sababu wewe wenyewe mkataba hujausoma, Waziri mwenyewe huenda vipengele havijui halafu tukazungumza hapa bila taarifa mahususi.

Lakini Mheshimiwa Ezra, hoja yako ni ya msingi ila kwa sababu sheria inaturuhusu sisi kuitazama hiyo mikataba tunaweza kutumia njia hiyo ili tutazame kiukamilifu kama kuna changamoto yoyote kwenye hilo eneo. Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kubwa la Wizara hii ni kufikisha umeme kwa wananchi; na tulivyoona utendaji wa *REA*, ni kwamba wenyewe unapeleka umeme vijijini, kwenye Kijiji; lakini ipo kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji na kwa bahati mbaya, hakujawa na wandarasi wa kupeleka umeme kwenye vitongoji. Umeme unaishia kijijini na mkandarasi anaishia pale kwenye Kijiji lakini sasa *distribution* kwenye vitongoji jambo hili halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka Mheshimiwa Waziri atupe maelezo kidogo kwamba programu ya kupeleka umeme kwenye vitongoji imekaa katika mtindo upi? Je, *REA* itaanza kupeleka wakandarasi kwenye vitongoji au kwa sasa inavyofanyika ambayo naiona *pace* yake haiendi na matarajio makubwa ambayo tunataka vitongoji hivi viweze kupata umeme?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwenye kitabu chako kuna hayo maelezo lakini Mheshimiwa Mbunge inawezekana hicho kisehemu cha sehemu ambayo imeandikwa hayo maelezo Mbunge hajakiona. Kwa hiyo hakuna ubaya kwenye wewe kueleza kwamba pesa zimetengwa kwa ajili ya hiyo kazi. Haya, nani anafafanua kati yenu? Mheshimiwa Naibu Waziri, ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwenye bajeti yetu tumesema mwaka wa fedha unaokuja tumetenga bilioni 377 kwa ajili ya kuanza upelekaji wa umeme kwenye vitongoji; na kwa kuanzia vitongoji angalau 15 kwa kila jimbo, wala siyo wilaya kwa kila Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitamani tufanye zaidi lakini unashona suti kulinganna na ukubwa wa kitambaa ulichonacho. Sasa kitambaa cha mwakani kinalingana hivyo lakini kama Mheshimiwa Waziri alivyoeleza tunatarajia kwenye mwaka ule mwingine unaokuja tutapata pesa nyingi Zaidi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji vyote. Sasa utaratibu tutakuwa tumeuona vizuri baada ya mwakani kuwa tumejifunza namna bora zaidi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji hivi vya kuanzia, 15 kwa jila Jimbo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nilikuwa najua tunaangalia kitambi, kumbe tunangalia ukubwa kitambaa, sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Lakini nafikiri Mheshimiwa Naibu Waziri kwa ufafanuzi ulioutoa kwa hapo baadaye, kwa mwaka huu ni sawa, kwa hapo baadaye kuna majimbo ambayo ni makubwa na majimbo mengine yana kata nne, tano kwa hiyo ni dhahiri hawawezi kulingana kwa maana ya ukisema wanapeleka tu vitongoji 15 kila Jimbo.

Jimbo moja lina kata arobaini na ngapi? Sijui arobaini na mbili, jimbo lingine lina kata sijui thelathini na ngapi, jingine lina kata tano kwa hiyo hawawezi kulingana kwa hiyo kwa huko baadaye muanze kuyatazama haya tayari ili muwe mnapeleka umeme kwa uwiano wananchi wote wapate kwa wakati huo. *(Makofi)*

Haya, kuna jina jina lingine hapa. Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Wakati nachangia niliainisha kadhia ambao wananchi wanakumbana nayo kupitia kodi ya majengo ambayo inakusanywa na hawa *TANESCO*. Ambapo tulisema kwa nyumba za kawaida zinatakiwa zilipe shilingi 1,000, kama sijakosea, kwa ghorofa ilikuwa ni 5,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa nataka uafafanuzi wala sitaki kushika shilingi yake. Nilikuwa nataka nijue ni lini sasa Serikali itafanya *reconciliation* ili kuweza kujua bayana kodi za ziada ambazo zimechajiwa kwenye zile nyumba ambayo unakuta ina mita Luku zaidi ya kumi au nane au moja, unatakiwa uchaji moja tu maana shilingi 12,000 au shilingi 60,000 lakini unakuta wamechajiwa zaidi. Sasa nakataka nijue lini *reconciliation* itafanyika ili kwa wale ambao umekuta wamechajiwa zaidi ili waweze kufidiwa hizo gharama kupitia *unit* za *TANESCO*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hilo tu.

**MWENYEKITI:** Sasa nilikuwa natafakari hii ni Wizara hii inatakiwa kutoa ufafanuzi kweli, ile pesa inakusanywa na nani? Na *TANESCO*? Ngoja Mheshimiwa Esther Matiko, ile fedha inaenda Wizara gani?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanakusanya *TANESCO,* kupitia Luku yaani unavyonunua ile…

**MWENYEKITI:** Wanakusanya *TANESCO* kwa ajili ya nani? Zile pesa zinaenda wapi? Ndio nataka kujua. Kwa sababu lazima huyo zinayeenda hela kwake ndiye atoe taarifa huku kwa sababu…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hapana wakusanyaji ambao ndio *TANESCO* ndio wanajua kabisa mteja A ana mita kumi na mbili lakini kiuhalisia hizi mita zimewekwa kwenye jengo moja.

**MWENYEKITI:** *TANESCO* wanao uwezo wa kujua, wakati ukichangia uzuri nilikuwa mimi mwenyewe nimekaa hapa, ukaeleza kwamba mwekezaji ana nyumba mbalimbali, zile nyumba pale zina yaani labda hati yake ni moja lakini nyumba ziko, halafu hizo nyumba kila nyumba ina Luku yake, nilikuelewa vizuri au Hapana?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano nina jengo moja nimeweka ni mafremu yapo, mathalani ni jengo moja lakini limewekwa fremu kama 12 na kila fremu ina mita LUKU yake moja. Kwa hiyo wale wanatakiwa, wachangie 12,000 tu; lakini wanachangia kwa LUKU.

**MWENYEKITI:** Ngoja twende vizuri, taratibu tu. Sasa hivi umesema lile jingo lina mita luku moja. Kama linayo moja maaa yake hapo hakuna shida. Zikiwa nyingi ndio kuna shida?

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *concept* iko hivi. Inachajiwa shilingi 12,000 kwa mwaka, kwa jengo. Ni kodi ya majengo. hawakusema kwa Luku ambayo inatolewa?

**MWENYEKITI:** Ambayo kodi ya majengo *TANESCO* siku hizi wanakusanya kodi ya majengo? Yaani hii kodi ya majengo ni ya kwao? Ama kuna taasisi…

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzoni walikuwa wanakusanya *TRA*…

**MWENYEKITI:** Ngoja tuelewane. Wale wanaotaka fedha wanatumia LUKU ya *TANESCO*. Mimi nataka nielewe tu hapo. Fedha zile ni za mtu wa umeme au? nataka nitafute hapa nani wa kujibu hoja yako.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *the proper* mtu wa kujibu hoja yangu ni *TANESCO*. Kwa sababu wao wametumika kama *collecting agent*. Mwanzoni walikuwa wanakusanya *TRA* wakasema hamna *effective* kwenye kukusanya, wakaielekeza *TANESCO* ndiyo inakusanya, kwa hiyo lazima *TANESCO* ndio inafanya hiyo *reconciliation*.

**MWENYEKITI:** Haya, tuanze na wewe ama tuanze na *TANESCO?* Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii. Mheshimiwa Mbunge ana hoja ya msingi, kwamba utaratibu huu kwa sababu tuliuanza mpya, ni kweli

tuliweka *prorate,* kwa maana ya viwango vya nyumba ambayo ni ya aina moja pamoja na zile za ghorofa. Lakini pia yalijitokeza mazingira ya eneo ambako mmiliki wa nyumba ni mmoja lakini wakazi wa ndani yake wameamua kugawana Luku. Kwa maana hiyo kwa utaratibu nyumba kama nyumba moja ile ilitakiwa itozwe tozo moja; lakini kwa sababu wakazi wa ndani ya ile nyumba wameamua kugawana Luku kwa maana hiyo unakuta kila mmoja amelipishwa kama ana nyumba yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo tulitengezeza timu ya Wizara zote ambazo zinaguswa, tukisaidiwa na takwimu mpya zilizopatikana za upande wa sensa kuhusu makazi, na tunatarajia tunaposoma bajeti mpya tutaelezea kitu ambacho kipya ambacho kimefanyika kuhusu masuala haya ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Luku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge ana hoja ya msingi lakini asishike shilingi hili jambo tumelifanyia kazi kwa sababu lilikuwa na mapungufu ambayo yalikuwa yamejitokeza.

**MWENYEKITI:** Ndiyo maana nilikuwa na maswali mengi. Nilikuwa najiuliza kama inafafanua Wizara hii au Wizara ambayo imeilekeza Wizara hii kutumika kukusanya hizo fedha. Lakini nashukuru kwa huo ufafanuzi maana yake huko baadaye Serikali inabidi ifanye utaratibu mzuri ili hawa watu wasiwe wanalipa kodi moja, vichwa vingi wakati alipaswa pengine mtu mmoja au mmiliki au kitu kama hicho.

Waheshimiwa Wabunge hayo ndio yalikuwa majina niliyokuwa nayo hapa mbele, yaliyokuwa yanataka ufafanuzi na kwa kuangalia muda wetu pale tunaenda kwenye mafungu.

Katibu.

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*......................................Sh. 5,090,722,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*..............Sh. 1,201,862,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................Sh. 1,603,581,000
Kifungu 1004 – *Internal Audit Unit*……...........................Sh. 644,707,000
Kifungu 1005 – *Legal Service Unit*……………….........Sh. 605,927,000
Kifungu 1006 – *Government Communication Unit*.....Sh. 586,420,000
Kifungu 1007 – *Procurement Management Unit*…........Sh. 17,052,000
Kifungu 1008 – *Environment Management Unit*….......Sh. 444,268,000
Kifungu 1009 – *Management Information System Unit*…....................................................Sh. 647,876,000
Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*…...........................................Sh. 56,215,488,000
Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*……………….....Sh. 20,271,795,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 58 - Wizara ya Nishati**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*...................................Sh. 20,500,000,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…................Sh. 1,200,000,000
Kifungu 3001 – *Electricity and Renewable Energy*…….................................…Sh. 2,858,558,773,200
Kifungu 3002 – *Petroleum and Gas*………………......Sh. 80,444,047,800

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa hoja, taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi limekamilisha kazi zake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiw Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji, Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Wizara ya Nishati kuhusu makadilio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 waseme ndiyo. Wasioafiki waseme siyo. Hakuna, wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana. Mheshimiwa Waziri wa Nishati, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na viongozi wote wa Wizara hii na watendaji wote ambao baadhi yao wako hapa wakiwakilisha wenzao, maana wasingeweza kuja wote maana umeme humu ndani ingekuwa mtihani. Kwa hiyo tunawapongeza kwa kazi nzuri mnayoifanya ambayo imepelekea makofi kuwa mengi namna hii na bajeti yenu kupitishwa na Bunge kwa asilimia 100.

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Yalipitishwa na Bunge)*

Kwa hiyo, nitumie fursa hii kutangaza rasmi kwamba makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 ya Wizara ya Nishati yamepitishwa rasmi na Bunge. *(Makofi)*

Wahehsimiwa Wabunge pia nitumie nafasi hii kuwashukuru sana Kamati yetu ya Nishati na Madini. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wote kwa kweli kwa kuisimamia vizuri Wizara hii mpaka tumefika sehemu ambayo na wao wanapata pongezi za kutosha kabisa. Kwa hiyo tunawashukuru sana viongozi wetu ambao mnatuongoza kwenye kamati hiyo mmefanya kazi nzuri sana kufika kwenye hatua hii.

Lakini wakati huo huo niipongeze pia Wizara kwa kushirikiana vizuri sana na kamati kwa sababu kufikia hatua hii siyo kazi nyepesi. Inaonekana mambo ambayo kamati inashauri mnayafanyia kazi na yale ambayo Wabunge wanawashauri mnayafanyia kazi na hapa mmeahidi kuyafanyia kazi mambo ambayo Wabunge wote wameyasema na tunawatakia kila la kheri katika kutekeleza ahadi zenu ambazo mlizisema wakati wa kusoma makadilio ya mapatio na matumizi lakini pia ahadi mlizozitoa hata ambazo hazipo kwenye bajeti yenu. Kwa hiyo tunawatakia kila la kheri kwenye utekelezaji na kwa kweli tuna matumaini makubwa kenye sekta hii katika mambo yote.

Waheshimiwa wabunge kuna ujumbe nililetewa hapa na Mheshimiwa Mbunge na mimi nimpelekee Mheshimiwa Waziri. Kwa sababu ile mitungi na yale majiko hayana namna ya mnunuzi kujua ujazo wa mule ndani. Kwa hivyo upo uwezekano kwa sababu ile mitungi ni mizito na yale majiko pia yana uzito fulani, mteja anapokwenda kununua hawezi kujua kama ule ujazo alioambiwa ndiyo uliomo kwenye ule mtungi ama kwenye lile jiko.

Kwa hiyo Mbunge alikuwa ameandika hapa kusema kwamba wako wananchi huenda wanaibiwa kwa maana ya kwamba wanaweza wakaambiwa ni kilo 15 mtungi huu, lakini kumbe ndani kule hakuna hiyo gesi ya kiasi hicho. Kwa hiyo sijui mtafanyaje; na kwa ubunifu mlioonesha kwenye maonesho haya,

naamini mtatafuta namna ya huyu mteja kujua kwamba kile anachonunua ndiyo kiasi halisi. *(Makofi)*

Lakini sasa na mimi niongeze hapo kidogo kwa sababu nia ile ya nishati safi ya kupikia ni pamoja na huyu mtu kuweza kujua sehemu ya kwenda kujaza kama ulivyosema hawa watu wako kila mahali lakini ile gesi inaweza kuisha muda ambao yeye ndiyo anasonga ugali pale. Sasa ataanza kukumbuka ningejua ningekusanya kuni, ningejua ningejua mkaa maana mkaa ukiwa unaisha unauona, lakini gesi ikiwa inaisha huioni sasa kwa nia ile ile ya kutaka nishati safi ya kupikia lazima ubunifu muongeze ili huyu anayetumia hiyo nishati safi kama ambavyo mtumiaji wa umeme anaona zile *units* zinavyokwisha anaweza kuongeza.

Huyu wa gesi na yeye aweze kuona kwamba sasa gesi yangu inaelekea mwisho niweze kununua mapema. Itamsaidia sana ili asiweze kupata changamoto yale mazingira ambayo tunafahamu kwa kule kijijini ambao ndio hasa tunataka watumie nishati hii kama baadhi ya maeneo ya mjini, lakini pia wa mijini wabadilike ni pamoja na kuweka mazingira rafiki zaidi ili yule anayetaka kupika chai ya mgonjwa asubuhi sana basi asiwashe halafu anashangaa haiwaki kumbe ndio imekwisha. Na ndiyo atakuwa amekwama na mkaa hana tena ndani. Kwa sababu ameshahama tena huko. *(Makofi)*

Kwa hiyo ule ubunifu mliyoonesha naamini hili nalo mnaweza kabisa, kuweka mazingira ambayo mtumiaji atajua sasa jiko langu linaishiwa au yule ambaye ana mtungi atajua mtungi wangu unaelekea mwisho.

Tunawatakia kila la kheri katika hayo yote. Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa shughuli yetu ya leo na hivyo nihairishe shughuli za Bunge mpaka kesho saa 03:00 Asubuhi.

*(Saa 1.45 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 2 Juni, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*